# KANISA LA MUNGU LA MASALIO



MaarifaMtandaoni.Com | SamaritanLaymenMinistries.Org

# Title:Kanisa la Mungu la Masalio

Translated from GODS REMNANT CHURCH
Jersey, 2025 Marekani

Angalia Vitabu vingine katika Website ya
RohoYaUnabii.Org
Au
MaarifaMtandaoni.Com

Au
SamaritanLaymen.Org

Ellen G. White

1950

**Shukurani:**

**Kwa Mwenyezi Mungu, Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Wahakiki Washauri, Wataalamu wa Teknolojia, na Watia Moyo Wote**

- Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani
    - Rachel Patrick Atandi- Nairobi, Kenya

- Niwael Mburuja-Kilimanjaro, Tanzania
- Judi na John Mugane-Boston, Marekani
- Sandra Barron-Carolina, Marekani
- Daniel Masaka-Kisii, Kenya
- Denis Masaka-Jersey, Marekani
- Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
- Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
- David Masaka-Carolina, Marekani

**Angalia video fupi: https://youtu.be/uiCgNgG9q9E**

# Title:Kanisa la Mungu la Masalio

Ellen G. White

1950

**MWANDISHI WA KALAMU YA MATUMAINI**

Inaaminika kwamba E.G.White(1827 – 1915), Mwandishi wa Kalamu ya Matumaini, ndiye mwandishi wa Marekani ambaye kazi zake zimetafsiriwa kuliko za wengine. Kazi zake zimechapishwa katika zaidi ya lugha 160. Aliandika zaidi ya kurasa laki moja kuhusu mada mbalimbali za kiroho na maisha ya kila siku. Akiongozwa na Roho Mtakatifu, alimwinua Yesu na kuelekeza kuwa Maandiko ndiyo msingi wa imani ya mtu.

**Taarifa zaidi**

Kwa maelezo zaidi kuhusu mwandishi, au mashauri, au jinsi wewe unavyoweza kusaidia huduma hii, ya kutafsiri vitabu, tafadhali wasiliana na MaarifaMtandaoni.Com au RohoyaUnabii.Org au UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com. Tunashukuru kwa kujali kwako na maoni yako na kukutakia baraka za Mungu unaposoma.

## Jedwali ya Yaliyomo


Taarifa kuhusu Kitabu hiki .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Dibaji .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Sehemu ya Kwanza - Upendo wa Mungu kwa Kanisa Lake .. **Error! Bookmark not defined.**

Lengo lake Kuu la kujali .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Tofauti zilizo wazi, zilizoamuliwa .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Majaribio ya Kiungu .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Kanisa Mali ya Mungu .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Kutambuliwa na Kanisa Lake .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Walimu Wazuiwe .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Shirika na Maendeleo .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Umoja katika Imani na Mafundisho .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Utangulizi wa Utaratibu wa Kanisa .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Kuingia kwenye Biashara Mpya .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Matokeo ya Juhudi za Muungano .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Kuepuka Hatari za Matatizo .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Wajibu wa Mtu Binafsi na Umoja wa Kikristo .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Mungu Ametenda Nini! .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Sehemu ya Pili – Kanisa la Masalio sio Babeli .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Mshitaki na Kazi Yake ........................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Maelekezo kwa Wanafunzi ................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Usaliti wa Kujiamini ......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Ujumbe wa Uongo ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Mashtaka ya Shetani ......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Ulimwengu Waitwa Kuwajibika ........................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mshtaki Alikemea .............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Neno la Kutia Moyo .......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Kanisa Si Babeli ................................................................. **Error! Bookmark not defined.**
Kazi ya Udanganyifu ......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Kanisa Hai .......................................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mpiganaji wa Kanisa ......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Shetani Ameruhusiwa Kujaribu ........................................ **Error! Bookmark not defined.**
Kanisa Nuru ya Ulimwengu .............................................. **Error! Bookmark not defined.**
Kazi ya Kubomoa ............................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Huduma Iliyoteuliwa na Mungu ....................................... **Error! Bookmark not defined.**
Jihadhari na Walimu wa Uongo ....................................... **Error! Bookmark not defined.**
Mfano Mwingine ................................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mungu Ana Kanisa ............................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Upendo wa Mungu kwa Kanisa Lake ................................ **Error! Bookmark not defined.**
Barua nyingine ............................................................. **Error! Bookmark not defined.**
"Nakemea na kuadhibu" ................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Kanisa Lisivunjwe .......................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Sehemu ya Tatu - Ushindi wa Kanisa ................................... **Error! Bookmark not defined.**
Uhakikisho Unaorudiwa Mara Kwa Mara ......................... **Error! Bookmark not defined.**
Milele katika Msingi wa Kupata ........................................ **Error! Bookmark not defined.**
Jina Letu la Kidhehebu ...................................................... **Error! Bookmark not defined.**
Makao Mkuu ya waadventista wasabato. .......................... **Error! Bookmark not defined.**
Hakuna Shirika Jipya ........................................................ **Error! Bookmark not defined.**
Mungu Yuko Uongozajini .................................................. **Error! Bookmark not defined.**

Ujumbe mnamo 1913 katika Kongamano Kuu la kanisa la waadventista Kikaoni ***Error! Bookmark not defined.**

Matumaini na Ujasiri ........................................................ **Error! Bookmark not defined.**

Wito wa Kuwekwa wakfu tena ........................................ **Error! Bookmark not defined.**

Matokeo ya Kutembea katika Nuru ................................ **Error! Bookmark not defined.**

Usemi wa Kujiamini ........................................................ **Error! Bookmark not defined.**

Ujasiri katika Bwana * .................................................... **Error! Bookmark not defined.**

Neno kwa mtu Binafsi ..................................................... **Error! Bookmark not defined.**

Ushawishi wa Watendakazi Wazee. ................................ **Error! Bookmark not defined.**

"Hata Mwisho" ................................................................ **Error! Bookmark not defined.**

Kuendeleza Ufanisi Kuongezeka .................................... **Error! Bookmark not defined.**

Ahadi ya Ushindi wa Mwisho .......................................... **Error! Bookmark not defined.**

**Dibaji**

Karne moja iliyopita kulitokea kikundi kinachohubiri ujio wa hivi karibuni wa Kristo na kutangaza kwamba Mungu amewaweka katika njia yao kufikia utimilifu wa unabii. Harakati hizo zilijulikana kama Wanamarejeo, ya kuja kwa Masihi, wa siku ya Sabato, na imeendelea kukua tangu mwanzo. Jambo muhimu zaidi ni hili, mafundisho mbalimbali yanayohubiriwa na Waadventista wa Sabato, yamepata nguvu na msukumo unaoongezeka, kulingana na nyakati, kwa kadri miaka inavyozidi kupita. **[GRCsw 4.1]**

Ulikuwepo wakati ulimwengu ulicheka fundisho kwamba mwisho wa dunia unakaribia. Leo sana wachache wanacheka kuhusu hili. Badala yake, kila mahali watu wanaongelea jambo hili kama Waadventista. Mafundisho yetu juu ya Sabato ya Mungu yanapata msukumo mpya kila muongo unaopita, kwani hivi sasa Sabato imefunuliwa kuwa ni ishara kuu na alama ya mtu asiye na sehemu katika uasi wa leo wenye chimbuko lake katika nadharia ya matengenezo. Mafundisho yetu kuhusu asili ya mwanadamu na hali ya wafu yanapata nguvu mpya kama ngome dhidi ya udanganyifu wa umizimu. Shuhuda kwamba mafundisho yetu ni Kweli na ni ya Mungu huzidi kudhihirika. **[GRCsw 4. 2]**

Lakini wapo waliotugeuka (wale waliojitoa kwetu), sio kwa kuamini sana kuwa mafundisho yetu ni ya uongo, bali ni kwa sababu Mungu Ameitelekeza taasisi yenye makao yake makuu kule Washington D.C.(G. C.); na kuwaagiza wale wote wenye moyo wa Kwei au safi(waaminifu) wanaotamani kuwa tayari kwa ajili ya siku ya Mungu watoke na kuanzisha taasisi mpya. Wanaamini kwamba wakati fulani uliopita harakati za majilio zilipoteza kibali cha Mungu hivyo Yeye Aliwakataa. Wanalijuaje hili? Jibu lao ni kwamba roho ya unabii inasema hivyo. Je, ni kweli Roho ya Unabii inasema hivyo? **[GRCsw 4. 3]**

Kurasa zifuatazo kutoka kwenye kalamu ya Ellen G. White zinatosha kusuluhisha suala hili iwapo Mungu leo Anawaongoza watu walewale ambao Aliowaongoza kwa Zaidi ya karne, na iwapo Ataendelea kuwaongoza hadi kwenye kilele cha utukufu. Tunakualika kusoma na kuburudishwa kiroho. Msingi wa Mungu unasimama kwa uhakika-imara **[GRCsw 4.4]**

# Kanisa la Mungu la Masalio (Kanisa la Masalia)

---

## Sehemu ya Kwanza - Upendo wa Mungu kwa Kanisa Lake

### Lengo Lake Kuu la kujali

**Melbourne, Australia**

**Desemba 23, 1892.**

Ndugu Wapendwa wa Konferensi Kuu (General Conference GC):

Ninashuhudia kwa kaka na dada zangu kwamba kanisa la Kristo, Japo limedhoofika na ni lenye kasoro nyingi, hili ndilo kitu pekee duniani ambacho Mungu amekitunukia kujali, upendeleo na heshima Yake kuu [supreme regard]. Huku Yeye Akiendelea kusambaza mwaliko Wake kwa wote ulimwenguni ili waje Kwake na kuokolewa, Yeye anaagiza Malaika Wake watoe msaada kwa kila mwanadamu anayemjia katika toba na majuto, Naye huja binafsi kwa Roho Wake Mtakatifu katikati ya kanisa Lake. "Ee Bwana, toka vilindini nimekulilia. [2] Bwana, uisikie sauti yangu.
Masikio Yako na yaisikilize Sauti ya dua zangu. [3] Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu,
Ee Bwana, nani angesimama? [4] Lakini Kwako kuna msamaha, Ili Wewe uogopwe.
[5] Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja, Na Neno Lake nimelitumainia. [6] Nafsi
yangu inamngoja Bwana, Kuliko walinzi waingojavyo asubuhi, Naam, walinzi waingojao
asubuhi. [7] Ee Israeli, umtarajie Bwana; Maana kwa Bwana kuna fadhili, Na Kwake kuna

ukombozi mwingi. [8]Yeye atamkomboa Israeli na maovu yake yote..”Zaburi 103 **[GRCsw 5.1]**

Wahudumu/wachungaji na kanisa lote, hebu hii iwe lugha yetu, kutoka kwenye mioyo ambayo inaitikia wema mkuu na upendo wa Mungu kwetu sisi kama watu na sisi kila mmoja wetu, “Israeli na imtumaini Bwana tangu sasa na hata milele.” “Ninyi msimamao nyumbani mwa Bwana, nyuani mwa nyumba ya Mungu wetu, msifuni Bwana; kwa kuwa Bwana ni mwema; sifa ni ya Jina Lake; kwa maana inapendeza. Kwa kuwa Bwana amemchagua Yakobo kwa nafsi Yake, na Israeli kwa hazina Yake ya pekee. Maana najua ya kwamba Bwana ni Mkuu, na ya kuwa Bwana wetu Yu juu ya miungu yote.” Fikiria, Ndugu zangu, kwamba Bwana ana watu, watu walioteuliwa, Kanisa Lake, liwe Lake, ngome Yake Mwenyewe, ambayo Yeye anaishikilia katika ulimwengu ulioadhibiwa na dhambi, ulioasi; na hakukusudia kuwa hakuna mamlaka ambayo inapaswa kujulikana ndani yake, hakuna sheria inayopaswa kutambuliwa nayo, bali Yake Mwenyewe tu. Shetani ana muunganiko mkubwa, na kanisa Lake. Kristo analiita sinagogi la Shetani kwa sababu washiriki wake ni wana wa dhambi. [6]Washiriki wa kanisa la Shetani wamekuwa wakifanya kazi isiyokoma, ili kutupilia mbali sheria ya Mungu na kuchanganya tofauti kati ya mema na mabaya. Shetani anafanya kazi kwa nguvu nyingi ndani, na kupitia kwa watoto wa kutotii/uasi, kuinua uhaini na uasi kuwa ndio Ukweli na uaminifu. Na kwa wakati huu, nguvu za uvuvio wake wa kishetani, zinawasukuma mawakala wake walio hai, ili watekeleze uasi mkubwa dhidi ya Mungu, ulioanza mbinguni.**[GRCsw 5.2]**

## Tofauti zilizo wazi, na zilizoamuliwa

Kwa wakati huu kanisa linapaswa kuvaa mavazi yake mazuri—"Kristo haki yetu." Kuna tofauti zilizo wazi, na zilizoamuliwa, na zinazopaswa kurejeshwa na mfano wake kuonekana kwa ulimwengu wote, katika kuzishikilia amri za Mungu na imani ya Yesu. Uzuri wa utakatifu unapaswa kuonekana katika mng'ao wake wa asili tofauti na ulemavu na giza la wasio waadilifu, wale walioasi sheria ya Mungu. Hivyo tunamkiri Mungu, na kuitambua sheria Yake, msingi wa serikali Yake mbinguni na mamlaka Yake duniani kote. Mamlaka Yake inapaswa kuwekwa wazi mbele ya ulimwengu; na hakuna sheria zinazopaswa kutambuliwa ambazo zinagongana na sheria za Yehova. Ikiwa ni kinyume na mipango ya Mungu, basi ulimwengu usiruhusiwe kuathiri maamuzi yetu au matendo yetu, na hivyo kusudi la Mungu liwe limeshindwa. Licha ya umuhimu wa kisingizio hiki,

kama kanisa linatetereka hapa, imeandikwa dhidi yake katika vitabu vya mbinguni usaliti wa amana takatifu zaidi, na usaliti kwa ufalme ya Kristo. Kanisa liko imara na limeamua kushikilia kanuni zake mbele ya sayari zote za mbinguni na falme za ulimwengu; uaminifu thabiti katika kudumisha heshima na utakatifu wa sheria ya Mungu vitavutia macho na kuthaminiwa hata na ulimwengu, na wengi kwa matendo yao mema ambayo watu watakayoyaona, kisha wataongozwa kumtukuza Baba yetu aliye mbinguni. Wale watu waadilifu na wakweli hubeba sifa za mbinguni, na sio za mamlaka za duniani. Watu wote watajua ni nani katika wanafunzi wa Kristo, waliochaguliwa na waaminifu, na watawatambua/watawajua watakapovishwa taji na kutukuzwa kama wale waliomheshimu Mungu na ambao Mungu Amewaheshimu, akiwaleta katika kumiliki uzito wa milele na wa utukufu. . . .**[GRCsw 6.1]**

Bwana amelitunukia kanisa Lake uwezo na baraka, ili liweze kuwakilishwa ulimwenguni, mfano Wake Mwenyewe toshelevu, na ili kanisa Lake liwe kamili katika Yeye, uwakilishi wa kudumu kwa mwingine, hata ulimwengu wa milele, wa sheria ambazo ni za juu kuliko sheria za kidunia. Kanisa Lake linapaswa kuwa hekalu lililojengwa baada ya mfano wa Kiungu, na ubunifu wa kimalaika umeleta fimbo Yake ya dhahabu kupimia kutoka mbinguni, ili kila jiwe lichongwe na kusawazishwa mraba kwa kipimo cha Kiungu/Bwana, na kusuguliwa ili kung'aa, naam ling'ae kama nembo ya mbinguni, ikiangazia pande zote kwa miale angavu na ya wazi ya Jua la Haki. Kanisa linapaswa kulishwa kwa mana kutoka mbinguni, na kuwekwa chini ya ulinzi wa neema Yake tu, Pekee Yake. Yeye Akiwa amevalia silaha kamili za nuru na haki, anaingia juu ya mgogoro Wake wa mwisho. Takataka, na nyenzo zisizo na maana, zitateketezwa, na mvuto wa Ukweli utashuhudia ulimwengu juu ya utakaso, na tabia Yake iliyoinuliwa, na ya hadhi ya juu. . . .**[GRCsw 6.2]**

## Majaribio ya Kiungu-Mitihani ya Mwenyezi Mungu

Bwana Yesu anaijaribu mioyo ya wanadamu kupitia onyesho la rehema Zake na neema tele. Yeye Anaathiri mabadiliko ya ajabu sana kiasi kwamba Shetani, pamoja na majivuno yake yote ya ushindi, pamoja na muungano wake wote wa uovu ulioungana dhidi ya Mungu na sheria ya serikali Yake, anasimama akiwaona kama ngome isiyopenyeka kwa ujanja na udanganyifu wake. Kwake ni mafumbo ya ajabu, siri na mambo yasiyoeleweka. Malaika wa Mungu, maserafi na makerubi, nguvu zilioagizwa na Bwana kushirikiana na mawakala wa kianadamu, wanatazama kwa mshangao na

shangwe, kwamba wanadamu walioanguka, ambao kabla ya hapo walikuwa wana wa ghadhabu, sasa kwa njia ya kufunzwa na Kristo, wanaendeleza tabia za mfano wa Uungu, kuwa wana na binti za Mungu, kutenda sehemu muhimu katika kazi na furaha ya mbinguni.**[GRCsw 7.1]**

Kwa kanisa Lake, Kristo ametoa nyenzo za kutosha, ili aweze kupokea/kuingiza mapato makubwa ya utukufu kutoka kwa wanadamu waliokombolewa, milki Yake aliyoinunua. Kanisa, likiwa limetunukiwa haki ya Kristo, kwenye hazina Yake, ambamo wingi wa rehema Zake, upendo Wake, Neema Yake, viweze kuonekana katika maonyesho kamili na ya mwisho. Tamko hilo katika sala Yake ya maombezi, kwamba upendo wa Baba ni mkuu kwetu kama ulivyo Kwake Yeye, Mwana wa pekee, na kwamba tutakuwa pamoja Naye, pale alipo Yeye, milele tukiwa wamoja na Kristo na Baba, ndiyo mshangao wa Jeshi la malaika wa mbinguni, na ndiyo shangwe yao kuu. Zawadi Yake Roho Mtakatifu, aliye tajiri na kusheheni kwa wingi, Ndiye anapaswa kuwa kwa kanisa Lake kama ukuta wa moto unaozunguka, ambao nguvu za kuzimu hazitashinda [8] dhidi yake. Katika usafi wao usio na mawaa na ukamilifu usio na doa, Kristo anawatazama watu Wake kama malipo ya mateso Yake yote, fedheha Yake, na upendo Wake na nyongeza ya utukufu Wake—Kristo, kitovu/kiini kikuu, ambapo utukufu wote huangazwa. "Heri walioitwa kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo."— *General Conference Daily Bulletin*, 1893, pages 408, 409. Reprinted in *Testimonies to Ministers*, pages 15-19. **[GRCsw 7.2]**

## Kanisa Mali ya Mungu

Kanisa ni mali ya Mungu, na Mungu hulikumbuka daima linaposisima duniani, kwenye vishawishi na majaribu ya Shetani. Kristo hajawahi kulisahau katika siku za kufedheheshwa Kwake. Katika kupita kutoka kwa matukio ya unyonge Wake, Yesu hajapoteza Ubinadamu Wake hata kidogo. Yeye Ana upendo ule ule mpole, wenye huruma, na daima huguswa na ole za mwanadamu. Daima hukumbuka kwamba Yeye alikuwa Mtu tu wa huzuni na sikitiko, na anayejua majonzi. Yeye kamwe Hawasahau wawakilishi Wake wanaojitahidi kushikilia sheria Yake iliyokanyagwa chini. Anajua kwamba ulimwengu uliomchukia, unawachukia wao pia. Ingawa Yesu Kristo amekwenda mbinguni, bado kuna mnyororo ulio hai, unaowafunga waumini Wake

kwenye moyo Wake kwa upendo usio na kikomo. Wale wanadamu wa hali ya chini na dhaifu wamefungwa na mnyororo wa huruma, karibu na Moyo wake. Kamwe Yeye Hasahau kwamba Yeye Ndiye mwakilishi wetu na amebeba asili yetu [ubinadamu].**[GRCsw 9.1]**

Yesu analiona kanisa Lake la Kweli duniani, ambalo matamanio na nia yake kuu ni kushirikiana Naye katika kazi kuu ya kungoa roho. Yeye Anazisikia sala zao, zikiwasilishwa kwa toba (majuto) na nguvu, Na Yeye Mwenye Uwezo usio na kikomo, hawezi kulipinga ombi lao la kusihi wokovu, kwa ajili ya yeyote anayepitia mitihani na kujaribiwa ambaye ni wa mwili wa Kristo. "Basi, iwapo tukijua tunaye Kuhani Mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuguswa na madhaifu yetu; bali Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

"Yesu daima anaishi ili kufanya maombezi kwa ajili yetu. Kupitia Mkombozi wetu, Je, ni baraka gani basi, ambazo muumini wa kweli hawezi kuzipokea? Kanisa ambalo hivi karibuni litaingia kwenye mzozo wake mkali zaidi, litakuwa kitu kinachopendwa zaidi na Mungu duniani. Muungano wa uovu utachochewa na nguvu kutoka chini, na Shetani atatupa lawama yote kadri inavyowezekana kwa wateule ambao hawezi kuwaongopea na kuwadanganya na mavumbuzi na uwongo wake wa kishetani. Lakini Je, Kristo Aliyeinuliwa "kuwa Mkuu na Mwokozi, ili awape Israeli toba na ondoleo la dhambi," Mwakilishi wetu na Kichwa, ataufunga moyo Wake kweli, au kuondoa mkono Wake, au kughairi ahadi Yake? Hapana; kamwe, kamwe.**[GRCsw 9.2]**

## Yeye Anajitambulisha na Kanisa Lake

Mungu ana kanisa. Watu waliochaguliwa; na kama wanadamu wote wangeweza kuona kama mimi nilivyoona jinsi ambavyo Kristo anajitambulisha Mwenyewe kwa ukaribu na watu Wake, hakuna ujumbe kama huo ungesikika, ambao unalishutumu kanisa kuwa ni ovu kama Babeli. Mungu ana watu ambao ni watenda kazi pamoja Naye, na wamekwenda mbele moja kwa moja, wakiwa na utukufu Wake mbele ya macho yao. Sikiliza sala ya Mwakilishi mbinguni: "Baba, nataka wao pia. Ulionipa, wawe pamoja

Nami nilipo; kwamba wao wapate kuutazama utukufu Wangu." Loo, jinsi Kichwa cha Kiungu kinavyotamani kuwa na kanisa Lake pamoja Naye! Walikuwa na ushirika Naye katika mateso Yake na unyonge Wake, na ni furaha Yake kuu kuwa nao pamoja Naye, kuwa washirika wa utukufu Wake. Kristo anadai fursa ya kuwa nalo Kanisa Lake pamoja Naye. "Nataka hao pia, uliowapa Mimi, wawe pamoja Nami mahali nilipo." Yohana 17:24. Kuwa na kanisa Lake pamoja Naye ni sawasawa na kufanya ahadi na mapatano na Baba Yake. Yeye kwa heshima anatoa kwenye kiti cha rehema, ukombozi Wake uliokamilika kwa watu Wake. Upinde wa ahadi huzingira Badala na Mdhamini wetu anapomimina ombi Lake la upendo, "Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja Nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu Wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu.." Tutamwona kwa macho yetu Mfalme katika uzuri Wake, na kanisa litatukuzwa.**[GRCsw 10.1]**

Sisi tunaweza kuomba sasa kama Daudi, "Wakati umewadia Kwako, Bwana fanya kazi; kwa maana wameibatilisha sheria Yako." Wanadamu wameendelea katika uasi wa sheria ya Mungu mpaka wamefikia hatua ya jeuri hiyo isiyo kifani. Wanadamu wanafunzwa kutotii/uasi, na wana haraka inakaribia kikomo cha uvumilivu na upendo wa Mwenyezi Mungu, na hakika Mungu ataingilia kati. Hakika atatetea na kuthibitisha utukufu Wake, na kukandamiza uovu ulioshamiri. Je, watu wa Mungu wanaoshika amri Zake watasombwa na uovu ulioenea? Je, watajaribiwa, kwa sababu ya dharau iliyoenea ulimwengu kote juu ya sheria ya Mungu, kufikiria kwa udogo sheria hiyo ambayo ndiyo msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani? Hapana. Kwa kanisa Lake, sheria Yake inakuwa yenye thamani, takatifu, na yenye kuheshimika zaidi, wakati wanadamu wanaitupia dharau, chuki na kejeli. Kama Daudi, wanaweza kusema, "Wameibatilisha sheria Yako. Kwa hiyo Nayapenda maagizo Yako kuliko dhahabu; naam, juu ya dhahabu safi. Kwa hiyo Ninayahesabu maagizo Yako yote kuhusu kila kitu kuwa sahihi; na Ninachukia kila njia ya uwongo."**[GRCsw 10.2]**

Kanisa vitani sio kanisa lenye ushindi sasa; bali Mungu analipenda kanisa Lake, na anaeleza kupitia kwa nabii jinsi ambavyo Yeye humpinga na kumzuia Shetani, ambaye huwavika watoto wa Mungu katika mavazi meusi mno na yaliyo najisi zaidi, na kuomba fursa ya kuwaangamiza. Malaika wa Mungu walikuwa wakiwalinda kutoka kwenye mashambulizi ya adui. Mtume anasema:**[GRCsw 11.1]**

Kisha akanionyesha Yoshua, kuhani mkuu, amesimama mbele ya malaika wa Bwana, na Shetani amesimama mkono wake wa kuume ili kushindana naye.
2 Bwana akamwambia Shetani, Bwana na akukemee ewe shetani; naam, Bwana, aliyechagua Yerusalemu, na Akukemee; je! Hiki sio kijinga kilichotolewa motoni? 3 Basi,
Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu sana, naye alikuwa akisimama mbele ya malaika.
4 Naye huyo akajibu, akawaambia wale waliosimama mbele yake, akisema, Mvueni nguo hizi zenye uchafu. Kisha akamwambia yeye, Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi. 5 Nikasema, Na wampige kilemba kizuri kichwani
pake. Basi, wakampiga kilemba kizuri kichwani pake, wakamvika mavazi; naye malaika wa Bwana akasimama karibu. 6 Kisha malaika wa Bwana akamshuhudia Yoshua,
akisema, 7 Bwana wa majeshi asema hivi, Kama ukienda katika njia Zangu, na kama ukishika maagizo Yangu, ndipo utakapoihukumu nyumba Yangu, nawe utazilinda nyua Zangu, nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu. **[GRCsw 11.2]**

## Walimu Waepukwe/Wazuiwe

Wanapotokea wanadamu, wanaodai kuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu, lakini badala ya kupigana na falme na mamlaka, na watawala wa giza wa dunia hii, wao huchimba mahandaki ya mraba, na kuzigeuza silaha zao ili kupigana vita dhidi ya wapiganaji wa kanisa, basi wewe uwaogope wanadamu kama hao. Watu hawa hawana sifa za Kiungu/mbingu/Bwana. Mungu hajawakabidhi mzigo wowote wa kazi, kama huo. Hakika wangebomoa kile ambacho Mungu angefanya urejeshaji kwa ujumbe wa Laodikia. Yeye hujeruhi ili tu apate kuponya, na wala sio kusababisha uangamivu. Bwana hamwekei mtu yeyote mabegani mwake ujumbe utakaolikatisha tamaa kanisa, na kulivunja moyo. Yeye hukemea, Yeye huonya, huthibithisha, Naye Anawarudi wanadamu; ila hufanya hivi kwa ajili ya kuwarejesha, kuwapokea, kuwathibithisha na kuwabariki wanadamu Hatimaye. Jinsi, moyo wangu ulivyoshangilia sana kwa ripoti kutoka makao makuu ya Waadventista (GC), kwamba mioyo mingi ililainishwa, iliguswa na kutiishwa hapo, ndipo wengi walifanya maungamo ya unyenyekevu, nao wakafagilia mbali matakataka nje ya mlango wa moyo ambayo yalikuwa yanamzuia Mwokozi nje. Jinsi nilivyoshangilia kujua kwamba wengi walimkaribisha Yesu kama mgeni wa kudumu. Je, inakuwaje sasa, kwamba vijitabu hivi vinavyoshutumu Kanisa la Waadventista Wasabato kwamba ndiyo Babeli vimetawanywa kila mahali? Wakati ule

ule kanisa hilo lilikuwa linapokea nguvu za Roho wa Mungu, ni aliyekuwa anamwagwa? Je, inawezekanaje kwamba wanadamu wanaweza kudanganywa hivi na Shetani, kiasi cha kufikiria kwamba kilio kikuu kinajumuisha kuwaita watu wa Mungu kutoka katika ushirika wa kanisa ambalo linafurahia majira ya kuburudishwa? Oh jamani, hebu roho hizi zilizodanganyika zingekuja kwenye mfereji [uamsho wa Roho Mtakatifu] na kupokea baraka na kutunukiwa nguvu za ustawi kutoka juu mbinguni.

*Review and Herald , Oktoba 17, 1893.* Reprinted in Testimonies to Ministers, pages 19-23.**[GRCsw 11.3]**

## Kupanga mambo (Ogarnization) na Maendeleo

Ni karibu miaka arobaini tangu kuanzishwa kwa taasisi kati yetu sisi kama watu (Organization introduction). Nilikuwa mmoja wa watu ambao walikuwa na uzoefu kulianzisha kanisa tangu mwanzo. Najua magumu ambayo tulipaswa kukabiliana nayo, maovu ambayo yalikusudiwa kurekebishwa na taasisi, na nimetazama ushawishi wake kuhusiana na kusudi la ukuaji wake. Katika hatua za mapema za hii kazi, Mungu alitupa nuru maalum juu ya kipengele hiki, na kwa hii nuru, pamoja na masomo ambayo uzoefu wetu umetufundisha, na hivi vinapaswa kuzingatiwa kwa makini.**[GRCsw 13.1]**

Tangu mwanzo kazi yetu ilikuwa ya bidii na kali sana (aggressive). Idadi yetu ilikuwa ndogo, na washiriki wengi walitoka miongoni mwa tabaka la watu maskini. Maoni/mafundisho yetu yalikuwa yanajulikana kwa uchache sana ulimwenguni. Hatukuwa na nyumba za ibada, tulikuwa na nyumba chache za uchapishaji, na miundo-mbimu michache sana ya kuendeleza kazi yetu. Kondoo walikuwa wametawanyika katika njia kuu na njia za vichochoro, katika miji mikubwa, katika miji midogo, na ndani ya misitu. Amri ya Mungu na imani ya Yesu zilikuwa jumbe zetu (Ufunuo 14:12)..**[GRCsw 13.2]**

## Umoja katika Imani na Mafundisho

Mume wangu, pamoja na Wazee Joseph Bates, Stephen Pierce, Hiram Edson, na wengine waliokuwa makini, waungwana, bora na wakweli, walikuwa miongoni mwa hao ambao, baada ya muda ule waliotegemea Yesu kurudi kupita, yaani mwaka 1844, walitafuta- na kuchunguza Ukweli kama ile hazina iliyofichwa. **[GRCsw 13.3]**

Tungekusanyika pamoja tukiwa na mizigo ya roho za watu, tukaomba kwamba tuwe wamoja katika imani na mafundisho; kwa maana tulijua kwamba Kristo hajagawanyika. Pointi moja baada ya nyingine ilifanywa kuwa mada ya uchunguzi. Maandiko yalifunguliwa kwa hisia ya kicho. Mara nyingi tulifunga, ili tuweze kuwa na mkao wa kufaa zaidi katika kuelewa Ukweli. Baada ya sala ya dhati na bidii, ikiwa kuna pointi au hoja yoyote ambayo haikueleweka, basi ilijadiliwa, na kila mmoja alitoa maoni yake kwa uhuru; kisha tungesujudu tena katika maombi, na dua za dhati zilipanda kwenda mbinguni ili Mungu atusaidie kuona mambo kwa mtazamo unaokubaliana-jicho kwa jicho [eye to eye], ili tuwe kitu kimoja kama Kristo na Baba walivyo Wamoja. Machozi mengi yalimwagika-Watu wengi walibubujikwa na machozi.**[GRCsw 13.4]**

Tulitumia saa nyingi kwa njia hii. Wakati mwingine usiku wote ulitumika katika uchunguzi mzito wa Maandiko, ili tupate kuelewa Ukweli wa wakati wetu. Wakati fulani Roho wa Mungu angenijia, na sehemu ngumu za Maandiko ziliwekwa wazi kupitia njia iliyowekwa na Mungu, na kisha kukawa na maelewano kamili. Sote tulikuwa na nia moja na roho moja.**[GRCsw 13.5]**

Tulijaribu kwa bidii kutoyapotosha Maandiko, kwamba tusiendane na maoni ya mtu yeyote isipokuwa Bwana tu. Tulijaribu kuzifanya tofauti zetu kuwa chache kwa kadri iwezekanavyo kwa kutozingatia mambo madogo-madogo, pale ambapo kulikuwa na maoni tofauti. Lakini mzigo wa kila nafsi ulipaswa kuleta hali fulani, miongoni mwa ndugu ambayo ingejibu ombi la Kristo ili wanafunzi Wake wawe na umoja kama Yeye na Baba walivyo wamoja. **[GRCsw 14.1]**

Wakati ndugu mmoja au wawili, waliposhupaa kwa ukaidi kinyume cha wasilisho lililotolewa, ndugu wangeweza kuweka kwa ukaidi wenyewe dhidi ya maoni yaliyowasilishwa, na wangethibithisha kwa kutenda kutokana na asili ya hisia za moyo; lakini mwenendo huu ulipoonekana, tuliahirisha uchunguzi wetu na kuahirisha mkutano wetu, kwamba kila mmoja apate fursa ya kumwendea Mungu kwa maombi, na,

bila mazungumzo pamoja na wengine, ajifunze uhakika wa tofauti, akiuliza nuru kutoka mbinguni. Kwa mwonekano wa kirafiki tuliachana, ili tukutane tena baadae kwa haraka iwezekanavyo kwa uchunguzi zaidi. Wakati fulani nguvu za Mungu zilitujia kwa namna iliyo dhahiri, na wakati nuru iliyokuwa wazi ilipofunua pointi za Ukweli, tungelia machozi na kushangilia pamoja. Tulimpenda Yesu; tulipendana sisi kwa sisi.**[GRCsw 14.2]**

[Sometimes one or two of the brethren would stubbornly set themselves against the view presented, and would act out the natural feelings of the heart; but when this disposition appeared, we suspended our investigations and adjourned our meeting, that each one might have an opportunity to go to God in prayer, and, without conversation with others, study the point of difference, asking light from heaven. With expressions of friendliness we parted, to meet again as soon as possible for further investigation. At times the power of God came upon us in a marked manner, and when clear light revealed the points of truth, we would weep and rejoice together. We loved Jesus; we loved one another. ]

## Utangulizi wa Utaratibu wa Kanisa

Idadi yetu iliongezeka polepole. Mbegu iliyopandwa ilikuwa iliyotiwa maji na Mungu, Naye Ndiye aliyeikuza. Mara ya kwanza tulikusanyika kwa ajili ya ibada, na kuwasilisha Ukweli kwa wale wanaokuja kusikia, katika nyumba za watu binafsi, katika majiko makubwa, katika maghala, katika mashamba, na katika majengo ya shule; lakini haikuchukua muda mrefu, nasi tukaweza kujenga nyumba duni za ibada.**[GRCsw 14.3]**

Idadi yetu ilipoongezeka, ilionekana wazi kuwa bila muundo fulani wa shirika kungekuwa na mkanganyiko mkubwa, na kazi isingeweza kupelekwa mbele kwa mafanikio. Ili kutoa msaada kwa huduma, ili ibebe kazi katika nyanja mpya, kwa ajili ya mambo mawili makubwa, yaani kulilinda kanisa, pamoja na huduma kutoka kwa washiriki wasio na stahiki au sifa za kusimamia mali ya kanisa, katika uchapishaji wa ile Kweli kupitia vyombo vya habari, na kwa vitu vingine vingi, kuwa na shirika ilikuwa jambo la lazima.

Hata hivyo kulikuwa na hisia kali dhidi ya kuwa na taasisi miongoni mwa watu wetu.**[GRCsw 14.4]**

Waadventista wa siku za kwanza walipinga kuwa na taasisi (organization), na wengi wa Waadventista Wasabato wamekuwa na mawazo haya haya mioyoni mwao. Tulimtafuta Bwana kwa maombi ya dhati ili tuweze kuelewa mapenzi Yake, na nuru ilitolewa na Roho Wake kwamba lazima kuwe na utaratibu na ukamilifu na nidhamu katika kanisa-kwamba shirika lilikuwa muhimu. Mfumo na utaratibu unadhihirika katika kazi zote za Mungu katika ulimwengu wote. Utaratibu ni sheria ya mbinguni, na inapaswa kuwa kanuni/sheria ya watu wa Mungu duniani.**[GRCsw 15.1]**

## Kuingia kwenye Biashara Mpya

Tulikuwa na shida kubwa katika kuanzisha shirika. Hata hivyo kwamba Bwana alitoa ushuhuda baada ya ushuhuda juu ya hili swala, upinzani ulikuwa na nguvu, na tulipaswa kukutana nao tena na tena. Lakini tulijua kwamba Bwana, Mungu wa Israeli, alikuwa akituongoza, na akiongoza kwa majaliwa/mipango Yake. Tulishiriki katika kazi ya shirika, na kuashiria ustawi ulihudhuria harakati hii ya mapema.**[GRCsw 15.2]**

Maendeleo ya kazi yalipotutaka tushiriki miradi mipya, tulikuwa tayari kuingia. Mungu Alielekeza akili zetu kwenye umuhimu wa kazi ya elimu. Tuliona hitaji la kuwa na shule, ili watoto wetu wapate mafundisho huru kutokana na makosa ya falsafa ya uongo, ili mafunzo yao yapate kuwa katika upatanifu na kanuni za Neno la Mungu. Haja ya taasisi ya afya ilikuwa imesisitiza juu yetu, wote kwa ajili ya kutoa msaada wa mafundisho kwa watu wetu wenyewe na kama njia ya baraka na mwangaza kwa wengine. Mkakati uliendelezwa. Yote hii ilikuwa kazi ya umishenari wa hali ya juu kabisa. **[GRCsw 15.3]**

## Matokeo ya Juhudi za Muungano

Kazi yetu haikudumishwa na zawadi kubwa au pesa za mirathi au wosia; kwa kuwa tulikuwa na matajiri wachache miongoni mwetu. Siri ya ustawi wetu ilikuwa nini? Tumesonga mbele chini ya maagizo ya Kapteni wa wokovu wetu. Mungu amebariki jitihada zetu za umoja. Ukweli umeenea na kushamiri. Taasisi zimeongezeka. Mbegu ya haradali imekua mti mkubwa. Mfumo wa shirika umeonyesha mafanikio makubwa. Mpango wa mfumo wa ukarimu usio na ubinafsi uliingizwa kulingana na mpango wa Biblia (sytematic benevolence). Mwili "umeunganishwa na kile kinachotolewa na kila kiungo." Tunapoendelea, mfumo wetu wa shirika bado umeonekana wenye ufanisi.**[GRCsw 15.4]**

## Kuepuka Hatari za Matatizo

Hebu mtu asitumbuize wazo moyoni, kwamba sisi tunaweza kuachana na matengenezo. Imetugharimu masomo mengi na maombi mengi kwaajili ya kupata hekima, hiyo tunajua Mungu amejibu, ili kusimamisha muundo huu-Jengo hili (kanisa). Kanisa limejengwa juu kwa uongozi Wake Bwana, kwa njia ya dhabihu nyingi na migogoro. Hebu ndugu yetu yeyote ya asidanganywe, au hata kujaribu kubomoa, kwa kuwa ataleta hali ya mambo ambayo mengi hamjawahi kuyawazia au kuyaota. Katika

Jina la Bwana nawatangazia  kanisa litasimama litaimarishwa, litasimikwa na matatizo yake yatatatuliwa na kutulia. Kwa amri ya Mungu, “Songeni mbele,” sisi tulisonga mbele wakati ulipokuwa mgumu, na wenye matatizo mengi yaliyohitaji kutatuliwa, ambayo yaliyonekana hayawezaniki. Tunajua imegharimu kiasi gani kutekeleza mipango ya Mungu katika siku za nyuma, jambo ambalo limetufanya kama watu tulivyo. Kisha kila mtu na awe mwangalifu sana ili  asiyumbishe akili za wengine katika jambo hilo kwa yale mambo ambayo Mungu ameyapanga kwa ajili ya ustawi na mafanikio yetu katika kuendeleza kazi Yake. **[GRCsw 16.1]**

Malaika hufanya kazi kwa mapatano. Utaratibu kamili una sifa za harakati zao zote. Kadiri tunavyoiga kwa ukaribu maelewano na utaratibu wa jeshi la malaika, ndivyo jitihada za hawa  mawakala wa mbinguni zitakavyofanikiwa zaidi  kwa niaba yetu. Ikiwa hatuoni umuhimu wa kuelewana katika utendaji wetu, na tu watu wa vurugu au machafuko, wavivu, watovu wa nidhamu, na wasio na mpangilio katika hatua zetu, malaika, ambao wamepangwa vizuri na wanasonga kwa mpangilio mkamilifu na maelewano, hawawezi kufanya kazi kwa ajili yetu kwa mafanikio. Wanageuka kwa huzuni, kwa maana hawana mamlaka ya kubariki machafuko, kukosa umakini kwa kumangamanga, mkanganyiko, na kutokuwa na mpangilio. Wote wanaotamani ushirikiano wa wakazi wa mbinguni lazima wajumbe hawa wafanye kazi pamoja nao. Wale ambao wamepakwa mafuta na Roho Mtakatifu kutoka juu, katika juhudi zao zote huhamasiha utaratibu, nidhamu, na muungano wa matendo/utendaji, na kisha malaika wa Mungu wanaweza kushirikiana pamoja nao. Lakini kamwe, kamwe hawa wajumbe wa mbinguni hawataidhinisha ukosefu wa nidhamu, kukosa mwendelezo au uthabiti, kukosa mpangilio au mfumo, mgawanyiko, na machafuko. Maovu haya yote ni matokeo ya juhudi za Shetani kudhoofisha nguvu zetu. kuharibu ujasiri wetu, na kuzuia hatua ya mafanikio.**[GRCsw 16.2]**

Shetani anajua vizuri kwamba mafanikio yanaweza tu kuwepo pale ambapo kuna utaratibu na utendaji wenye mapatano. Adui anajua vizuri kwamba kila kitu kilichounganishwa na mbingu kina utaratibu kamili, kujisalimisha na nidhamu kamili hutia alama kwa Mungu, harakati za jeshi la malaika. Ni juhudi zake adui, anazosomea daima, ili kuwaongoza Wakristo wanaokiri kwa mdomo tu, kuwa mbali sana na mpango wa mbinguni kadiri awezavyo; kwa hiyo anawadanganya hata wale wanaojiita kuwa ni watu wa Mungu, kwa kuwafanya waaamini kwamba utaratibu na nidhamu ni adui wa

mambo ya kiroho, kwamba eti usalama wao pekee kwao ni kuacha kila mmoja ajifanyie apendayo, yaani afuate njia yake mwenyewe, na kubaki kuwa tofauti na miili ya Wakristo walio na umoja na wanaofanya kazi ili kuweka nidhamu na mapatano katika utendaji. Juhudi zote zinazofanywa ili kuleta utaratibu, huzingatiwa kama hatari, na kizuizi cha uhuru wa haki za mtu, na hivyo huogopwa kama upapa. Nafsi hizi zilizojitoa kwa namna hii, huona kuwa ni fadhila kujivunia uhuru wao wa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea. Hawachukui usemi wa mtu yeyote, hawataki mambo ya "hivi ndivyo asema fulani nk". Hawakubaliani na mtu yeyote. Nilionyeshwa kwamba ni kazi maalum ya Shetani kuwaongoza wanadamu kuona kwamba ni mpango wa Mungu, kuanza jambo jipya kwa uhuru wa mtu binafsi na kulifanya bila msaada wa mtu, watu hawa huchagua njia yao wenyewe bila ya ndugu zao.**[GRCsw 17.1]**

Mungu anawaongoza watu kutoka duniani kutumia jukwaa lililoinuliwa la Ukweli wa milele, amri za Mungu na imani ya Yesu. Yeye Atawaadhibu na kuwapa stahiki watu Wake. Hakutakuwapo na tofauti ya mmoja kuamini jambo moja na mwingine kuwa na imani na maoni kinyume kabisa, kila mmoja akisonga kwa kujitegemea, mbali na mwili wa Kristo. Kupitia utofauti wa karama na uongozi ambao Yeye ameweka ndani ya kanisa, wote watakuja kwenye umoja wa imani. Ikiwa mtu mmoja anachukua maoni yake juu ya ile Kweli ya Biblia bila kujali maoni ya ndugu yake, na kuhalalisha mwenendo wake, akidai kwamba ana haki ya kuwa na maoni yake mwenyewe ya kipekee, na kisha kushinikiza juu ya wengine, Je, ni kwa jinsi gani anaweza kuyatimiza maombi ya Kristo? (Yohana 17) Na mtu mwingine na bado mwingine tena akatokea, na kila mmoja akidai haki yake ya kuamini na kuzungumza kile anachopendezwa nacho pasipo kurejelea imani ya mwili, je, hali ile ya maelewano yaliyokuwepo kati ya Kristo na Baba Yake, na ambayo Kristo aliomba iwepo miongoni mwa ndugu Zake itakuwa wapi? Au itakuwepo kweli? **[GRCsw 17.2]**

## Wajibu wa Mtu Binafsi na Umoja wa Kikristo

Ingawa tuna kazi-binafsi na jukumu la mtu binafsi mbele za Mungu, hatupaswi kufuata maamuzi yetu huru, bila kujali maoni na hisia za ndugu zetu; kwani hii ingesababisha machafuko katika kanisa. Ni wajibu wa wachungaji kuheshimu maamuzi/hukumu ya ndugu zao; pia mahusiano kati yaom wao kwa wao, pamoja na Mafundisho ya Imani wanayofundisha, yanapaswa kuletwa kwa jaribio au kutahiniwa

kwa sheria na ushuhuda; basi, ikiwa mioyo iko tayari kufundishika, hakutakuwa na migawanyiko kati yetu. Baadhi wana mwelekeo wa kuwa wavivu, na wanaondoka polepole kutoka kwenye alama kuu za imani; lakini Mungu anafanya kazi juu ya watumishi Wake ili wawe kitu kimoja katika Mafundisho ya imani na katika roho [Doctrine and Spirit].[GRCsw 17.3]

Ni muhimu kwamba umoja wetu leo uwe wa tabia ambayo itastahimili [18] mtihani wa majaribio. . . . Tuna masomo mengi ya kujifunza, na mengi, mengi ya kuyaondoa vichwani ambayo tumejifunza [unlearn]. Mungu na mbingu pekee ndivyo hawana makosa, wala hafanyi makosa. Wale wanaofikiri kwamba hawatalazimika kamwe kuacha maoni yao pendwa, kamwe hawatakuwa na tukio la kubadilisha maoni yao, watakatishwa tamaa. Ilimradi sisi tunayashikilia mawazo na maoni yetu wenyewe kwa uthabiti na kwa kudhamiria, sisi hatuwezi kuwa na umoja ambao Kristo aliuombea. [GRCsw 18.1]

- Ndugu anapopokea nuru mpya juu ya Maandiko, anapaswa aeleze msimamo wake kwa uwazi, na kila mtumishi/mchungaji achunguze Maandiko kwa roho ya unyoofu ili kuona ikiwa mambo ambayo yametolewa yanaweza kuthibitishwa na Neno lililovuviwa. "**24** Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; **25** akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awajalie ili watubu na kuijua Kweli ." 2 Timotheo 2:24, 25 .[GRCsw 18.2]

## Mungu Ametenda!

Katika kukagua historia yetu ya zamani, baada ya kusafiri juu ya kila hatua inayosonga mbele kwa msimamo wetu wa sasa, ninaweza kusema, Mungu asifiwe! Navyoangalia kile ambacho Mungu amekifanya, nimejawa na mshangao, na ujasiri katika Kristo kama kiongozi. Hatuna chochote ya kuogopa kuhusu siku zijazo isipokuwa kama tutasahau njia ambayo Bwana ametuongoza na Mafundisho Yake katika Historia yetu iliyopita .[GRCsw 18.3]

Sisi sasa tu watu wenye nguvu, tunamtumaini Bwana; kwa maana tunashughulikia zile Kweli kuu za Neno la Mungu. Sisi tuna sababu zote za kuwa na roho ya shukrani. Tukienenda katika nuru kama ilivyo, Nuru hii hutuangazia kutoka kwa Maneno yaliyo hai na yasiyokosea ya Mungu, tutakuwa na majukumu mengi,

yanayolingana na nuru kuu tuliyopewa na Mungu. Tuna majukumu mengi ya kufanya kwa sababu tumeaminiwa kuwa wahifadhi wa hazina za Kweli takatifu zitakazotolewa kwa ulimwengu katika uzuri Wake wote na utukufu. Tuna deni kwa Mungu kutumia kila faida aliyoikabidhi kwetu, kuzipamba zile Kweli kwa utakatifu wa tabia, na kuzifanya ziwe nzuri na tuna jumbe za onyo, za faraja, za tumaini na upendo, kwa wale walio katika giza la upotofu, makosa na dhambi.**[GRCsw 18.4]**

Asante Mungu kwa kile ambacho tayari kimefanyika katika kutupatia, vifaa na miundombinu kwa vijana kwa mafunzo ya kidini na kiakili. Wengi wamewahi kuelimishwa kushika nafasi katika matawi mbalimbali ya kazi, si tu katika Bara la Amerika, lakini pia katika nyanja za kigeni. Vyombo vya habari, na hasa mashine za uchapaji zimetoa fasihi ambayo imeeneza maarifa ya Ukweli mbali na karibu. Hebu **zawadi** zote ambazo ni kama vijito vidogo, vivyosheheni na kujaa mkondo wa wema na ukarimu, zitambuliwe kama sababu ya kumshukuru Mungu. [19] Tuna jeshi la vijana leo ambao linaweza kufanya mengi ikiwa linaweza kuelekezwa, kuhamasishwa na kutiwa moyo ipasavyo. Tunataka watoto wetu waamini Ukweli. Tunataka wabarikiwe na Mungu. Tunataka watende sehemu fulani katika mikakati iliyopangwa vizuri ya kuwasaidia vijana wengine. Hebu wote wawe wamefunzwa na kuzoezwa ili waweze kuwakilisha Ukweli ipasavyo, wakitoa sababu ya tumaini lililo ndani yao, na kumheshimu Mungu katika tawi lolote la kufanya kazi pale ambapo wana sifa za kufanya kazi. . . .**[GRCsw 19.1]**

Kama wanafunzi wa Kristo ni wajibu wetu kueneza nuru ambayo tunajua dunia haina. Watu wa Mungu "wawe matajiri katika kazi njema, tayari kusambaza, tayari kuwasiliana; kujiwekea akiba kwa ajili yao wenyewe, msingi mzuri kwa wakati ujao, ili waupate uzima wa milele." *1 Timotheo 6:18, 19.- Testimonies for the Ministers , ukurasa wa 24-32*…….**[GRCsw 19.2]**

# Sehemu ya Pili - Kanisa na Masalio Sio Babeli

*Sehemu hii inaundwa na mfululizo wa makala ambayo yalichapishwa katika Mapitio na Herald kuanzia Agosti 22 hadi Septemba 19, 1893.

## Mshitaki na Kazi Yake

Nimehuzunishwa sana katika kusoma chapisho ambalo limetolewa na Ndugu S. na wale walioshirikiana naye katika kazi aliyoifanya imekuwa ikifanya. Bila ridhaa yangu, wamechagua nukuu kutoka kwenye Shuhuda, na wameziingiza katika kijitabu walicho nacho na kukichapa, ili kufanya ionekane kwamba maandishi yangu yanaidhinisha na kuukubali msimamo wanaoutetea. Kwa kufanya hivi wamefanya jambo lisilo la haki au uadilifu. Kupitia kujichukulia uhuru usio na msingi wamewasilisha kwa watu nadharia ambayo ni ya tabia ya kudanganya na kuharibu. Kuna wengine wengi wamefanya hivi jambo lile lile siku za nyuma, na wameifanya ionekane kwamba Shuhuda zilishikilia nafasi na hoja ambazo hazikubaliki na za uongo. **[GRCsw 20.1]**

Nimepata nuru kuwa msimamo uliochukuliwa na Brothe S. na wale wanaomhurumia si wa kweli, bali ni mmoja wa "tazama, Yuko hapa" na "tazama! Yuko kule" [Luka 17:21] ambayo itaonyesha siku tunazoishi. Kama sampuli ya njia ambayo Ndugu S. ametayarisha kijitabu hiki, nitafuatilia tukio hili kwa kusema yafuatayo: Niliandika barua ya kibinafsi kwa mmoja wa wachungaji wetu, na kwa wema, wakififikiri kwamba inaweza kuwa msaada kwa Ndugu S., ndugu huyu alimpelekea nakala yake; lakini badala ya kuichukulia kama jambo la msaada wake binafsi, yeye alichapisha sehemu zake katika kijitabu kama Ushuhuda ambao haujachapishwa [Unplublished Testimony], ili kudumisha msimamo aliokuwa amechukua. Je, hii ni heshima? Hakukuwa na kitu katika Ushuhuda cha kutetea msimamo alio nao Ndugu S.; lakini aliitumia vibaya, kama wengi wanavyofanya na Maandiko, kwa kuumiza nafsi yake na nafsi za wengine. Mungu atawahukumu wale wanaojichukulia uhuru usiofaa au usio na msingi na kuutumia kwa njia zisizo na adabu/heshima ili kutoa tabia na ushawishi kwa kile watu wanachoona ndiyo Ukweli. Kwa kutumia barua ya kibinafsi iliyotumwa kwa mwingine, Ndugu S. ametumia vibaya juhudi za fadhili za mtu aliyetamani kumsaidia yeye. **[GRCsw 20.2]**

Kundi lililochapisha kijitabu hicho Kilio kikuu, na anguko la makanisa yote, vinatoa uthibitisho huo Roho Mtakatifu wa Mungu hafanyi kazi pamoja nao. "Kwa matunda yao ninyi mtawajua." **[GRCsw 21.1]**

Wale wanaopokea vijitabu vya kutetea misimamo hii ya uwongo, watapokea hisia kwamba mimi ninashikilia misimamo na nafasi hizi, na naungana na wafanyakazi hawa katika kutangaza kile wanachokiita "Nuru mpya." Ninajua kwamba ujumbe wao umechanganyikana na Ukweli, lakini Ukweli unatumiwa vibaya na kupokonywa kwa kuunganishwa kwa makosa. Ningemwambia ndugu aliyetuma kwa wanaume hao nakala ya barua ambayo nilikuwa nimemwandikia, kwamba sikuwa na wazo hata moja la kukulaumu; wala mtu asitupe lawama hata ndogo juu ya jambo hili. Nikikuhukumu vibaya na kukushutumu, wakati nia yako na makusudi ilikuwa nzuri, ningejiletea ghadhabu ya Mungu kwangu mwenyewe. Kama Yule ndugu uliyetaka kumsaidia amejichukulia uhuru na kuusaliti ujasiri wako, usijilaumu na kuhuzunika juu ya matokeo ya kutokuwa mwaminifu kwake.**[GRCsw 21.2]**

## Maelekezo kwa Wanafunzi

Kuna mambo yaliyoandikwa katika Shuhuda ambayo sio kwa ajili ya ulimwengu kwa ujumla, bali kwa watoto wa Mungu wanaoamini, na hivyo haitafaa kutoa mafundisho, maonyo, karipio, au shauri lenye tabia hii hadharani kwa ulimwengu. Mkombozi wa ulimwengu, Yule Aliyetumwa na Mungu, Mwalimu mkuu zaidi ambaye watoto wa wanadamu wamewahi kumjua, aliwasilisha baadhi ya mada zingine za mafundisho, sio kwa ulimwengu wote, bali kwa wanafunzi Wake peke yao. Wakati Alikuwa na mawasiliano yaliyowekwa kwa ajili ya makutano waliosongamana karibu na nyayo Zake, Yeye pia alikuwa na nuru maalum na maagizo ya kuwapa wafuasi Wake, yale ambayo hakuyatoa kwa kusanyiko kubwa, endapo lile somo lisingeeleweka wala kuthaminiwa nao. Yeye Aliwatuma wanafunzi Wake kuhubiri, na waliporudi kutoka kwa kazi yao ya kwanza ya umishenari, walikuwa na aina mbalimbali za uzoefu wa kusimulia kuhusu mafanikio yao katika kuhubiri injili juu ya ufalme wa Mungu,"Akawaambia, Njooni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula." Katika mahali pa kujitenga Yesu aliwapa wafuasi Wake maagizo kama hayo, ushauri, maonyo, na masahihisho kama alivyoona yalihitajika katika namna yao ya kazi; lakini maagizo aliyowapa hayakuwa ya kurushwa kwenye matangazo kwa kundi la watu wapotovu, kwa maana Maneno Yake yalikusudiwa kwa ajili ya wanafunzi tu.**[GRCsw 21.2]**

Katika matukio kadhaa wakati Bwana alikuwa ametenda kazi za uponyaji, Aliwaamuru wale aliowabariki wasiseme tukio hilo kwa yeyote. Walipaswa kutii amri Zake na kutambua kwamba Kristo hakuhitaji ukimya tu kwa upande wao kwenye hili tukio, lakini alikuwa na sababu ya kutoa amri Yake, wala hawakupaswa kulipuuza takwa lake hili hata kidogo. Ilipaswa kutosha kwao kujua kwamba Yeye alitamani walishike shauri hili wao wenyewe, na alikuwa na sababu nzuri ya kutoa ombi Lake la dharura. Bwana alijua kwamba katika kuponya wagonjwa, katika kufanya miujiza ya kuwafanya vipofu wapate kuona tena na kutakaswa kwake mtu mwenye ukoma, alikuwa akihatarisha maisha Yake Mwenyewe; kwani kama makuhani na watawala hawatapokea ushahidi aliowapa juu ya utume Wake wa Kiungu, wangeweza kupotosha, kuongopa, na kufanya mashtaka dhidi Yake. Ni kweli kwamba Masihi alifanya miujiza mingi

hadharani, lakini wakati fulani aliomba wale aliowabariki wasimwambie mtu yeyote yale aliyowafanyia. Wakati ubaguzi ulikuwa unachochewa, husuda na kijicho , na njia Yake imezingirwa, akaondoka mijini, akaenda kutafuta wale ambao wangesikiliza na kuthamini Ukweli aliokuja kuwapa.**[GRCsw 22.1]**

Bwana Yesu aliona ni muhimu kuweka mambo mengi wazi kwa wanafunzi Wake ambayo hakuwafungulia makutano. Yeye aliendelea kuwafunulia kwa uwazi sababu ya chuki iliyodhihirishwa Kwake na waandishi na Mafarisayo na makuhani, akawapasha habari za mateso Yake, usaliti, na kifo; lakini hakuyafanya mambo haya kwa ulimwengu kuwa wazi sana. Alikuwa na maonyo ya kuwapa wafuasi Wake, na alifunua kwao matukio ya huzuni ambayo yangetokea, na nini walipaswa kutarajia. Aliwapa wafuasi Wake mafundisho ya thamani hata wao hawakuyaelewa mpaka baada ya kufa Kwake, ufufuo na kupaa. Wakati Roho Mtakatifu alipomiminwa juu yao, mambo yote yaliletwa kwenye kumbukumbu zao, yote aliyoyasema kwao.**[GRCsw 22.2]**

## Kusaliti Ujasiri

Ilikuwa ni usaliti wa amana takatifu, kuchukua kile ambacho Yesu alidizaini ili kiwekwe kama siri, na kukitangaza kwa wengine, na kuleta kusudi la kazi ya Ukweli, au Kazi ya Mungu kulaumiwa na kuumizwa. Bwana amewapa watu Wake ujumbe unaofaa wa onyo, karipio, shauri na mafundisho, lakini haifai kuondoa jumbe hizi kwenye muunganiko wao na kuziweka mahali ambapo zitaonekana kutoa nguvu za kosa kwa jumbe. Katika kijitabu kilichochapishwa na Ndugu S. na washirika wake, analishutumu kanisa la Mungu kuwa Babeli, na anasisitiza kwa watu kujitenga na kanisa. Hii ni kazi isiyo na heshima, inaabisha, inakosa maadili na wala haitendi haki. Katika kuandaa kazi hii, wametumia jina langu na maandishi, kwa ajili ya kuunga mkono ajenda nisiyokubaliana nayo na kuikanusha kama makosa. Watu ambao kijitabu hiki kitawafikia, watatoa hukumu kwa msimamo huu wa udanganyifu juu yangu, wakati ni kinyume kabisa na mafundisho ya maandiko yangu na nuru ambayo Mungu amenipa. Sina kigugumizi kusema kwamba hao wanaosukuma mbele kazi hii wanadanganywa sana.**[GRCsw 22.3]**

## Ujumbe wa Uongo

Kwa miaka mingi nimetoa ushuhuda wangu kwamba wakati wowote atakapotokea mtu na kudai kuwa na nuru kubwa, na bado akatetea kuyakata-kata yale ambayo Bwana amekuwa akijenga kupitia mawakala Wake wa kianadamu, basi wamedanganyika sana, na hawafanyi kazi sambamba na ile ambayo Kristo anafanya. Wale wanaodai kuwa makanisa y aWaadventista wa siku ya saba ndiyo yanaunda Babeli, au sehemu yoyote ya Babeli, bora wakae nyumbani. Hebu wasimame na kufikiria ujumbe gani unaopaswa kutangazwa kwa wakati huu. Wao badala ya kufanya kazi pamoja na vyombo vya Kiungu ili kuwatayarisha watu kusimama katika siku ya Bwana, wamechukua msimamo wao pamoja na yeye ambaye ni mshitaki wa ndugu, wanaowashitaki wengine mbele za Mungu mchana na usiku. Mawakala ya Kishetani yamehamishwa kutoka chini, na yamehamasisha watu waungane katika muungano wa uovu, ili wapate kutatanisha, kusumbua, na kuwapa watu wa Mungu dhiki kubwa. Dunia nzima inachochewa na uadui dhidi ya Waadventista Wasabato, kwa sababu hawatatoa heshima kwa upapa, na hawatamwabudu papa kwa kuheshimu Jumapili, Taasisi ya nguvu hii ya mpinga Kristo. Ni kusudi la Shetani kuwafanya wanadamu wafutiliwe mbali katika dunia, ili ukuu wake duniani usipingwe.**[GRCsw 23.1]**

## Mashtaka ya Shetani

Tukio la mashtaka ya Shetani liliwasilishwa mbele ya nabii. Anasema nabii Zekaria, “Akanionyesha Yoshua kuhani mkuu amesimama mbele ya malaika wa Bwana, na Shetani amesimama upande wake wa mkono wa kuume kumpinga.” Yesu Ndiye Kuhani wetu Mkuu mbinguni. Je, anafanya nini sasa? Anafanya maombezi na upatanisho kwa ajili ya watu wanaomwamini. Kwa njia ya haki Yake anayowahesabia wattu, wanakubaliwa na Mungu kama wale wanaodhihirika kwa ulimwengu kwamba wanakiri utii kwa Mungu, wakishika amri Zake zote.**[GRCsw 23.2]**

Shetani amejaa chuki ya kutisha dhidi yao, na anadhihirisha kwao roho ile ile aliyomdhihirishia Yesu Kristo wakati Yeye alipokuwa duniani. Yesu alipokuwa mbele ya Pilato, mtawala huyu wa Kirumi alitaka kumwachilia huru, na alitaka watu wachague kumwachilia Yesu kutoka katika hukumu ambayo alikuwa karibu kuivuka. Aliwasilisha mbele ya umati unaopiga kelele kuchagua kati ya Mwana wa Mungu na yule mhalifu

Baraba, akauliza, “Je, Yupi Mnataka nimwachilie na kwenu? Baraba au Yesu anayejulikana kama Kristo? "Walisema, Baraba. Pilato akawaambia, Nifanye nini basi na Yesu Aitwaye Kristo? Wote wakamwambia, Asulubiwe.**[GRCsw 24.1]**

Ulimwengu ulichochewa na uadui wa Shetani, na watu walipoulizwa kuchagua kati ya Mwana wa Mungu na mhalifu Baraba, wao walimchagua jambazi badala ya Yesu. Makundi ya wajinga yaliongozwa na mawazo ya udanganyifu ya wale walio katika vyeo vya juu, na kumkataa Mwana wa Mungu, na kumchagua jambazi na muuaji badala ya Masihi. Hebu sote tukumbuke kwamba bado tuko katika ulimwengu ambamo Yesu, Mwana wa Mungu, alikataliwa na kusulubiwa, mahali ambapo hatia ya kumdharau Kristo na kuwapendelea wanyang'anyi badala ya Mwana-Kondoo wa Mungu asiye na doa bado inaendelea. Pasipo sisi binafsi kutubu kwa Mungu kwa sababu ya makosa ya sheria Yake, na kuwa na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ulimwengu umemkataa, tutalala chini ya hukumu kamili kwamba kitendo cha kumchagua Baraba badala ya Kristo ambaye Ndiye anastahili na Ndiye Mwenye sifa. Dunia nzima inasimama chini ya mashtaka leo kwa kumkataaa Masihi kwa makusudi na mauaji ya Mwana wa Mungu. Neno linashuhudia kwamba Myahudi na mtu wa Mataifa, wafalme, magavana, wahudumu, makuhani, na watu wa tabaka zote na madhehebu yanayofunua roho ileile ya husuda, chuki, ubaguzi, na kutokuamini kulikodhihirishwa na wale waliomuua Mwana wa Mungu hutenda sehemu ile ile, kama wangekuwa na fursa, kama walivyofanya Wayahudi na watu wa wakati wa Kristo. Hakika wangeshiriki roho sawa ambayo iliyodai kifo cha Mwana wa Mungu.**[GRCsw 24.1]**

Katika tukio linalowakilisha kazi ya Kristo kwa ajili yetu, na mashitaka yaliyoamuliwa ya Shetani dhidi yetu, Yoshua anasimama kama kuhani mkuu, na kufanya maombezi kwa niaba ya watu wazishikao amri za Mungu. Wakati huo huo Shetani anawawakilisha watu wa Mungu kama ‘wenye dhambi wakuu’, na kuwasilisha mbele za Mungu orodha ya dhambi alizowajaribu nazo watu katika maisha yao yote, na kusisitiza kwamba ni kwa sababu ya makosa yao, na hivyo wametiwa mikononi mwake ili awaangamize. Adui hapa anasisitiza kwamba hawapaswi kulindwa na malaika wanaohudumia watu dhidi ya muungano wa uovu. Amejaa hasira kwa sababu hawezi kufunga watu wa Mungu kuwa matita pamoja na ulimwengu, ili kumpa yeye utii kamili. Wafalme na watawala wameweka juu yao wenyewe chapa ya mpinga Kristo, na kuwakilishwa kama joka ambaye huenda na kufanya vita dhidi ya watakatifu - pamoja

na wale wanaozishika amri za Mungu na walio na imani ya Yesu. Katika uadui wao dhidi ya watu wa Mungu, wanajionyesha kuwa na hatia pia kwa chaguo lao la Baraba badala ya Kristo.**[GRCsw 24.2]**

## Ulimwengu Waitwa Kuwajibika

Mungu ana mgogoro na dunia. Wakati wa hukumu utakapofika, na vitabu vitakapofunguliwa, Yeye ana hesabu/akaunti ya kutisha sana ya kusuluhisha, ambayo sasa ingeifanya dunia kuwa na hofu na kutetemeka kama wanadamu hawakuwa wamepofushwa na kulogwa na udanganyifu na uongo wa kishetani. Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kifo cha Mwanawe wa pekee, ambaye kwa nia na makusudi yote ulimwengu umemsulubisha upya, na kumtuipa aibu ya wazi katika mateso ya watu Wake. Dunia imemkataa Kristo katika nafsi ya watakatifu Wake, imekataa jumbe Zake katika kukataa jumbe za manabii, mitume, na wajumbe. Wanadamu wamewakataa wale ambao wamekuwa watenda kazi pamoja na Kristo, na kwa hili watalazimika kutoa hesabu.**[GRCsw 25.1]**

## Mshtaki Alikemea

Shetani anasimama kama kiongozi wa washitaki wote wa ndugu; lakini anapowasilisha dhambi za watu wa Mungu, je! Bwana atamjibu nini? Anasema, “Bwana amkemee [si Yoshua, ambaye ni mwakilishi wa watu wa Mungu waliojaribiwa na waliochaguliwa, lakini] wewe, O Shetani; hata Bwana aliyeichagua Yerusalemu na akukemee; hii ni chapa iliyong'olewa kutoka kwa moto? Yoshua wakati huu alikuwa amevaa mavazi machafu, na akasimama mbele ya Malaika.” Shetani alikuwa amewawakilisha watu waaminifu waliochaguliwa na Mungu wakiwa wamejaa unajisi na dhambi. Adui angeweza kuonyesha dhambi bainishi walizokuwa na hatia nazo. Je, hakuwa ameratibu muungano wote wa uovu kazini ili kuwaongoza wanadamu, kupitia ufundi wake wa kushawishi, ili waingie katika dhambi hizi hizi? Lakini watu walitubu, na kukubali haki ya Kristo. **[GRCsw 25.2]**

Kwa hiyo walikuwa wamesimama mbele za Mungu wakiwa wamevikwa mavazi ya haki ya Kristo, na “Akajibu, akasema kwa wale waliosimama mbele yake, akisema, Ondoeni nguo chafu kutoka kwake. Akamwambia, Tazama, nimekuondolea maovu yako

yatoke kwako, Nami nitakuvika mavazi tofauti." Kila dhambi ambayo walikuwa wameifanya ilisamehewa, na walisimama mbele za Mungu kama wateule na na wakweli/waadilifu, wasio na hatia, wakamilifu, kama vile hawakuwahi kutenda dhambi kamwe.**[GRCsw 26.1]**

## Neno la Kutia Moyo

"Nami nikasema, Na waweke kilemba kizuri juu ya kichwa chake. Hivyo wao [Malaika wa Mungu] wakamwekea kilemba kizuri kichwani, wakamvika mavazi. Na Malaika wa Bwana akasimama karibu Naye [Yesu Mkombozi wao]. Malaika wa Bwana akamkemea Yoshua, akisema, Bwana wa majeshi asema hivi; kama Ukienda katika njia Zangu, na kama ukishika maagizo yangu, ndipo utakapoihukumu nyumba Yangu, nawe utailinda nyua Yangu, nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu." Natamani kwamba wote wanaodai kuamini Ukweli wa sasa wangefikiria kwa uzito mambo ya ajabu yaliyowasilishwa katika sura hii. Ingawa watu wa Mungu wanaweza kukosa nguvu na kuzingirwa na udhaifu kadri inavyoweza kuwa, wale wanaogeuka kutoka katika kukosa uaminifu kwa Mungu katika uovu huu na kizazi cha ukaidi, na kisha wakarudi kwenye utii wao, wakisimamana kuthibitisha sheria takatifu ya

Mungu, na kurakabati uvunjaji wa sheria uliofanywa na mtu wa dhambi chini ya uongozi wa Shetani, watahesabiwa kuwa wana wa Mungu, na kwa njia ya haki kupitia

Kristo watasimama wakamilifu mbele za Mungu. Ukweli hautalala mavumbini siku zote, ili kukanyagwa ya wanadamu. Ukweli utatukuzwa na kuheshimiwa; utainuka na kung'aa katika mng'ao wake wote wa asili, na utasimama imara milele na milele. *Review and Herald , Agosti 22, 29, 1893*. Imechapishwa tena *kutoka Testimonies for the Ministers*, ukurasa wa 32-41 angalia MaarifaMtandaoni. Com, au RohoyaUnabii.Org.**[GRCsw 26.2]**

## Kanisa Si Babeli

Mungu ana watu ambao mbingu zote zinapendezwa nao, nao ni vitu pekee duniani vinavyopendwa na moyo wa Mungu-anavyovithamini. Hebu kila mtu anayesoma maneno haya ayazingatie kwa kina, kwani katika Jina la Yesu ningeyasisitiza maneno haya nyumbani mwa kila roho. Pale mtu yeyote atatokea, ama kati yetu au nje yetu, ambaye analemewa na ujumbe unaotangaza kwamba watu wa Mungu

wamehesabiwa na Babeli, na kudai kwamba 'kilio kikuu' ni mwito wa kutoka kwake [kutoka katika kanisa], unaweza kujua kwamba yeye habebi ujumbe wa Kweli. Mtu huyo msimpokee, wala msimtakie mafanikio au safari njema; kwa maana Mungu hajasema naye, wala hakumpa huo ujumbe, amekimbia kabla hajatumwa au kupewa ujumbe. Ujumbe uliomo kwenye kijitabu hicho uitwao 'Kilio kikuu', ni udanganyifu. Ujumbe kama huo utakuja, na watu watadai kwamba wametumwa na Mungu, lakini dai litakuwa uongo; kwa maana hawakujazwa nuru, bali giza. Kutakuwa na ujumbe wa mashtaka dhidi ya watu wa Mungu, sawa na kazi inayofanywa na Shetani katika kuwashtaki watu wa Mungu, na jumbe hizi zitasikika wakati ule ule Mungu atakapowaambia watu Wake, "Ondoka, na uangaze; kwa maana nuru yako imekuja, na utukufu wa Bwana umezuka juu yako. Maana, tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litaifunika dunia watu wa giza; bali Bwana atakuzukia Wewe na utukufu Wake utaonekana juu yako." **[GRCsw 27.1]**

### Kazi ya Udanganyifu

Itapatikana kwamba wale wanaobeba ujumbe wa uongo hawatakuwa na hali ya juu ya heshima na uadilifu. Watadanganya watu, na kuchanganya makosa yao na *Shuhuda* za Dada White, na kulitumia jina lake kutoa ushawishi kwa kazi zao. Wanafanya chaguzi kama hizo kutoka kwa *Shuhuda* wanapofikiri wanaweza kupindisha mada ili kusaidia misimamo yao, na na kuyaweka mada katika udanganyifu, ili upotofu wao uweze kuwa na uzito na kukubaliwa na watu. Wanatafsiri vibaya na kutumia vibaya yale ambayo Mungu amelipatia kanisa kuonya, kushauri, kukaripia, kufariji, na kuwatia moyo wale watakaounda namba ya watu wa Mungu wa masalio. Wale wanaopokea *Shuhuda* kama ujumbe wa Mungu watasaidiwa na kubarikiwa kwa hilo; lakini wale ambao huzichukua sehemu-sehemu au vipande-vipande vya hizi shuhuda, ili tu kuunga mkono nadharia fulani au wazo lao wenyewe, watajithibitisha wenyewe katika njia ya upotofu, hawatabarikiwa na kufaidika na yale wanayofundisha. Kudai kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato wa Siku ya Saba ni Babeli, ni kufanya madai sawa na yale aliyofanya Shetani, ambaye ni mshitaki wa ndugu, ambaye daima huwashtaki waamini mbele za Mungu, usiku na mchana. Kwa matumizi haya mabaya ya *Shuhuda*, roho zitaletwa katika mshangao, kwa sababu watu hawawezi kuelewa uhusiano wa *Shuhuda* kwa msimamo unaochukuliwa na wale walio katika makosa; kwa maana Mungu

alikusudia kwamba Shuhuda ziwe na mpangilio kila wakati kwenye mfumo wa Ukweli.[GRCsw 27.2]

Wale wanaotetea makosa husema, “Bwana asema hivi,” “wakati Bwana hakusema.” Wanashuhudia uwongo, na wala sio Ukweli. Ikiwa wale ambao wamekuwa wakitangaza ujumbe kwamba kanisa ni Babeli wangekuwa wametumia pesa za taasisi ya uchapishaji ili kusambaza hili kosa na hivyo kujenga badala ya kubomoa, wangekuwa wameonesha wazi kwamba walikuwa watu ambao Mungu anawaongoza.[GRCsw 28.1]

Kuna kazi kubwa ya kufanywa duniani, kazi kubwa za kufanywa katika nchi za kigeni. Shule lazima zianzishwe kwa utaratibu huo, ili vijana, watoto, na wale wa umri wa kukomaa zaidi wanaweza kuelimishwa kwa wepesi kwa kadri iwezekanavyo ili kuingia katika eneo la umishenari. Sio tu kwamba kuna haja ya kupata wahudumu wa mashamba ya kigeni, lakini pia watendakazi wenye hekima, na maamuzi ya busara za kila aina. Kilio cha Makedonia kinasikika kutoka sehemu zote za ulimwengu, "Njoo huku, ... na utusaidie." Pamoja na uwajibikaji wote, hebu twende kuhubiri injili kwa kila kiumbe, ipo haja kubwa ya kuwa na watu na fedha, na Shetani anafanya kazi kwa kila njia inayowezekana kuzifungia fedha, na kuwazuia watu kushiriki katika kazi hiyo hiyo ambayo wanapaswa kuifanya. Pesa zinazopaswa kutumika katika kufanya kazi nzuri ya kujenga nyumba za ibada, za kuanzisha shule kwa madhumuni ya kuelimisha watenda kazi kwa ajili ya shamba la kimishenari, za kuelimisha na kufunza vijana wa kiume na wa kike ili waende na kufanya kazi kwa subira, kwa akili, na kwa ustahimilivu wote ili wapate kuwa mawakala ambao kupitia kwao watu wanaweza kutayarishwa kusimama katika siku kuu ya Mungu, inageuzwa kutoka kwa mkondo wa manufaa na baraka na kwenda kwenye mkondo wa uovu na laana.[GRCsw 28.2]

Sikukuu ya Mungu iko juu yetu, na inakuja haraka, na kuna kazi kubwa ya kufanywa, na ni lazima ifanywe haraka. Lakini tunaona kwamba kati ya kazi inayopaswa kufanywa, wapo wanaokiri kuamini Ukweli wa leo, ambao hawajui jinsi ya kutumia fedha walizokabidhiwa kwa hekima ili zifanye mengi zaidi, na kwa sababu ya ukosefu wa upole na unyenyekevu wa moyo, hawaoni jinsi kazi ya kufanywa ilivyo kubwa sana. Wale wote wanaojifunza juu ya Yesu watakuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Lakini wale waendao kutangaza makosa au mafundisho ya uongo, wakitumia wakati na fedha kwa ubatili tu, huwabambikia mizigo watenda kazi wa Kweli katika maeneo mapya yenye mzigo ulioongezeka tayari; na badala ya kutoa muda wao katika kutetea Ukweli,

wanalazimika kuipinga kazi ya wale wanaotangaza uwongo, wakidai kwamba wana ujumbe kutoka mbinguni.[GRCsw 28.3]

Ikiwa wale ambao wamefanya kazi ya aina hii wangehisi umuhimu wa kujibu maombi ya Kristo ambayo alitoa kwa Baba Yake kwa haki kabla ya kusulubishwa Kwake, ili wanafunzi wa Kristo wawe kitu kimoja kama alivyokuwa mmoja na Baba, -hawangekuwa wanapoteza fedha iliyokabidhiwa kwao na ambayo inahitajika sana kuendeleza Ukweli. Hawatapoteza muda na mali za thamani katika kusambaza makosa, na hivyo kulazimu kutenga muda wa watendakazi/vibarua kupinga na kuzima ushawishi wake mtendakazi mwenye makosa. Kazi ya mhusika huyu imepewa nguvu, si kutoka juu mbinguni, bali kutoka chini.[GRCsw 29.1]

"[10] Ni nani miongoni mwenu amchaye Bwana, aitiiye sauti ya mtumishi Wake? Yeye aendaye katika giza, wala hana nuru, naye alitumainia Jina la Bwana, na kumtegemea Mungu wake. [11] Tazama, ninyi nyote mwashao moto, mjifungiao hiyo mienge; endeni ninyi katika mwali wa moto wenu, na katikati ya mienge mliyoiwasha. Mtayapata haya kwa mkono wangu; mtalala kwa huzuni.." Ujumbe ambao umebebwa na wale ambao wametangaza kanisa kuwa Babeli wameleta hisia kwamba Mungu hana kanisa duniani Isaya 50:10,11.[GRCsw 29.2]

## Kanisa Hai

Je, Mungu hana kanisa lililo hai? Yeye Ana kanisa, lakini ni kanisa la wapiganaji, sio kanisa lenye ushindi [church militant and not church triumphant]. Tunasikitika kwamba wapo washiriki wenye kasoro, kwamba kuna magugu katikati ya ngano. Yesu alisema, ""Ufalme wa mbinguni unaweza kufananishwa na mtu aliyepanda mbegu nzuri katika shamba lake. Lakini watu walipokuwa wamelala, adui yake akaja na akapanda magugu katikati ya ngano, na akaenda zake. Ngano ilipoota na kuzaa, magugu nayo yakachipua.[GRCsw 29.3]

"Watumishi wa yule mwenye shamba wakamwendea, wakamwuliza, 'Bwana, si ulipanda mbegu nzuri shambani mwako? Imekuwaje kuna magugu?' Akawajibu, 'Adui ndiye amefanya jambo hili'. Wale watumishi wakamwuliza, 'Je, ungetaka tukayang'oe?' Lakini akasema, 'Hapana msiyang'oe, kwa maana huenda katika kung'oa magugu mkang'oa na ngano pia. Acheni ngano na magugu yakue pamoja mpaka wakati wa

mavuno. Wakati huo nitawaambia wavunaji wayang’oe magugu kwanza wayafunge katika matita tayari kwa kuchomwa moto, lakini waivune ngano na kuikusanya ghalani Mwangu. ”[GRCsw 30.1]

Katika mfano wa ngano na magugu, tunaona sababu ya magugu kutong'olewa; ili kwamba ngano isije ikakatwa na magugu. Maoni na maaamuzi ya mwanadamu yangefanya makosa makubwa. Lakini sasa badala ya kufanya kosa, na hata mche mmoja wa ngano kung'olewa, Bwana asema, “Acheni vyote viwili vikue pamoja mpaka wakati wa mavuno;” ndipo malaika watayakusanya magugu, ambayo yataharibiwa. Ingawa katika makanisa yetu, kuna wale wanaodai kuamini Ukweli wa hali ya juu, wapo walio na makosa na kama magugu kati ya ngano, Mungu ni mvumilivu na mwenye subira. Yeye huwakemea na kuwaonya wapotovu, lakini hawaangamizi wale ambao wanatamani kujifunza somo ambalo Yeye angewafundisha; Yeye hang’oi magugu kutoka kwa ngano. Magugu na ngano yanapaswa kukua pamoja, mpaka wakati wa mavuno; wakati ngano inapofikia ukuaji wake kamili na maendeleo, hata hivyo kwa sababu ya tabia yake wakati ikikomaa, itakuwa tofauti kabisa na magugu.[GRCsw 30.1]

Kanisa la Kristo duniani litakuwa si kamilifu, lakini Mungu haliangamizi kanisa Lake kwa sababu ya kutokamilika kwake. Kumekuwa na wale waliojawa na bidii na sio maarifa; ambao wangependa kulitakasa kanisa, na kung'oa magugu katikati ya ngano. Lakini Kristo ametoa nuru ya kipekee ya namna ya kushughulika pamoja na wale wanaokosea, na wale ambao hawajaongoka kanisani. Hakupaswi kuwa na hatua za ghafla hapa na pale bila mwendelezo, hatua za haraka za kuchukuliwa na washiriki wa kanisa katika kuwakatilia mbali wale ambao wanaweza kufikiriwa kuwa na kasoro ndani ya tabia zao. Magugu yataota kati ya ngano; lakini italeta madhara zaidi, kung'oa magugu, isipokuwa kwa njia iliyoamriwa na Mungu, yaacheni magugu kwa sasa. Wakati Bwana analeta ndani ya kanisa wale ambao wameongoka Kweli, Shetani wakati huohuo huleta kanisani watu ambao wameongoka bila kubadilishwa katika ushirika. Wakati Kristo anapanda mbegu njema, Shetani anapanda magugu. Kuna athari mbili zinazopingana mara kwa mara miongoni mwa washiriki wa kanisa. Ushawishi mmoja unafanya kazi kwa ajili ya utakaso wa kanisa, na mwingine kwa ajili ya kuwaharibu watu wa Mungu.[GRCsw 30.3]

Yesu alijua kwamba Yuda alikuwa na kasoro katika tabia, lakini licha ya hilo, alimkubali kama mmoja wa wanafunzi, na kutoa nafasi na upendeleo ule ule ambao Aliwapa wengine aliowateua. Yuda aliachwa bila udhuru katika uovu [31] ambao aliufuata baadaye. Yuda angeweza kuwa mtendaji wa Neno, kama ilivyokuwa hatimaye kwa Petro na Yakobo na Yohana na wanafunzi wengine. Yesu alitoa masomo ya thamani ya mafundisho ya imani, ili wale ambao walikuwa wakishirikiana Naye waweze kuongoka, na kuwa hakuna haja ya kung'ang'ania kasoro zilizoharibu tabia zao. *Review and Herald* , Agosti 29, Septemba 5, 1893. Imechapishwa tena katika Testimonies for Ministers *,* ukurasa wa 41-47.**[GRCsw 30.4]**

## Mpiganaji wa Kanisa

Baadhi ya watu wanaonekana kufikiri kwamba wanapoingia kanisani, matarajio yao yatatimizwa, kwani watakutana tu na wale ambao ni safi na kamili. Wana bidii katika imani yao, na wakati wao wanaona makosa katika washiriki wa kanisa, wanasema, "Tuliuacha ulimwengu ili tusishirikiane na watu wabaya, lakini ubaya uko hapa ndani pia; nao wanauliza, kama walivyouliza watumishi katika mfano huo, Je, magugu yametoka wapi basi?" Lakini sisi hatuhitaji kukatishwa tamaa namna hiyo, kwa vile Bwana hajatupa waranti/dhamana ya kufikia hitimisho kwamba kanisa ni kamilifu; na bidii yetu yote haitafanikiwa katika kufanya wapiganaji wa kanisa kuwa wapiganaji safi kama kanisa linaloshinda. Bwana ametukataza kutenda kwa njia yoyote ya jeuri dhidi ya wale ambao tunafikiri wamekosea, na hatupaswi kushughulika kwa kutenga na kukashifu wale mbao wana makosa.**[GRCsw 32.1]**

Mwanadamu mwenye ukomo ana uwezekano wa kuhukumu vibaya tabia, lakini Mungu haiachi kazi ya hukumu na kutamka juu ya tabia za wanadamu, kwa wale ambao hawafai kwa ajili ya kazi hii. Hatupaswi kusema ipi ni ngano, na yapi ni magugu. Wakati wa mavuno utaamua kikamilifu tabia ya makundi haya yaliyotajwa chini ya takwimu ya magugu na ngano. Kazi ya kutenganisha magugu na ngano, au watu wa Mungu na watu wa Shetani, imetolewa kwa malaika wa Mungu, na haijawekwa mikononi mwa mwanadamu yeyote.**[GRCsw 32.2]**

Mafundisho ya uwongo* ni mojawapo ya mvuto wa kishetani unaofanya kazi katika kanisa, na kuwaleta ndani yake wale ambao hawajaongoka moyoni [false doctrines]. Wanadamu hawayatii Maneno ya Yesu Kristo, na hivyo kutafuta umoja katika imani, roho, na mafundisho. Hawafanyi kazi kwa ajili ya umoja wa roho ambao Kristo aliomba, ambao ndio ungetoa ushuhuda wa wanafunzi wa Kristo wenye ufanisi katika kuushawishi ulimwengu kwamba Mungu alimtuma Mwana Wake ulimwenguni, "ili kila mtu amwaminiye asipate kupotea, bali uwe na uzima wa milele." Ikiwa umoja ambao Kristo aliuombea ungekuwepo miongoni mwa watu wa Mungu, basi wangetoa ushuhuda ulio hai, na Yeye angetuma nuru angavu kuangaza katikati ya giza la maadili Dunia.**[GRCsw 32.3]**

## Shetani Ameruhusiwa Kujaribu

Badala ya umoja unaopaswa kuwepo miongoni mwa waumini, kuna utengano; kwa maana Shetani ameruhusiwa kuingia na kupitia kwa ustadi wake wa hila na udanganyifu na imani potofu, huwaongoza wale wasiojifunza upole na unyenyekevu wa moyo wa Kristo, kuchukua mkondo tofauti kutoka kwa kanisa, na kuvunja, umoja wa kanisa, ikiwezekana. Watu huinuka wakisema mapotovu ili kuwavuta wanafunzi wawafuate wenyewe. Wanadai kwamba Mungu amewapa wao nuru kuu; lakini wanatendaje chini ya ushawishi Wake Bwana? Je, wanafuata mkondo wa wanafunzi wawili waliotembea katika safari yao ya kwenda Emau? [Luka 24:13-35] Wakati hawa wanafunzi walipopokea nuru, walirudi na kuwakuta wale ambao Mungu alikuwa amewaongoza na Alikuwa bado anaendelea kuwaongoza, akawaeleza jinsi walivyomwona Yesu na jinsi walivyomkuta njiani na kuzungumza Naye.**[GRCsw 32.4]**

Je, wanadamu ambao wamedai kuwa na nuru kuhusu kanisa, wameifuata njia hii? Je, wamekwenda kwa wale walioteuliwa na Mungu kutoa ushuhuda ulio hai, na kuwapa ushahidi kwamba nuru hii ingewastahilisha vyema kuwatayarisha wanadamu kusimama katika siku ile kuu ya Mungu? Je! wameomba ushauri kwa wale wanaobeba ile Kweli na ambao wanaendelea kuibeba ile Kweli, na kuupa ulimwengu ujumbe wa onyo la mwisho? Je, wameshauriana na wale waliopata uzoefu wa kina katika mambo ya Mungu? Kwa nini wanadamu hawa waliokuwa na usongo sana kwa ajili ya jambo hilo, hawakuwepo

kwenye mkutano wa Konferensi kuu au General Konferensi (GC) ulilofanyika huko Battle Creek, kama walivyokuwa watu wacha Mungu huko Yerusalemu wakati wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu? Katika moyo mkuu wa kazi, watu walifungua hazina zao za nuru; na wakati Bwana alipokuwa akimimina Roho Wake juu ya watu, Je, watu hawa hawakupokea kutoka mbinguni upako wa Roho Mtakatifu? Huku harakati za kina za Roho wa Mungu zikifanywa dhahiri miongoni mwa watu, na roho zikiwa zinaongoka, na mioyo migumu kuvunjika-vunjika, kulikuwa na wale ambao walikuwa wakisikiliza Mapendekezo ya Shetani, na wakajawa na bidii kutoka chini, na kwenda mbele na kutangaza kwamba watu wale ambao waliokuwa wanapokea kutoka kwa Roho Mtakatifu, mvua ya masika na utukufu utakaotia nuru dunia yote, walikuwa Babeli. Je! Bwana aliwapa wajumbe hawa ujumbe wao? Hapana, kwa kuwa haukuwa ujumbe wa Ukweli.**[GRCsw 33.1]**

## Kanisa Nuru ya Ulimwengu

Ingawa kuna maovu yaliyopo katika kanisa, na yatakuwepo mpaka mwisho wa dunia, kanisa katika siku hizi za mwisho linapaswa kuwa nuru ya ulimwengu uliochafuliwa na kuharibiwa na dhambi. Kanisa la Kristo, Japo limedhoofika na ni lenye kasoro nyingi, linalohitaji kukemewa, kuonywa na kushauriwa hili ndilo kitu pekee duniani ambacho Mungu amekitunukia heshima Yake kuu. Dunia ni karakana ambayo, kupitia ushirikiano wa mawakala wa kibinadamu na Kiungu, Yesu Yuko akifanya majaribio kwa neema Yake na rehema Zake za Kiungu juu ya mioyo ya wanadamu. Malaika wanashangaa wanapoona mabadiliko ya tabia inayoletwa ndani ya wale wanaojitoa wenyewe kwa Mungu, na kuonyesha furaha yao kwa kurindima nyimbo za sifa kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. Wanawaona wale ambao kwa asili ni watoto wa ghadhabu, wakiongoka na kuwa watenda kazi pamoja na Kristo katika kuzivuta na kuzileta roho kwa Mungu. Wanawaona wale waliokuwa gizani wakigeuka kuwa mianga na kuangaza katikati ya usiku wa kiadili wa kizazi hiki kiovu na kikaidi. Wanawaona wakijitayarisha kwa uzoefu kama wa Kristo, kwamba wateseke pamoja na Bwana wao Mlezi, na baadaye wawe washirika Wake katika utukufu Wake mbinguni juu.**[GRCsw 33.2]**

Mungu ana kanisa duniani ambalo linainua sheria Yake iliyokandamizwa, na kumwasilisha kwa ulimwengu Mwana-Kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu. Kanisa ni hazina ya mali ya utajiri wa neema ya Kristo, na kwa njia ya kanisa hatimaye litadhihirishwa onyesho la mwisho, na kamili la upendo wa Mungu kwa ulimwengu utakaoangazwa kwa utukufu Wake. Sala ya Kristo ili kanisa Lake liwe na umoja kama alivyokuwa umoja na Baba Yake hatimaye itajibiwa. Mahari nono ya Roho Mtakatifu itatolewa, na kupitia ugavi Wake wa kudumu kwa watu wa Mungu, watu hawa watafanywa kuwa mashahidi katika ulimwengu, kwa uweza wa Mungu uletao wokovu.**[GRCsw 34.1]**

## Kazi ya Kubomoa

Kuna kanisa moja tu ulimwenguni ambalo lipo kwa wakati wa sasa ambalo limesimama katika mvunjiko, na kujenga ua, kukarabati maeneo ya zamani yaliyoharibika; na kwa mtu yeyote kuvutia umakini wa ulimwengu na makanisa mengine kwa kanisa hili, wakilishutumu kama ndilo Babeli, ni kufanya kazi kwa mapatano na yeye ambaye ni mshitaki wa ndugu. Je, inawezekana kwamba watu watatokea kati yetu, wanaozungumza mambo mapotovu, na kutoa sauti kwa hisia zile zile ambazo Shetani anaeneza ulimwenguni kuhusiana na wale wanaoshika amri za Mungu, na kuwa na imani ya Yesu? Je, hakuna kazi za kutosha ili kutosheleza usongo wako katika kuwasilisha ile Kweli kwa wale ambao wako katika giza la upotovu? Kama wale ambao wamefanywa mawakili wa mali na uwezo, wewe umekuwa ukitumia vibaya mali za Bwana wako Mlezi katika kusambaza makosa. Ulimwengu wote umejaa chuki kwa hao wanaotangaza madai yenye mashiko ya sheria za Mungu, sheria tunayobidishwa kuitii, na kanisa ambalo ni adilifu kwa Yehova halipaswi kupigana vita vya kawaida. "Sisi hatushindani na damu na nyama, bali juu ya falme na mamlaka yenye nguvu, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya uovu wa kiroho mahali pa juu." Wale ambao wana utambuzi wowote wa maana ya vita hivi hawatageuza silaha zao na kupigana na wapiganaji vita wa kanisa au wanajeshi wa kanisa, lakini kwa nguvu zao zote watashindana wakiwa pamoja na watu wa Mungu dhidi ya muungano wa uovu. **[GRCsw 34.2]**

Wale wanaoanza kutangaza ujumbe kwa wajibu wao binafsi, ambao, ingawa wanadai kufundishwa na kuongozwa na Mungu, bado hufanya kazi yao maalum iwe

kubomoa kile ambacho Mungu amekuwa akikijenga kwa miaka, hakika hawa hawafanyi mapenzi ya Mungu. Hebu ifahamike kwamba watu hawa wako upande wa yule mdanganyifu mkuu. Msiwaamini watu hawa. Watu hawa wanajifungamanisha na maadui wa Mungu na Ukweli. Watadharau utaratibu wa huduma wakisema kwamba huo ni mfumo wa utumishi wa kazi ya Mungu ili kujipatia umashuhuri wa kisiasa, na kijamii na fedha (priestcraft). Jiepushe na watu kama hao, msishiriki jumbe zao, hata kama wanaweza kunukuu *Shuhuda* na kutafuta kujiimarisha nyuma yao. Msiwapokee, kwani Mungu hajawapa kufanya kazi hii. Matokeo ya kazi hiyo itakuwa kutoamini S*huhuda*, na, kadiri inavyowezekana, watafanya Shuhuda zisiwe na uzito au athari, kazi ambayo nimekuwa nikiifanya kwa miaka mingi. **[GRCsw 35.1]**

Takribani maisha yangu yote yametolewa kwa kazi hii, lakini mzigo wangu mara nyingi umefanywa kuwa mzito zaidi kwa kuibuka kwa watu waliokwenda kutangaza ujumbe ambao Mungu hakuwa amewapa. Kundi hili la watenda mabaya wamechagua sehemu za *Shuhuda* nilizoandika, na wameziweka katika mfumo wa makosa, ili kwa mpangilio huu watoe ushawishi kwa Shuhuda zao za uongo. Inapodhihirika kwamba ujumbe wao ni upotovu, Shuhuda zilizoletwa kwa mvuto wao zinaonekana kana kwamba zina makosa pia, na hivyo kushiriki hukumu sawa; na watu wa ulimwengu, ambao hawajui kwamba *Shuhuda* zilizonukuliwa ni dondoo tu kutoka kwa barua-binafsi za watu (waliojitungia au kuongeza kutoka kwenye maandishi ya RohoYaUnabii), na kuyatumia/zilizotumiwa bila idhini yangu, huwasilisha mambo haya kama ushahidi kwamba kazi yangu si ya Mungu, au ya Ukweli, bali ya uongo. Wale wanaoiletea kazi ya Mungu sifa mbaya hivyo, itawabidi kujibu mbele za Mungu kwa kazi wanayofanya. -*Review na Herald*, Septemba 5, 1893. Reprinted *Testimonies to Ministers* , ukurasa wa 47-52.**[GRCsw 35.2]**

### Huduma Iliyoteuliwa na Mungu

Mungu ana kanisa, na ana huduma iliyowekwa Naye. "Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana

Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike Kweli katika upendo na kukua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye aliye kichwa, Kristo. Katika Yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo. Efeso 4:11-16." **[GRCsw 36.1]**

Bwana ana wakala Wake aliowateua, na kanisa ambalo limeishi kupitia mateso, migogoro na giza. Yesu analipenda kanisa, na akajitoa kwa ajili Yake, Naye atalijaziliza, atalisafisha, ataliboresha, atalitukuza, na atalinyanyua, ili lisimame imara katikati ya athari za uharibifu za dunia hii. Wanadamu walioteuliwa na Mungu wamechaguliwa kukesha na kulilinda pamoja kwa utunzaji wenye wivu, kwa uvumilivu wa kukesha, ili kanisa lisiweze kuangushwa na hila mbaya za Shetani, lakini kwamba litasimama ndani ya ulimwengu ili kufanya promosheni kwa utukufu wa Mungu kati ya wanadamu. Daima kutakuwa mzozo mkali kati ya kanisa na ulimwengu. Akili itakuja katika kuwasiliana na akili, kanuni na kanuni, ukweli na makosa; lakini katika mgogoro ambao hivi karibuni utafikia kilele, ambao tayari umeanza, watu wenye uzoefu watapaswa kufanya kazi yao waliyopewa na Mungu, na kuzilinda nafsi, kama wale ambao wanapaswa kutoa hesabu. **[GRCsw 36.2]**

Wale wanaobeba ujumbe huu wa makosa, wakilikemea na kulikanusha kanisa kama ndiyo Babeli, wanaipinga kazi yao waliyopangiwa na Mungu, wanafanya kazi kinyume na taasisi ya kanisa, kinyume na amri ya Mungu ya wazi, iliyonenwa na Malaki kuhusiana na kuleta zaka zote ndani ya hazina ya nyumba ya Mungu, na kufikiri kwamba wana kazi ya kufanya katika kuwaonya wale ambao Mungu amewachagua kusambaza ujumbe Wake wa Ukweli. Watendakazi hawa hawaleti ufanisi katika kusudi la kazi ya ufalme wa Mungu, lakini wanajishughulisha na kazi inayofanana na ile ambayo adui wa haki yote anahusika nayo. Hebu hawa watu wanaoinuka dhidi ya njia na mali zilizowekwa na Mungu ili kuiendeleza kazi Yake

katika siku hizi za hatari, wajitenge na Maoni yote yasiyo ya Kimaandiko kuhusu asili, ofisi/kazi, na nguvu ya mawakala walioteuliwa na Mungu. **[GRCsw 36.3]**

Hebu watu wote waelewe maneno ambayo ninayaandika sasa. Wale walio watenda-kazi pamoja na Mwenyezi Mungu ni vyombo Vyake, na wao ndani ya nafsi zao wenyewe, hawana neema au utakatifu wa kipekee au ulio muhimu. Ni wakati tu wanaposhirikiana na akili za mbinguni ndiyo hufanikiwa. Wao ni vyombo vya udongo tu, maghala ambayo Mwenyezi Mungu anaweka hazina ya Ukweli Wake. Paulo anaweza kupanda, na Apolo akamwagilia maji, lakini Mungu pekee Ndiye hukuza. **[GRCsw 37.1]**

Mungu huzungumza kupitia wakala Wake aliowateua, na Yeye haruhusu mtu yeyote, au muungano wa watu, kumtukana Roho wa Mungu kwa kukataa kusikia ujumbe wa Neno la Mungu kutoka kwa midomo ya wajumbe Wake wateule. Kwa kukataa kusikia ujumbe wa Mungu, wanadamu hujifungia ndani ya chumba cha giza: Hujifungia nafsi zao mbali na eneo lenye baraka kubwa na anuwai; na kumnyang'anya Kristo utukufu unaopaswa kuja Kwake, kwa kuonyesha kutoheshimu watu Wake aliowateua. **[GRCsw 37.2]**

## Jihadhari na Walimu wa Uongo

Mungu si mwanzilishi wa machafuko, bali wa amani. Lakini Shetani ni adui aliye macho, asiyelala, na anayefanya kazi daima juu ya akili za wanadamu, akitafuta ardhi ambayo anaweza kupanda magugu yake. Akimpata yeyote ambaye anaweza kumshinikiza ili aingie huduma yake, atapendekeza mawazo na nadharia za uongo, na kuwafanya watu wawe wenye usongo katika kutetea makosa. Ukweli hauongoi watu tu, bali pia hufanya utakaso kwa mpokeaji wake. Yesu ametuonya tujihadhari na walimu wa uongo. Tangu mwanzo wa kazi yetu, wamekuwa wakitokea watu mara kwa mara, ambao hutetea nadharia ambazo zilikuwa mpya na za kushtua. Endapo wale wanaodai kuamini Ukweli wangeenda kwa wale ambao wamekuwa na uzoefu, waende kwa Neno la Mungu na kwa roho inayofundishika, roho ya unyenyekevu, na kuzichunguza nadharia zao katika nuru ya Ukweli na kwa msaada wa akina ndugu ambao wamekuwa wanafunzi wa Biblia wenye bidii na uadilifu, na wakati huo huo wamwombe Mungu, wakiuliza, Je! Hii ni njia ya Bwana, au ni njia ya uongo ambayo Shetani ameniongoza mimi kuipitia? Basi watu hawa wangepokea nuru, na wangetoka nje ya wavu uliotegwa na mwindaji wa ndege.**[GRCsw 37.3]**

Hebu ndugu na dada zetu wote wajihadhari na mtu yeyote ambaye anaweka muda bainishi au tarehe ya wakati wa Bwana kutimiza Neno Lake kuhusu kuja Kwake, au kuhusiana na ahadi nyingine yoyote alizotoa zenye umuhimu maalum. "**Si kazi yenu kujua nyakati wala majira**, **Baba** aliyoyaweka **katika** mamlaka Yake **Mwenyewe**." Walimu wa uwongo wanaweza

kuonekana kuwa wenye usongo/bidii sana kwa ajili ya kazi ya Mungu, na wanaweza kutumia fedha ili kuwaletea watu nadharia ulimwenguni na kanisani; lakini wanapochanganya makosa na Ukweli, ujumbe wao ni wa udanganyifu, na utaongoza roho za watu kwenye njia za uwongo. Watu hawa mnapaswa kukutana nao katika kushugulikia hizi mada zao na wanapaswa kupingwa, si kwa sababu wao ni watu wabaya, lakini kwa sababu wao ni walimu wa uwongo na ni walimu wanaojaribu kuweka muhuri wa ile Kweli juu ya uwongo wao.**[GRCsw 37.4]**

Ni jambo la kusikitisha namna gani, kwamba wanadamu wanahenyeka sana ili tu wagundue baadhi ya nadharia za makosa wakati kuna ghala za hazina nyingi zenye vito vya thamani vya ile Kweli ambazokwa hizo, watu wangetajirishwa katika imani takatifu sana. Badala ya kufundisha Ukweli, wanaacha mawazo yao yakae juu ya hilo ambalo ni jipya, geni na la ajabu au kushtua, na kujitupa nje ya mapatano na wale ambao Mungu anawatumia kuwaleta watu juu ya jukwaa ya Ukweli. Wanatupilia mbali yote yaliyosemwa kuhusiana na umoja wa mguso na hisia, na kukanyaga sala ya Kristo kana kwamba umoja ambao Masihi aliuombea haukuwa wa lazima, na kwamba haikuwa lazima kwa wafuasi Wake kuwa kitu kimoja, kama vile Yeye alivyo umoja pamoja na Baba [Yohana 17]. Wanaenda nje ya ulingo, kama Yehu, wanawaita ndugu kufuata mfano wao wa usongo kwa ajili ya Bwana [2 Wafalme 10-Yehu kwanza alifanya mapenzi ya Mungu kwa kumshugulikia Yezebeli, baadaye akatoka na kuanza kuweka madhabahu ya Baali] . **[GRCsw 38.1]**

Ikiwa bidii yao iliwaongoza kufanya kazi katika mistari ile ile ambayo ndugu zao walibeba kazi yenye changamoto na mzigo katika joto la mchana la siku, katika kazi ya Bwana wanayofanya; kama wangevumilia na kushinda hali ya kukatishwa tamaa na vizuizi kama vile ndugu zao walivyoshinda, wanaweza kuigwa vyema, na Mungu angewakubali. Lakini wanadamu wanaoanza kwa tangazo la nuru ya ajabu, na kisha wanaondoka kutoka kwa mawakala ambao Mungu anawaongoza, wanapaswa

kuhukumiwa. Hii ilikuwa ni njia ambayo Kora, Dathani na Abiramu walienenda, na kitendo chao kimeandikwa kama onyo kwa wengine wote. Hatupaswi kufanya kama walivyofanya-kuwatuhumu na kuwalaani wale ambao Mungu ameweka mzigo wa kazi juu yao.**[GRCsw 38.2]**

Wale ambao wametangaza Kanisa la Waadventista Wasabato kuwa ndiyo Babeli, wametumia Shuhuda nilizoandika ili kutetea msimamo wao; lakini kwa nini hawakuwasilisha kile ambacho kwa miaka mingi kimekuwa mzigo wa ujumbe wangu-yaani umoja wa kanisa? Kwa nini hawakunukuu maneno ya malaika, "Shikaneni pamoja, Shirikianeni pamoja, Vuteni pamoja-Press together"? Kwa nini hawakurudia mawaidha na kutaja kanuni, kwamba "katika muungano kuna nguvu, katika utengano kuna udhaifu -umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu"? Ni jumbe kama hizo ndizo ambazo watu hawa wamebeba, na ambazo zinaligawanya kanisa, na kututia aibu mbele ya maadui wa ile Kweli, na katika jumbe kama hizo panadhihirishwa kwa uwazi utendajikazi wa kipekee wa yule adui na mdanganyifu mkuu, ambaye huzuia kanisa kufikia umoja kwa ukamilifu-umoja kamili. Walimu hawa wanazifuata cheche za moto waliouwasha wao wenyewe [sio moto wa Bwana], wanaenenda kulingana na maamuzi yao wenyewe, na wanausumbua Ukweli kwa kuugandamiza kwa dhana na nadharia potofu. Wanakataa shauri la ndugu zao, wanaendelea katika njia yao wenyewe mpaka wanakuwa vile tu ambavyo Shetani angetamani kuwafanya wawe—watu wasio na msawaziko au utimamu akilini.**[GRCsw 38.3]**

Nawaonya ndugu zangu wajilinde na utendaji wa Shetani katika jambo la kila aina. Adui mkuu wa Mungu na mwanadamu anashangilia leo kwamba yeye amefaulu kuzihadaa nafsi, na kuchepusha kando mali zao na uwezo wao kwenye mikondo hatarishi. Pesa zao zingeweza kutumika ili kuendeleza Ukweli wa sasa, lakini badala ya hii, zimetumiwa katika kuwasilisha mawazo ambayo hayana msingi katika ile Kweli.**[GRCsw 39.1]**

## Mfano Mwingine

Mnamo 1845, mtu mmoja kwa jina Curtis alifanya kazi kama hiyo katika Jimbo la Massachusetts, Marekani. Aliwasilisha fundisho la uwongo, na kuzisuka katika nadharia zake sentensi na nukuu kutoka katika Shuhuda, na alizichapisha nadharia

zake katika gazeti la *Day Star*, kama makabrasha. Kwa miaka kadhaa, kazi hizi zilizaa matunda yake mabaya na kuleta lawama juu ya *Shuhuda,* ambazo, kwa ujumla wake, hazikuunga mkono kwa njia yoyote kazi yake. Mume wangu alimwandikia, na kumuuliza anamaanisha nini kwa kuwasilisha *Shuhuda* na kuziunganisha na maneno yake mwenyewe, tukamwomba kwamba aunge mkono yale tuliyoyapinga na kumuomba afanye hivyo kwa kusahihisha maoni ambayo kazi yake ilitoa. Alikataa katakata kufanya hivyo, akisema kwamba nadharia zake zilikuwa za kweli, na kwamba maono niliyopewa yanapaswa kuthibitishwa kwa maoni yake mwenyewe, na kwamba hayo yaliunga mkono kabisa, lakini kwamba nilikuwa nimesahau kuandika mambo ambayo yalifanya nadharia zake kuwa wazi.**[GRCsw 39.2]**

Tangu mwanzo wa kazi, mtu mmoja baada ya mwingine ameinuka na kufanya kazi ya aina hii, na nimepata shida ya kuingia kwenye gharama ya kupinga uwongo huu. Watu wamechapisha nadharia zao, na wamedanganya watu wengi, hebu Mungu Mwenyewe awalinde kondoo wa malisho Yake. *Review and Herald*, Septemba 12, 1893. Reprinted from Testimonies for the Ministers *(Angalia katika MaarifaMtandaoni.Com nakala ya Kiswahili)*, ukurasa wa 52-57.**[GRCsw 39.3]**

## Mungu Ana Kanisa

Ninawasihi wale wanaodai kuamini Ukweli, waenende kwa umoja na ndugu zao. Usitafute kutoa fursa kwa ulimwengu kusema kwamba sisi ni watu wenye msimamo unaopitiliza au mashabiki, tusiotumia busara, kwamba tumetengana, kwamba mtu mmoja anafundisha jambo moja, na mtu mwingine anafundisha lingine kabisa. Epuka mifarakano. Hebu kila mtu awe macho, na kuwa mwangalifu, na kisha apatikane amesimama kwenye ufa ili kurekebisha mpasuko/mvunjiko [isaya 58:2], badala ya kusimama kwenye ukuta ili kuleta mpasuko au pengo. Hebu waamini wote wawe waangalifu kwa kutotoa kilio cha hasira dhidi ya watu pekee ambao wako hapo kutimiza maelezo yaliyotolewa kwa watu wa masalio, wanaozishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, wale ambao wanainua kiwango cha haki katika siku hizi za mwisho.**[GRCsw 40.1]**

Mungu ana watu bainishi/maalumu, kanisa Lake duniani, hili ni la pili na hakuna jingine kama hili, lakini ni bora katika yote kwenye vituo vyake vya kufundisha Ukweli, nakutetea sheria ya Mungu [Kanisa la mbinguni ni kanisa la kwanza na la ushindi, la

malaika nk]. Mungu ana mawakala aliowateua - watu ambao Yeye ni Kiongozi wao, ambao wamebeba joto la changamoto na mzigo wa siku, ambao wanashirikiana na vyombo vya mbinguni vya kuendeleza Ufalme wa Kristo katika ulimwengu wetu. Hebu wote waungane na mawakala hawa waliochaguliwa na Mungu, na hatimaye wapatikane miongoni mwa watakatifu wenye subira na ambao huzishika amri za Mungu, na kuwa na imani ya Yesu.**[GRCsw 40.2]**

Barua

Ifuatayo ni barua iliyotumwa kwa Ndugu S.: **[GRCsw 40.3]**

**Napier, New Zealand**

**Machi 23, 1893.**

"*Ndugu Mpendwa S.:*

“Naandika kwako mistari michache. Sipatani na msimamo uliouchukua, kwa kuwa nimeonyeshwa na Bwana kwamba msimamo huo utachukuliwa na wale walio katika makosa. Paulo alitupa onyo hili: 'Basi Roho anena waziwazi; ya kwamba nyakati za mwisho, wengine watajitenga na imani wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani.' “Ndugu yangu nimesikia kwamba unachukua msimamo kuwa Kanisa la Waadventista Wa Sabato ndiyo Babeli, na kwamba wote ambao wangeokolewa lazima watoke ndani yake. Shetani amewadanganya wengine katika hili, wewe hauko peke yako katika uongo huu. Kwa miaka arobaini huko nyuma, mtu mmoja baada ya mwingine ametokea, akidai kwamba Bwana amemtuma na ujumbe ule ule; lakini wacha nikuambie kama ambavyo nimewaambia wengine, ya kwamba ujumbe huu mnaotangaza ni mojawapo wa udanganyifu wa kishetani uliokusudiwa kuleta mkanganyiko kati ya makanisa. **[GRCsw 40.4]**

“Ndugu yangu, hakika umetoka nje ya njia. Ujumbe wa malaika wa pili ulikuwa uende Babeli [makanisa ambayo hayashiki amri za Mungu] na kutangaza anguko lake, na kuwaita watu watoke kwake. Ujumbe huu-huu utatangazwa mara ya pili. 'Na baada ya mambo hayo nikaona malaika mwingine anashuka kutoka mbinguni, mwenye uwezo mkuu; na dunia iliangazwa kwa utukufu wake. Naye akalia kwa nguvu sauti kuu, ikisema, Umeanguka, umeanguka, umeanguka Babeli ule mji mkuu kwa kuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu na ngome ya kila ndege mchafu na

mwenye kuchukiza. Kwa maana mataifa yote yamekunywa mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake. Nao wafalme wa dunia wamefanya uzinzi naye, na wafanyabiashara wa dunia wametajirika kutokana na wingi wa utajiri wake."**[GRCsw 41.1]**

Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. "Ndugu yangu, wewe kama unafundisha kwamba Kanisa la Waadventista Wasabato ni Babeli, unakosea. Mungu hajakupa ubebe ujumbe wa namna hiyo. Shetani ataitumia kila akili ambayo anaweza kuifikia, na akiichochea ili watu waanzishe nadharia za uongo au kwenda mbali na ulingo wa Maandiko au mada ya Maandiko,, ili apate kuleta msisimko wa uongo, na hivyo kugeuza roho za watu kutoka kwenye suala la Ukweli wa wakati huu. Ninadhani kwamba kuna watu wengine ambao wanaweza kudanganywa na ujumbe wako, kwa sababu wamejaa mioyoni mwao udadisi na hamu ya kitu kipya.**[GRCsw 41.2]**

"Ninanisikitishwa sana kwamba unakubali udanganywe kwa njia yoyote kwa kupokea mapendekezo ya adui; maana najua nadharia hiyo unayoitetea sio Ukweli. Katika kuendeleza mawazo hayo kama unavyofanya, wewe utajidhuru mwenyewe na wengine pia. Usitafute kutafsiri vibaya, na kupindisha Ukweli, na kupotosha Shuhuda ili kuthibitisha ujumbe wowote kama huo wa makosa. Wengi wamepita juu ya ardhi hii, na wamefanya madhara makubwa. Hata wengine wameanza kujaa usongo katika kutangaza ujumbe huu, tena na tena, nimeonyeshwa kuwa huu sio Ukweli.**[GRCsw 41.2]**

Naelewa kwamba wewe unawatangazia watu pia kwamba wasirudishe zaka. Ndugu yangu, 'Vua viatu vya miguuni yako;' kwa maana mahali unaposimama ni mahali Patakatifu. Bwana amezungumza kuhusiana na kutoa zaka. Amesema, 'Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya

wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema BWANA wa majeshi' Wakati Yeye anatamka baraka juu ya wale warudishao zaka zao, Yeye pia anatangaza laana juu ya wale wanaowazuia watu wasipeleke zaka zao au wasiopeleka wenyewe. Hivi majuzi nimepata mwangaza wa moja kwa moja kutoka kwa Bwana juu ya swala hili, kwamba Waadventista Wasabato wengi wamekuwa wakimwibia Mungu zaka na matoleo/sadaka, na ilifunuliwa wazi kwangu kwamba Malaki ameelezea kesi hii jinsi ilivyo. Basi mtu yeyote anawezaje kuthubutu moyoni mwake kufikiri kwamba pendekezo la kuzuia zaka na matoleo latoka kwa Bwana? Ni wapi ndugu yangu ulipochepuka na kutoka nje ya njia? Lo, rudisha miguu yako kwenye njia iliyonyooka tena.**[GRCsw 42.1]**

"Tuko karibu na mwisho, lakini ikiwa wewe au mtu mwingine atadanganywa na adui, na kuongozwa katika kuweka tarehe au wakati bainishi wa kuja kwa Kristo, atakuwa anafanya kazi ile ile mbaya ambayo imesababisha uharibifu wa roho kama wale waliofanya hivyo siku za huko nyuma.**[GRCsw 42.2]**

“Kama wewe umevaa nira ya Kristo, na ikiwa unauinua mzigo Wake, utaona kwamba kuna mengi ya kufanya katika mistari hiyo hiyo ambamo watumishi wa Mungu wanataabika katika kumhubiri Kristo na Yeye Alisulubiwa. Lakini mtu yeyote yule, ambaye ataanza kutangaza ujumbe kwa kutangaza saa, siku, au mwaka wa kuonekana kwa kwa Kristo mara ya pili, atakuwa amevaa nira isiyo ya Kristo, na kutangaza ujumbe ambao Bwana hajawahi kumpa.**[GRCsw 42.3]**

“Mungu ana kanisa duniani ambao ni wateule Wake, wanaozishika amri Zake. Yeye Ndiye ayenaongoza, sio machipukizi yanayoota tofauti au matawi yanayoota nje ya mpango Wake [offshoot], moja hapa na jingine pale, bali watu. Ukweli ni nguvu ya utakaso; lakini Kanisa lililo vitani sio Kanisa ambalo limeshinda vita [The church militant is not the church Triumpanth]. Humo kuna magugu kati ya ngano. 'Je, wewe unataka tuyangoe magugu, na kuyakusanya na kuyatupa?' lilikuwa swali la mtumishi; lakini yule bwana akajibu, La; msije mkatoa magugu na, mkang'oa na ngano pia.' Wavu wa injili hauvuti samaki wazuri tu, bali wabaya pia, na Bwana pekee Ndiye anayejua walio Wake.**[GRCsw 42.4]**

“Ni wajibu wetu binafsi kutembea kwa unyenyekevu na Mungu. Hatupaswi kutafuta ujumbe wowote wa ajabu, mpya au mgeni kabisa. Hatupaswi kufikiri kwamba wateule wa Mungu wanaojaribu kutembea katika nuru ni sehemu ya Babeli. Makanisa ya madhehebu yaliyoanguka ni Babeli. Babeli amekuwa akikuza mafundisho yenye sumu, divai ya upotovu. Mvinyo huu wa makosa unajumuisha mafundisho ya uwongo, kama vile asili ya kutokufa kwa roho [au mtu kwenda mbinguni mara anapokufa], mateso ya milele ya Jehanamu kwa waovu, kukana kwa uwepo wa Kristo kabla ya kuzaliwa Kwake katika mwili pale Bethlehemu, na kutetea na kuinua siku ya kwanza ya juma ya Jumapili, kuwa ndiyo siku takatifu ya Mungu ya Kutoka 20:8-11, badala ya Jumamosi. Makosa haya yanayoshabihiana ambayo ni mafundisho ya uongo yenye udugu [kindred errors], yanawasilishwa kwa ulimwengu na makanisa mbalimbali, na hivyo Maandiko yasemayo maneno haya hutimia, “Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake”. Ghadhabu inatokana na kuwa na mafundisho ya uongo, na wakati wafalme na maraisi wa nchi wanakunywa mvinyo hii ya ghadhabu ya uasherati wake, wanachochwa na hasira dhidi ya wale ambao hawana mapatano na uzushi na uongo wa kishetani unaoitukuza sabato ya uongo ya Jumapili badala ya Jumamosi, na kuwaongoza wanadamu kukanyaga kumbukizi za Mungu.**[GRCsw 42.5]**

“Malaika walioanguka duniani hufanya ushirika na watu waovu. Katika wakati huu mpinga-Kristo atatokea kama Kristo wa kweli, na kisha sheria ya Mungu itabatilishwa kabisa katika mataifa ya ulimwengu wetu. Uasi kinyume na sheria takatifu ya Mungu utakuwa umeiva kabisa. Lakini kiongozi wa Kweli wa uasi huu wote ni Shetani aliyejivika kama malaika wa nuru. Wanadamu watakuwa wamedanganywa na watamwinua Shetani katika nafasi ya Mungu, na kumfanya kuwa mungu. Lakini Yeye ambaye Ndiye Mweza wa Yote, ataingilia kati, na kwa yale makanisa yaliyoasi yanayoungana katika kuinuliwa kwa Shetani, hukumu itatolewa kwao, '*8* Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni Mwenye nguvu.*9* Na hao wafalme wa nchi, waliozini naye na kufanya anasa pamoja naye, watalia na kumwombolezea; wauonapo moshi wa kuungua kwake; *10* wakisimama mbali kwa

hofu ya maumivu yake, wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu, Babeli, mji ule ulio na nguvu! Kwa kuwa katika saa moja hukumu yako imekuja.Ufunuo 18 ”- *Review and Herald* , Septemba 12, 1893. Imechapishwa tena ndani Shuhuda kwa Wachungaji , ukurasa wa 57-62.**[GRCsw 43.1]**

## Upendo wa Mungu kwa Kanisa Lake

### Barua nyingine

**Wellington, New Zealand**

**Juni 11, 1893.**

Ndugu C.:

Bwana hajakupa ujumbe wa kuliita kanisa la Waadventista wa Sabato Babeli, na kuwaita watu wa Mungu kutoka ndani yake. Sababu zote unazoweza kuwasilisha haziwezi kuwa na uzito kwangu juu ya mada hii; kwa sababu Bwana amenipa nuru iliyokusudiwa, ambayo kinyume na ujumbe kama huo wako.**[GRCsw 44.1]**

Sina shaka na udhati au uadilifu wako. Nimeandika kwa muda mrefu barua kwa nyakati tofauti-tofauti kwa wale waliokuwa wakilishutumu kanisa ya Waadventista Wasabato kuwa ndilo Babeli, kwamba hakika hawashughulikii kuubeba Ukweli. Je, unafikiri watu binafsi wameipindisha akili yangu na kuifanya iwe na ubaguzi. Ikiwa nipo katika hali hiyo, sistahili kuaminiwa na kazi ya Mungu. Lakini jambo hili limeletwa akilini mwangu katika visa vingine ambapo watu binafsi wamedai kuwa na ujumbe kwa ajili ya kanisa la Waadventista wa Sabato, wenye tabia kama hiyo, na neno nililopewa kwangu ni, “Usiwaamini.” “Mimi sijawatuma, na bado watu hao wanakimbia mbio.”**[GRCsw 44.2]**

Mungu anaongoza watu. Yeye Ana watu waliochaguliwa, kanisa Lake lililo ulimwenguni, ambalo amelifanya kuwa kuwa ghala la hazina ya sheria Yake. Yeye amelikabidhi hili amana takatifu na Ukweli wa milele utakaotolewa kwa Dunia. Yeye atawakemea na kuwarekebisha. Ujumbe kwa Walaodikia unatumika kwa Waadventista wa Sabato ambao wamekuwa na nuru kubwa ila hawakutembea katika nuru. Ni wale ambao wamekiri kwa mdomo tu kwa namna kubwa, lakini hawajaendana na hatua/nyayo za Kiongozi wao, ndio ambao watatapikwa kutoka katika kinywa Chake wasipotubu. Ujumbe wa kutamka kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato ni Babeli, na kuwaita watu wa Mungu kutoka kwa hilo kanisa, hautoki kwa mjumbe yeyote wa

mbinguni, au wakala yeyote wa kianadamu aliyevuviwa na Roho wa Mungu. [GRCsw 44.3]

Shahidi wa Kweli asema, "[18] Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. [19] Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. [20] Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia Kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. [21] Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti chake cha enzi. [22] Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.[GRCsw 45.1]

### "Nakemea na kuadhibu"

Yesu anakuja ndani ili kuwapa washiriki binafsi wa kanisa baraka nyingi zaidi, ikiwa watamfungulia mlango. Yeye hakuwaita Babeli hata mara moja, wala kuwaomba watoke nje. Lakini Anasema, "Wote niwapendao Mimi huwakemea na kuwarudi" (kwa jumbe za karipio na onyo). Karipio hizi mimi sio mjinga vile, hata nisizifahamu. Nimetoa maonyo kwa sababu Roho wa Bwana amenibidisha kufanya hivyo, na kukemea kwa sababu Bwana amenipa Maneno ya karipio. Mimi sikujiepusha kutangaza kusudi lote la Mungu, ambalo nimepewa kwa ajili ya kanisa. Nitasema kwa hofu na upendo wa Mungu, najua kwamba Bwana ana mawazo ya upendo na rehema, katika kuwarejesha na kuwaponya watu, kwa kurudi nyuma kwao na maasi yao yote. Yeye Ana kazi kwa Kanisa Lake kufanya. Kanisa la Waadventista wa Sabato halipaswi kutangazwa kama ndilo Babeli, bali linapaswa kuwa kama chumvi ya dunia, nuru kwa ulimwengu. Watu wake wanapaswa kuwa wajumbe walio hai ili kutangaza ujumbe ulio hai katika siku hizi za mwisho. [GRCsw 45.2]

### Kanisa Lisivunjwe

Nasema tena, Bwana hakunena kupitia mjumbe yeyote ambaye analiita kanisa linalozishika amri za Mungu, kwamba ndiyo Babeli. Ni kweli, kuna magugu pamoja na ngano pamoja; lakini Kristo alisema angetuma Malaika Zake wakusanye kwanza magugu na kuyafunga kwenye matita ili yaunguzwe, lakini ngano ikusanywe ghalani.

Najua kwamba Bwana analipenda kanisa Lake. Kanisa halipaswi kuwa bila mpangilio au kuvunjwa katika atomi za zinazojitegemea. Hakuna uthabiti hata kidogo katika hili; hakuna ushahidi hata mdogo kabisa kuwa jambo kama hilo lipo au litakuwepo. Wale ambao watasikiliza ujumbe huu wa uwongo na wajaribu kuwatia wengine chachu, watadanganyika na watakuwa tayari kupokea udanganyifu mkubwa zaidi, na shauri lao litabatilika, na wala halitasimama Isaya 8:10. Kuna baadhi ya washiriki wa kanisa wenye kiburi, wenye kujitosheleza wenyewe, wana ukaidi wa kutoamini, na kukataa kuacha mawazo yao, ingawa ushahidi juu ya ushahidi unaweza kukusanywai, hii inatimiza maneno ya ujumbe kwa kanisa la Laodikia. Lakini hilo halitalifuta kanisa, kwamba lisiwepo tena. Acha magugu na ngano vikue pamoja mpaka wakati wa mavuno. Kisha ni kazi ya Malaika kufanya kazi ya kutenganisha ngano na magugu. **[GRCsw 45.2]**

Ninalionya Kanisa la Waadventista Wasabato kuwa makini jinsi mnavyofanya katika kupokea kila dhana mpya kutoka kwa wale wanaodai kuwa na nuru kubwa. Tabia ya kazi yao inaonekana kushtaki na kubomoa. Waumini waisikilize sauti ya malaika ambaye ameliambia kanisa, “Shikaneni kwa umoja -Press together.” Katika umoja ndipo ipo nguvu yako. Pendaneni kama ndugu, iweni na huruma kwa kusikitiana, iweni na uungwana na adabu. Mungu analo kanisa, na Kristo ametangaza, "Milango ya kuzimu haitalishinda." The Messengers the Lord Sends, bear the divine credentials.- *Review and Herald , Sept. 19, 1893.* **[GRCsw 46.1]**

# Sehemu ya Tatu - Ushindi wa Kanisa

---

* Uhakikisho wa upendo wa Mungu kwa kanisa Lake, uliotolewa kwa uwazi sana mwaka wa 1893, na kurudiwa katika miaka iliyofuata tena na tena. Mpaka karibu sana na mwisho wa maisha Ellen G. White, Bwana aliwahakikishia watu Wake ushindi wa Kanisa la Waadventista Wa Sabato. Mkusanyiko wa kauli hizi zinazorudiwa kutoka kwenye nukuu za Ellen G. White zimetoka kwenye mswada wa maandishi yake [Manuscript release files] na kutoka katika makala zake zilizochapishwa katika majarida ya dhehebu, zikijumuisha sehemu hii ya kuhitimisha hiki kitabu.-[Trustees of the Ellen G. White Publications.] **[GRCsw 46.1]**

## Uhakikisho Unaorudiwa Mara Kwa Mara

Baba anawapenda watu Wake leo kama anavyompenda Mwanawe Mwenyewe. Siku moja itakuwa fursa kwetu kumuona uso kwa uso.-MS. 103, 1903. (Imeandikwa Septemba 15, 1902.) **[GRCsw 47.1]**

Tunapaswa kukumbuka kwamba kanisa la Kristo, Japo limedhoofika na ni lenye kasoro nyingi, hili ndilo kitu pekee duniani ambacho Mungu amekitunukia umakini, upendeleo na heshima Yake ya hali ya juu. Yeye Analitazama na kulilinda kila mara kwa ukaribu, na analitia nguvu kwa Roho Wake Mtakatifu.-MS. 155, 1902. (Nov. 22, 1902.) **[GRCsw 47.2]**

Amini ulinzi na uongozi wa Mungu [guardianship]. Kanisa Lake linapaswa kufundishwa. Japo kanisa limedhoofika na ni lenye kasoro, ndilo chombo pekee ambacho Yeye amekitunukia heshima Yake ya hali ya Juu, umakini na upendeleo.-Barua 279, 1904.(Agosti 1, 1904.) **[GRCsw 47.3]**

Yeye Anaitazama kila mara kwa ukaribu, na analitia nguvu kwa Roho Wake Mtakatifu.-MS. 155, 1902.

## Daima Linasonga Mbele na kufikia Maeneo Mapya

Kanisa linapaswa kuongezeka katika utendaji na kupanua mipaka yake. Juhudi zetu za kimishenari zinapaswa kupanuka; ni lazima tupanue mipaka yetu. . . ...**[GRCsw 47.4]**

Japokuwa kumekuwa na malumbano makali katika juhudi za kudumisha sifa yetu bainishi/tofauti na wengine, lakini bado sisi kama Wakristo wa Biblia tunasonga mbele na kufikia maeneno mapya. Tunapoendelea kukumbuka kwamba kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima, tunapaswa kufanya kazi kwa bidii, daima kuomba kwamba neema ya kuokoa ya Mungu itatufundisha katika kila hatua. Ni lazima kutafuta daima kujua mapenzi ya Bwana, na kutembea kwa kupatana nayo. Daima tutafute kumjua Bwana, Yeye ambaye kwa kumjua kwa usahihi ni uzima wa milele.-Barua 170, 1907.(Mei 6, 1907.)**[GRCsw 47.5]**

Ushahidi ambao tumekuwa nao kwa miaka hamsini iliyopita ya uwepo wa Roho wa Mungu pamoja nasi kama watu, utastahimili majaribu ya hao ambao sasa wanajipanga upande wa adui na wanajiimarisha dhidi ya ujumbe wa Mungu.-Barua 356, 1907. (Okt.24, 1907.)**[GRCsw 48.1]**

Ninawaandikia ninyi mambo haya ndugu zangu, ijapokuwa ninyi nyote mnaweza kutonielewa kikamilifu. Ikiwa sikuamini kuwa jicho la Mungu lipo juu ya Watu Wake, nisingeweza kuwa na ujasiri wa kuandika mambo haya tena na tena. . ....Mungu ana watu ambao Yeye anaowaongoza na kuwafundisha.-Barua 378, 1907.(Nov. 11, 1907.) **[GRCsw 48.2]**

Nimeagizwa kuwaambia kwamba Waadventista wa Sabato ulimwenguni kote, Mungu ametuita sisi watu tuwe hazina ya kipekee Kwake. Yeye ameteua kwamba kanisa Lake duniani litasimama katika umoja kikamilifu, katika Roho na shauri la Bwana wa majeshi hata mwisho wa nyakati. Barua 54, 1908. (Jan.21, 1908.)**[GRCsw 48.3]**

Kwa maana maalum Waadventista wa Sabato wamewekwa ulimwenguni kama walinzi na wabeba nuru. Kwao limekabidhiwa onyo la mwisho kwa ulimwengu unaoangamia. Juu yao inaangaza nuru ya ajabu kutoka kwa Neno la Mungu. Wamepewa kazi adhimu/nzito zaidi - Kutangaza Ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Hakuna kazi nyingine yenye umuhimu mkubwa sana kama hii. Hawapaswi kuruhusu kitu kingine chochote kichote mawazo yao.**[GRCsw 48.5]**

Kweli za adhimu na nzito kabisa zilizowahi kukabidhiwa kwa wanadamu zimetolewa kwao ili tuutangazie ulimwengu. Kutangazwa kwa Kweli hizi kunapaswa kuwa kazi yetu. - *Testimonies* , Vol.9, p.19. (Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mnamo 1909 |Angalia Shuhuda kwenye Website ya RohoYaUnabii.org)**[GRCsw 48.6]**

Hakuna kitu katika ulimwengu huu kinachopendwa sana na Mungu kama kanisa Lake. Kwa wivu wenye kujali, Yeye huwalinda wale wamtafutao. Hakuna kinachomchukiza Mungu kama watumishi wa Shetani wanaojitahidi kuwaibia watu Wake haki zao. Bwana hajawatelekeza watu wake. Shetani anasonda makosa ambayo wamefanya, na kujaribu kuwafanya waamini kwamba kwa kufanya hivyo wamejitenga na Mungu. Malaika waovu wanatafuta kila njia ya kuwakatisha tamaa wale wanaopigania ushindi juu ya dhambi. Wanashikilia mbele yao kutostahili kwao huko nyuma, na kuwakilisha kwamba kesi yao haina matumaini. -Barua 136, 1910. (Nov.26, 1910.)**[GRCsw 48.1]**

## Jina Letu la Kidhehebu

Nilionyeshwa kuhusiana na masalio ya watu wa Mungu kuchukua jina. Makundi mawili yaliwasilishwa mbele yangu. Kundi moja lilikumbatia makundi makuu ya wale wanaojiita Wakristo. Walikuwa wanakanyaga Sheria ya Mungu na kuinama kwa taasisi ya upapa. Walikuwa wakiitunza siku ya kwanza ya juma, yaani Jumapili, kama ndiyo sabato ya Bwana. Kundi jingine, walikuwa wachache tu kwa idadi, walikuwa wakimsujudia Yule Mpaji Mkuu wa Sheria. Wao walikuwa wakishika amri ya nne. Sifa ya kipekee na umaarufu wa imani yao zilikuwa ni utunzaji wa siku ya Saba ya Juma yaani, ambayo ni Sabato ya Jumamosi, na kutazamia kufunuliwa kwa Bwana wetu kutoka mbinguni.........**[GRCsw 50.1]**

Hakuna jina ambalo tunaweza kubeba litakalofaa isipokuwa lile ambalo linaafikiana na kukiri kwetu na linalodhihirisha imani yetu na kututia alama kama watu wa kipekee. Jina la Waadventista wa Sabato ni msimamo unaokemea ulimwengu wa Kiprotestanti. Hapa kuna mstari wa tofauti kati ya wale waabudu wa Mungu na wale wanaomwabudu mnyama na kupokea alama yake. Mgogoro mkuu ni kati ya amri za Mungu na matakwa ya mnyama. Ni kwa sababu watakatifu wanatunza amri zote kumi za Mungu, ambazo joka hufanya vita juu yao. Ikiwa watapunguza kiwango na kuondoa sifa zao za kipekee imani, joka litakuwa na amani; lakini wanachochea hasira yake kwa sababu wao wamethubutu kuinua kiwango na kufunua bendera yao kwa upinzani kwa ulimwengu wa Kiprotestanti, ambao wanaabudu taasisi ya upapa.**[GRCsw 50.2]**

Jina la Waadventista wa Sabato limebeba sifa halisi za maisha yetu ya imani mbele, na litasadikisha akili inayouliza na yenye udadisi. Kama mshale kutoka katika podo la Bwana, utawajeruhi waasi wa sheria ya Mungu; na italeta toba kwa Mungu na imani katika Bwana wetu Yesu Kristo.**[GRCsw 50.3]**

Nilionyeshwa kuwa karibu kila mshabiki aliyetokea, anayetaka kuficha hisia zake ili apate kuwapotosha wengine, hudai kuwa ni wa kanisa la Mungu [church of God]. Jina kama hilo litasisimua mara moja tuhuma/kushukiwa; kwani linatumika kuficha makosa ya kipuuzi kabisa. Hilo jina halipo wazi kwamba linamaanisha nini, na linakuwa kama vile halina mipaka mahsusi kwa masalio ya watu wa Mungu. Jina hilo lingeongoza kwa kudhania kwamba tuna imani ambayo tulitaka kuificha. - *Testimonies* , Vol.1, pp.223, 224.(Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1861.)**[GRCsw 50.4]**

Sisi ni Waadventista wa Sabato. Je, tunaliaibikia kwa jina letu? Tunajibu, Hapana, hapana! Sio Sisi. Ni jina ambalo Bwana ametupa sisi. Linaonyesha Ukweli ambao unapaswa kuwa mtihani wa makanisa.-Barua 110, 1902. (Imeandikwa Julai 7, 1902.)**[GRCsw 51.1]**

Sisi ni Waadventista wa Sabato, na kwa jina hili sisi kamwe hatupaswi kuaibika nalo. Kama watu, ni lazima tuchukue msimamo thabiti kwa Ukweli na haki. Hivyo tutamtukuza Mungu. Tunapaswa kuokolewa kutokana na hatari na mitego na kupotoshwa nayo. Ili hii iweze kuwa, lazima tumtazame Yesu daima, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu.-Barua ya 106, 1903. (Iliyoandikwa Mei 20, 1903.)**[GRCsw 51.2]**

## Makao Makuu ya Waadventista wa Sabato.

Nimeonyeshwa kwamba hakuna maamunzi au hukumu ya mtu mmoja inayopaswa kusalimishwa kwamba ndiyo amri ya maamuzi au hukumu ya mtu mwingine yeyote. Lakini wakati maamuzi na hukumu ya Konferensi kuu (GC), ambayo ndiyo mamlaka kuu ambayo Mungu aliyonayo juu ya dunia, vinapotekelezwa, basi uhuru wa kibinafsi na maamuzi ya faragha hayapaswi kudumishwa bali kusalimishwa.-Shuhuda, Vol. 3, uk. 492. (Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mnamo 1875.) **[GRCsw 52.1]**

Sikuwa na hata mwale mmoja wa nuru kwamba Yeye [Bwana] angenitaka mimi nije katika nchi hii ya [Australia]. Mimi nilikuja huku kwa kujisalimisha kwa sauti wa Konferensi Kuu (GC), ambao nimeichukulia kuwa ni mamlaka [ya Mungu].-Barua ya 124, 1896. (Iliyoandikwa Agosti 9, 1896.)**[GRCsw 52.2]**

Kamwe akili ya mtu mmoja au ya watu wachache haipaswi kuchukuliwa kuwa ndiyo yenye kutosheleza katika hekima na uwezo wa kusimamia na kudhibiti kazi ya Mungu na kusema ni mipango gani itafuatwa. Lakini wakati, mkutano wa Konferensi Kuu wa Waadventista wa Sabato (GC), maamuzi/hukumu ya ndugu waliokusanyika kutoka kwenye sehemu zote za filidi za dunia unatekelezwa, uhuru wa kibinafsi na uamuzi wa kibinafsi haupaswi kudumishwa kwa ukaidi, bali kusalimishwa. Kamwe mtendakazi hapaswi kuchukua kama ni fadhila kudumisha msimamo wake wa uhuru au uliojitenga, kinyume na uamuzi wa mwili wa jumla au Taasisi yote.**[GRCsw 52.3]**

•

Wakati fulani kumekuwa na kikundi kidogo cha watu ambacho kimekabidhiwa usimamizi wa kazi kwa jumla, kwa jina la Konferensi Kuu ya Kanisa ya Waadventista wa Sabato, kikundi hicho kilijaribu kutekeleza mipango isiyo ya busara na kuzuia kazi ya Mungu. Nimesema kwamba wakati huo mimi binafsi, sikuweza tena kuzingatia sauti ya Konferensi Kuu (GC), inayowakilishwa na kikundi cha watu hawa wachache, kama ndio sauti ya Mungu. Lakini hii haimaanishi kwamba maamuzi ya Konferensi Kuu, inayoundwa na mkutano wa watu walioteuliwa ipasavyo, yaani wawakilishi kutoka filidi na konferensi zote duniani hayapaswi kuheshimiwa. Mungu amepanga hilo, kwamba wawakilishi wa kanisa Lake kutoka sehemu zote za dunia, waliokusanyika katika Konferensi Kuu (General Konferensi), watakuwa na mamlaka. Hitilafu ambayo wengine wako hatarini kuchukua ni akili na hukumu ya mtu mmoja, au ya kikundi kidogo cha watu wanaofanya kazi na Halmashauri hiyo kuu, kuwa kiwango/kipimo kamili cha mamlaka na ushawishi ambao Mungu amelipa katika kanisa Lake katika [53] maamuzi na sauti ya Konferensi kuu, iliyokusanyika ili kupanga ustawi na maendeleo ya kazi Yake. [Kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu wa Kanisa la Waadventista wa Siku ya Saba kilikuwa na wajumbe 20-Mkutano huu unajulikana kama General Konferensi- GC of SDA. Kilifanywa tarehe: Mei 20–21, 1863. Mahali: Battle Creek, Michigan. Konferensi zilizowakilishwa- jimbo la ndani (Michigan, New York, Ohio, Minnesota, Wisconsin, na Iowa). Jumla ya Washiriki Waliowakilishwa walikuwa takriban wanachama 3,500, na wote walitoka Marekani]. Battle Creek ilikuwa mahali pa Vikao 26 kati ya 31 vya kwanza vya GC-Konferensi kuu. Vikao vilikuwa kila miaka miwili ila kwa sasa ni kila miaka mitano. Kikao cha kwanza kilichofanyika magharibi mwa Mto wa Mississippi kilikuwa mnamo Novemba 1887 huko Oakland, California. Kikao hiki kimefanyika nje ya Marekani mara tatu: huko Austria mnamo 1975, Uholanzi mnamo 1995 na Canada mnamo 2000. Kikao cha mwisho kilifanyika mnamo 2025 huko St. Louis, Missouri, kilikuwa kikao cha 62 na wajumbe toka filidi mbalimbali duniani walikuwa 2804 na jumla ya washiriki waliowakilishwa walikuwa milioni 23.5 na kutoka katika nchi 212. Nusu a washiriki wa nchi hii 51% wanatoka Afrika.]








**[GRCsw 52.4]**

Wakati uwezo huu, ambao Mungu ameuweka katika kanisa, unapothibitishwa kabisa kwa mtu mmoja, na mtu huyu anavishwa mamlaka ya kuwa muamuzi kwaajili ya akili zote zingine, ndipo utaratibu wa Kweli wa Biblia unabadilishwa. Juhudi za Shetani juu ya akili ya mtu kama huyo zingekuwa za hila nyingi na wakati mwingine atakaribia kumshinda kabisa, kwa maana adui angetumaini kufanya hilo kupitia akili yake, kwani angeweza kuathiri wengine wengi. Wacha tuipe mamlaka ya juu kabisa ya kanisa kufanya maamuzi, kile ambacho tuna mwelekeo wa kumpa mtu mmoja tu au kikundi kidogo cha watu kufanya. - Testimonies , Vol. 9, uk. 260, 261. (Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1909.)**[GRCsw 53.1]**

### Hakuna Shirika Jipya

Bwana ametangaza kwamba historia ya wakati uliopita itarudiwa na kwamba isomwe tena tunapoingia kwenye hatua ya kuhitimsha-kufunga kazi. Kila Ukweli ambao ameutoa kwa ajili ya siku hizi za mwisho utatangazwa kwa ulimwengu. Kila nguzo aliyoisimamisha ni ya kuimarishwa. Hatuwezi sasa kutoka kwenye msingi ambao Mungu ameweka. Hatuwezi sasa kuingia katika shirika lolote jipya; kwa maana hii ingemaanisha uasi kutoka katika Ukweli.-Notebook Leaflets, The Church, No. 1. (Imeandikwa Des. 24, 1905.)**[GRCsw 53.2]**

### Mungu Yuko Katika Usukani Akiongoza

Hakuna haja ya kuwa na shaka, kuwa na hofu kwamba kazi haitaweza kufanikiwa. Mungu Yuko katika kichwa cha kazi, na ataweka kila kitu katika mpangilio. Ikiwa mambo yanahitaji kurekebishwa kichwani mwa kazi, Mungu atafanyia kazi hilo, na kufanya kazi ya kurekebisha kila lisilo sahihi. Hebu tuwe na imani hiyo kwamba Mungu atakwenda kubeba merikebu tukufu inayobeba watu wa Mungu salama bandarini.-Review and Herald , Septemba 20, 1892.**[GRCsw 53.3]**

Mungu mioyoni mwao, watu wanahitaji kwenda ndani zaidi na zaidi, kwa kina kirefu katika kujifunza mambo ya Mungu.- *Review na Herald , Aprili 15, 1915. Imechapishwa tena katika Misingi ya Kikristo Elimu , ukurasa wa 547, 548.*

### Ujumbe mnamo 1913 katika Kongamano Kuu la kanisa la waadventista Kikaoni *

**"Elmshaven," Sanitarium, California,**
**Mei 4, 1913.**

*Kwa wale waliokusanyika katika mkutano wa Mkutano wa Konferensi Kuu, Salamu!* **[GRCsw 54.1]**

*Ndugu zangu Wapendwa:*

"Neema na iwe kwenu na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na kutoka kwa Bwana Yesu Kristo. Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili tuweze kuwafariji

wale walio katika dhiki yoyote, kwa faraja ambayo kwayo sisi wenyewe tunafarijiwa na Mungu."**[GRCsw 54.2]**

"Shukrani kwa Mungu, ambaye hutufanya tushinde kila mara katika Kristo, na kudhihirisha harufu ya ujuzi Wake kupitia sisi ndani yetu kila mahali. Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo kwa Mungu ndani yao wanaookolewa, na katika ya hao wanaopotea."**[GRCsw 54.3]**

"Kwa maana hatujihubiri sisi wenyewe, bali tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo. Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa Kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. "**[GRCsw 54.4]**

"Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti. Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena; tukijua ya kwamba Yeye aliyemfufua Bwana Yesu, atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi. Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe. Kwa hiyo sisi hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya, siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele."**[GRCsw 54.5]**

## Matumaini na Ujasiri

Ni fursa ya watu wetu wanaotuwakilisha katika mahudhurio ya Konferensi Kuu (GC) kuenzi roho ya matumaini na ujasiri. Ndugu zangu, Mwokozi amejidhihirisha kwenu kwa njia nyingi; Yeye Ameujaza moyo wako na mwanga wa jua wa uwepo Wake wakati mmefanya kazi katika nchi za mbali na katika nchi mliyozaliwa, nyumbani kwenu; Yeye Amekutunza wewe na ukapita katika hatari zinazoonekana na zisizoonekana; na sasa, kama mnavyokutana mara moja tena pamoja na ndugu zenu katika baraza la General Konferensi, ni fursa kwenu kuwa na furaha katika Bwana, na kufurahi katika ujuzi wa neema Yake inayotegemeza. Hebu Upendo Wake uteke akili na moyo wako. Jilinde dhidi ya kuwa wachovu, walegevu, wenye masumbufu, na sonona/huzuni. Toeni ushuhuda wa kutia moyo kwenye mkutano wa Halmashauri Kuu (General Konferensi). Geuza macho yako mbali na chochote chenye giza na kukatisha tamaa, na umtazame Yesu, Kiongozi wetu mkuu, ambaye chini ya uangalizi Wake makini, wa Kusudi la Ukweli wa sasa, ambalo sisi tumetoa maisha yetu na yote yetu, vifikie ushindi wenye kurindima kwa utukufu. **[GRCsw 55.1]**

Tabia ambayo wanaume wawakilishi wetu hudumisha wakati wa mkutano itanena ushawishi mkubwa kwa wote katika uwanja wa kazi (fildi zote), na pia juu ya wajumbe wenyewe. Loo, na ionekane Ndugu zangu, ya kuwa Yesu anakaa moyoni, akitegemeza, akitia nguvu na kufariji. Ni upendeleo wako kujazwa, siku hadi siku, kwa kiasi kikubwa na Roho Wake Mtakatifu, na kuwa na maoni yaliyopanuliwa ya umuhimu na upeo wa ujumbe tunaoutangazia Dunia. Bwana Yuko tayari kukufunulia mambo ya ajabu kutoka kwa sheria Yake. Wewe Mngojee tu kwa unyenyekevu wa moyo. Omba sana kwa bidii kupata ufahamu wa nyakati tunazoishi, kwa dhana kamili ya kusudi Lake, na kuongeza ufanisi katika kuokoa roho. **[GRCsw 55.2]**

Mara nyingi nyakati za usiku ninaalikwa kuwasisitizia ndugu zetu katika nafasi za uwajibikaji, kufanya juhudi za dhati kufuatilia kumjua Bwana kwa ukamilifu zaidi. Wakati watendakazi wetu wanatambua kwamba wanapaswa kujua umuhimu wa nyakati tunazoishi, kutaonekana kuwa na kusudi la kuwa upande wa Bwana, nao watakuwa katika Kweli- watenda-kazi pamoja na Mungu. Wanapoweka wakfu moyo na roho kwa utumishi wa Mungu, watapata uzoefu wa kina zaidi kuliko uzoefu wowote ambao

wameshawahi kupata ambao ni muhimu ikiwa wangeshinda juu ya dhambi zote.[GRCsw 55.3]

Itakuwa vyema kwetu kuzingatia yale yatakayokuja hivi karibuni duniani. Huu sio wakati wa kucheza-cheza na mambo madogo-madogo au kujitafutia faida binafsi au kujiweka mbele na bila kujali watu wa Mungu. Ikiwa nyakati tunazoishi zimeshindwa kugusa akili zetu kwa umakini, ni nini basi kinaweza kuifikia mioyo yetu? Je, Maandiko hayahitaji kazi iliyo safi na takatifu zaidi kuliko ile ambayo bado hatujawahi kuona? [GRCsw 55.4]

### Wito wa Kujitoa Wakfu Tena (Reconsecration)

Watu wenye ufahamu ulio wazi wanahitajika sasa. Mungu huita wale walio tayari kuthibitiwa na Roho Mtakatifu kuwaongoza nje katika kazi ya matengenezo kamili. Ninaona mgogoro mbele yetu, na Bwana anawaita watenda kazi Wake kuingia kwenye mstari. Kila nafsi inapaswa sasa kusimama katika nafasi ya wakfu wa kina zaidi, kuwa wakweli kwa Mungu kuliko wakati wa miaka ambayo imepita.[GRCsw 56.1]

Wakati wa mkutano wa Konferensi Kuu (GC) wa 1909 kazi ilipaswa kufanyika katika mioyo ya wale waliohudhuria, jambo ambalo halikufanyika. Saa inapaswa kutolewa kwa uchungazaji wa moyo, ambao ungesababisha k kuvunjwa kwa udongo mgumu wa mioyo ya wale ambao walikuwa kwenye mkutano-[udongo ambao bado haukuwa umekatuliwa -fallow]. Hii ingewapa ufahamu wa kuelewa kazi muhimu sana ya kufanywa nao, katika toba na ungamo. Lakini, ingawa hizi fursa zilitolewa kwa kukiri dhambi, kwa toba ya moyo, na kwa ajili ya matengenezo yaliyoamuliwa, kazi kamili haikufanyika. Wengine walihisi ushawishi wa Roho Mtakatifu, na wakaitikia; lakini wote hawakujisalimisha kwa ushawishi huu. Akili za baadhi ya watu zilikuwa zinakimbia katika maeneo yaliyopigwa marufuku-maeneo yaliyokatazwa kwenda. Kama kungekuwa na nafasi/sehemu ya unyenyekevu wa moyo katika mkutano huu, kungekuwa na udhihirisho wa baraka za ajabu.[GRCsw 56.2]

Kwa muda wa miezi kadhaa baada ya kufungwa kwa mkutano huo, nilibeba mzigo mzito, na kusisitiza usikivu wa akina ndugu katika kuwajibika kwa yale mambo ambayo Bwana alikuwa akiniagiza kuyaweka mbele yao waziwazi. Hatimaye, baadhi ya wale walio katika nafasi za uaminifu/amana kuhusiana na kazi ya jumla, baada ya

maombi mengi na makini, na kujifunza jumbe mbalimbali zilizotolewa, walidiriki kufanya kwa imani kazi waliyoitiwa kuifanya-kazi ambayo hawakuweza kuielewa kikamilifu; na jinsi walivyosonga mbele kwa hofu ya Mungu, walipata baraka tele.**[GRCsw 56.3]**

### Matokeo ya Kutembea katika Nuru

Imeniletea furaha kubwa moyoni mwangu kuona mabadiliko ya ajabu ambayo yamefanywa katika maisha ya baadhi ya watu ambao walichagua kusonga mbele kwa imani katika njia ya Bwana, badala ya kufuata njia ya chaguo lao wenyewe. Endapo hao ndugu katika nafasi za kuwajibika wangeendelea kuyaona mambo katika mtazamo wa udanganyifu, wangeumba hali ya mambo ambayo yangeharibu kazi ya Mungu kwa huzuni; lakini walipoyatii maagizo yaliyotumwa, na kumtafuta Bwana; Mungu aliwaleta katika nuru kamili, na kuwawezesha kutoa utumishi unaokubalika na kuleta matengenezo ya kiroho. **[GRCsw 56.4]**

Bwana anapoweka mkono Wake ili kutayarisha njia mbele za watumishi Wake, ni wajibu wao hawa watumishi kufuata pale Yeye anapoelekeza. Yeye kamwe hawezi kuwatelekeza watendakazi Wake au kuwaacha gizani bila ujuzi wazi au mwelekeo kwa wale wanaofuata miongozo Yake, wakiwa na kusudi kamili la moyo [Bwana hawezi kuwaacha kwenye mataa wale wanaofuata miongozo Yake, wakiwa na kusudi kamili la moyo].**[GRCsw 57.1]**

### Usemi wa Kujiamini au Ujasiri

“ Nafurahi, kwa sababu katika kila neno nina moyo mkuu kwa ajili yenu. 1Wak 7:16.” Na wakati bado nahisi wasiwasi mkubwa juu ya mtazamo huo ambao wengine wanachukua kuelekea hatua muhimu zinazohusiana na maendeleo ya kusudi la kazi ya Mungu duniani, lakini nina imani yenye nguvu katika watendakazi kote shambani mwa Bwana (Fildi), na kuamini kwamba wanapokutana pamoja na kujinyenyekeza mbele za Bwana na kujiweka wakfu wao wenyewe upya kwa utumishi Wake, watawezeshwa kufanya mapenzi Yake. Kuna wengine ambao hata sasa hawaoni mambo kwa nuru ifaayo, lakini hawa wanaweza kujifunza kupatana na watendakazi wenzao katika kazi, na wanaweza kuepuka kufanya makosa mazito, kwa kumtafuta Bwana kwa bidii katika

wakati huu, na kwa kuwasilisha mapenzi yao kikamilifu kwa mapenzi ya Mungu.**[GRCsw 57.2]**

Nimevutiwa na kuguswa moyo sana na matukio ambayo yamepita hivi karibuni mbele yangu wakati wa usiku. Kulionekana kuwa na harakati kubwa katika kazi ya uamsho-kwenda mbele katika sehemu nyingi. Watu wetu walikuwa wanakwenda kwenye mstari, kuitikia wito wa Mungu. Ndugu zangu, Bwana Ndiye Anazungumza nasi. Je! tutaisikiliza sauti Yake? Je, hatutaoa masinzi kwenye utambi katika taa zetu, na kutenda kama watu wanaomngoja Bwana wao aje? Muda ni ule unaohitaji tubebe nuru, na kuchukua hatua za utendaji hai.**[GRCsw 57.3]**

"Basi, nawasihi, ndugu, mwenende kama inavyostahili mapenzi ya Mungu wito mlioitiwa kwa unyenyekevu wote na upole; kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani."- General Conference Bulletin , Mei 19,1913, ukurasa wa 33,34.**[GRCsw 57.4]**

•

**Ujasiri katika Bwana ***

Hivi majuzi katika msimu wa usiku, akili yangu iliguswa na Roho Mtakatifu kwa wazo kwamba ikiwa Bwana atakuja mara tu sisi tutakapo amini Yupo, tunapaswa kuwa watendaji zaidi kuliko vile tulivyokuwa miaka iliyopita katika kupeleka Ukweli, mbele za watu.**[GRCsw 58.1]**

Katika tukio hili akili yangu ilichukuliwa kwenye shughuli za mwaka wa 1843 na 1844, wakati waumini walipokuwa wanatarajia kurudi kwa Kristo (Advent time). Wakati huo kulikuwa na nyumba nyingi za kutembelea, na jitihada zisizochoka zilifanywa katika kuwaonya watu juu ya mambo yanayosemwa katika Neno la Mungu. Tunapaswa kuweka bidii kubwa zaidi sasa, kuliko hata ilivyowekwa na wale waliotangaza ujumbe wa malaika wa kwanza kwa uaminifu sana. Tunakaribia kwa kasi mwisho wa historia ya dunia hii; na kama tunavyotambua kwa hakika kwamba ni Kweli Yesu anakuja hivi karibuni, sisi tutaamshwa kufanya kazi kuliko hapo awali. Tunaagizwa kupiga kengele/kingora kwa watu. Na katika maisha yetu sisi wenyewe, tuonyeshe nguvu ya ile Kweli na Haki. Dunia ipo njiani hivi karibuni kukutana na Mtoa Sheria mkuu juu ya

sheria Yake iliyovunjwa. Ni wale tu wanaogeuka kutoka katika uasi na kwenda kwenye utiifu, ndiyo wanaweza kutumainia msamaha na amani.**[GRCsw 58.2]**

Tunapaswa kuinua bendera ambayo imeandikwa, "Amri ya Mungu, na imani ya Yesu." Utii kwa sheria ya Mungu ndio suala kubwa. Hebu hili lisiondolewe machoni petu-kwenye uoni wetu. Lazima tujitahidi kuwazindua washiriki wa kanisa, na wale wasiokiri Neno la Mungu na imani ya Yesu, ili waone na kutii madai ya sheria ya Mbinguni. Tunapaswa kuikuza hii sheria na kuifanya iheshimiwe/isidharauliwwe.**[GRCsw 58.3]**

Kristo ametuagiza tupande mbegu za Kweli, na kuwahimiza watu wetu umuhimu wa kazi inayofanywa na watu hao ambao wanaishi katikati ya matukio ya siku za mwisho wa historia ya dunia hii. Kadri Maneno ya ile Kweli yanapotangazwa katika njia kuu, kutakuwa na ufunuo wa utendaji kazi wa Roho wa Mungu juu ya mioyo ya wanadamu.**[GRCsw 58.4]**

Jamani, ni kiasi gani cha mema kinaweza kutimizwa ikiwa wote walio na ile Kweli, Neno la uzima, wangefanya kazi kwa ajili ya kuwaangazia wale ambao hawana hilo Neno. Wasamaria walipomjia Kristo kwa wito wa mwanamke Msamaria wa Yohana 4, Kristo alizungumza juu yao kwa wanafunzi Wake kama shamba la nafaka tayari kwa kuvunwa. "Je, hamsemi ninyi, **Bado miezi minne**, **ndipo yaja mavuno**? Tazama, Mimi nawaambieni, Inueni **macho** yenu myatazame **mashamba**, **ya** kuwa yamekwisha kuwa meupe." Kristo alikaa pamoja na Wasamaria kwa siku mbili; kwa maana walikuwa na njaa ya kusikia Ukweli. Na walikuwa na shughuli nyingi kama nini! Kama matokeo ya hizo siku za kazi, "Wengi zaidi wakaamini kwa sababu ya Neno Lake Mwenyewe." Huu ulikuwa ushuhuda wao: "Sisi tumemsikia wenyewe, na tunajua hayo kuwa Huyu Ndiye Kristo, Mwokozi wa ulimwengu."**[GRCsw 58.5]**

Ni nani kati ya wale wanaodai kuwa watu wa Mungu, atakayechukua kazi hii takatifu, na kufanya kazi kwa ajili ya roho zinazoangamia kwa kukosa maarifa? Dunia lazima ionywe. Maeneo mengi yameonyeshwa kwangu kama yale yanayohitaji watendakazi waliojiweka wakfu, waaminifu, na wenye juhudi isiyochoka. Kristo anafungua mioyo na akili za wengi, katika miji yetu mikubwa. Hawa wanahitaji Kweli za Neno la Mungu; na ikiwa tutaingia kwenye ukaribu mtakatifu na Kristo, na tutafute jinsi

ya kuwakaribia watu hawa, hisia kwa wema zitafanywa. Tunahitaji kuamka, na kuingia katika huruma na Kristo na wanadamu wenzetu. Miji mikubwa na midogo, na maeneo ya karibu na ya mbali, yapaswa kufanyiwa kazi, na ifanyiwe kazi kwa akili. Wewe usirudi nyuma kamwe. Bwana atagusa moyo kwa hisia sahihi, ikiwa tutafanya kazi pamoja na Roho Wake.**[GRCsw 59.1]**

Nina maneno ya kuwatia moyo ndugu zangu. Sisi twapaswa kusonga mbele kwa imani na matumaini, tukitarajia mambo makubwa kutoka kwa Mungu. Adui atatafuta kila njia kuzuia juhudi zilizofanywa ili kuendeleza Ukweli, lakini kwa uweza wa Bwana mnaweza kupata mafanikio. Hebu maneno ya kukatisha tamaa yasizungumzwe, bali tu yale maneno ambayo yataelekea kuwaimarisha na kuwategemeza watendakazi wenzako.**[GRCsw 59.2]**

## Neno Kwako Binafsi

Ninatamani kujishughulika mimi mwenyewe katika kazi ya dhati na bidii shambani mwa Bwana, na Kwa hakika nilipaswa kujishughulisha zaidi na kazi ya hadhara/umma, kama nisingeamini kwamba katika umri wangu sio jambo la busara kudharau mambo ya nguvu za kimwili au afya yangu ilivyo. Nina kazi ya kufanya katika kuwasiliana na kanisa na kwa ulimwengu, nuru ambayo imekabidhiwa kwangu wakati kwa wakati katika miaka ambayo ujumbe wa malaika wa tatu umetangazwa. Moyo wangu umejawa na bidii na hamu ya dhati kabisa ya kuweka Ukweli mbele ya wote wanaoweza kufikiwa. Na bado ninatenda sehemu katika kuandaa mada kwa ajili ya kuchapishwa. Lakini lazima nisogee sana kwa uangalifu, nisije nikajiweka mahali ambapo siwezi kuandika kabisa. Sifahamu kwamba ninaweza kuishi kwa muda gani, lakini siteseki sana kiafya kama ambavyo mimi ningetarajia iwe [umri nk].**[GRCsw 59.3]**

Kufuatia Mkutano Konferensi Kuu wa 1909, nilitumia wiki kadhaa kuhudhuria mikutano ya kambi na mikusanyiko mingine mikuu kwa ujumla, na kutembelea taasisi mbalimbali, huko New England, Marekani ya Kati, na Magharibi ya Kati.**[GRCsw 60.1]**

Niliporudi nyumbani kwangu huko California nilianza upya kazi ya kuandaa mada kwa vyombo vya habari, mada za kuchapa kwenye mtambo wa uchapishaji. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita Nimeandika barua chache kwa kulinganisha. Nguvu zangu nilizokuwa nazo zimetolewa zaidi kwa kukamilisha kazi muhimu ya vitabu.**[GRCsw 60.2]**

Mara zingine nimehudhuria mikutano, na nimetembelea taasisi huko California, lakini sehemu kubwa ya wakati tangu huo mkutano wa Konferensi Kuu uliopita, imetumika katika kazi kushugulikia muswada huko nyumbani kwangu, "Elmshaven," karibu na Saint Helena. **[GRCsw 60.3]**

Ninashukuru kwamba Bwana ameniongezea maisha tena ili nifanye kazi kidogo tena kwenye vitabu vyangu. Laiti ningekuwa na nguvu za kufanya yote ninayoona yanafaa kufanyika! Ninaomba kwamba Bwana anipe hekima, ili Ukweli ambao watu wetu wanauhitaji sana, uweze kuwasilishwa kwa uwazi na kukubalika. Ninatiwa moyo kwa kuamini kwamba Mungu ataniwezesha kufanya hivi.**[GRCsw 60.4]**

Nia yangu katika kazi ya jumla bado ni ya kina kama zamani, na mimi natamani sana kwamba kusudi la kazi ya Ukweli wa Leo uliopo, itasonga mbele polepole katika sehemu zote za dunia. Lakini naona sio vyema kujaribu kufanya sana kazi ya hadhara na huku kazi yangu ya vitabu inadai usimamizi wangu. Nina baadhi ya watenda kazi ambao bora sana - wale ambao katika majaliwa na mipango ya Mwenyezi Mungu wameunganishwa nami nilipokuwa Australia, na wengine ambao wameungana nami tangu nirudi Marekani. Namshukuru Bwana kwa wasaidizi hawa. Sisi sote tuna shughuli nyingi, tukifanya kazi kadri tuwezavyo ili kutayarisha mada za kuchapishwa. Nataka nuru ya Ukweli iende kila mahali, ipate kuangaza wale ambao sasa hawajui sababu za imani yetu. Katika baadhi ya siku, macho yangu hunisumbua, na ninapata maumivu mengi ndani Yake. Lakini mimi ninampa sifa Bwana kwamba kwa kuhifadhi macho yangu. Haitakuwa jambo la ajabu kama katika umri wangu umri sitaweza kuona tena kabisa.**[GRCsw 60.5]**

Ninashukuru zaidi kuliko ninavyoweza kueleza kwa Roho wa Bwana anayeniinua, kwa faraja na neema anayoendelea kunipa, na kwamba Yeye ananipa nguvu, upendeleo na fursa ya kuwapa watu Wake ujasiri na msaada. Maadamu Bwana ananipa maisha, mimi nitakuwa mwaminifu na wa kweli Kwake, nikitafuta kufanya mapenzi Yake na kutukuza Jina Lake. Acha Bwana aniongezee imani, ili nimfuate na kumjua, na kufanya mapenzi Yake kikamilifu zaidi. Bwana ni mwema, na wa kusifiwa sana.**[GRCsw 60.6]**

## Ushawishi wa Watendakazi Wazee.

Ninatamani sana kwamba askari wa zamani wa msalaba, wale waliokua na mvi au nywele nyeupe katika utumishi wa Bwana, wataendelea kubeba ushuhuda wa haki kwa pointi/kipengele chake, ili wale walio wadogo katika imani wapate kuelewa kwamba huo ujumbe ambao Bwana alitupatia zamani ni wa muhimu sana katika hatua hii ya historia ya dunia. Uzoefu wetu wa zamani haujapotea HATA nukta moja ya nguvu zake.**[GRCsw 61.1]**

Hebu wote wawe waangalifu ili wasiwakatishe tamaa waanzilishi/pioniya/pioneers, au kuwasababisha kuhisi kwamba kuna kidogo wanaweza kufanya. Ushawishi wao unaweza kuwa wa bidii kubwa bado katika kazi ya Bwana. Ushuhuda wa wachungaji na wahudumu wazee utakuwa msaada na baraka kwa kanisa. Mungu anawaangalia na kuwalinda Watendakazi Wake, washika viwango Wake waliojaribiwa na waaminifu, usiku na mchana, mpaka utakapofika wakati wa wao kuweka silaha zao chini [kifo]. Hebu watendakazi hawa wawe na uhakika kwamba wako chini ya ulinzi wa Yeye asiyesinzia wala kulala; kwamba wanaangaliwa na walinzi wasiochoka. Kujua hii, na kutambua kwamba wanakaa ndani ya Kristo, wanaweza kupumzika kwa matumaini katika mipango na majaliwa ya Mungu.**[GRCsw 61.2]**

## "Hata Mwisho"

Ninaomba kwa dhati na bidii kwamba kazi tunayofanya wakati huu itagusa yenyewe moyo, akili na roho kwa kina. Matatizo yataongezeka; lakini sisi, kama watu wanaomwamini Mungu, tufarijiane sisi kwa sisi. Tusipunguze kiwango, bali tukiinue juu, tukimtazama Yeye ambaye Ndiye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu. Wakati wa msimu wa usiku ninaoposhindwa kulala, nainua moyo wangu kwa maombi kwa Mungu, Naye hunitia nguvu yangu na kunipa uhakikisho kwamba Yeye Yuko pamoja na watumishi Wake katika shamba la nyumbani hapa Marekani na katika nchi za mbali. Ninatiwa moyo na kubarikiwa, ninapotambua kwamba Mungu wa Israeli bado anawaongoza watu Wake, na kwamba ataendelea kuwa pamoja nao, hata mwisho-hata ukamilifu wa dahari.**[GRCsw 61.3]**

**Kusonga Mbele Katika Kuongeza Ufanisi**

Nimeagizwa kuwaambia ndugu zetu wanaohudumu, Acheni jumbe zitokazo midomoni mwenu zichajiwe kwa nguvu za Roho wa Mungu-ziwe na umeme wa Roho Mtakatifu. Ikiwa kuna wakati tulihitaji uongozi maalumu wa Roho Mtakatifu, basi ni sasa. Tunahitaji kujiweka wakfu kikamilifu sasa. Wakati umefika ambao tunapaswa kutoa kwa ulimwengu onyesho la nguvu za Mungu katika maisha yetu na katika huduma zetu. **[GRCsw 62.1]**

Bwana anatamani kuona kazi ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu ikiendelea mbele na kuongeza ufanisi. Kwa vile Yeye amefanya kazi katika nyakati zote katika kuwapa watu wake ushindi, vivyo hivyo katika zama hii Yeye Anatamani kufikisha kazi katika ushindi timilifu wa makusudi Yake kwa ajili ya Kanisa Lake. Yeye anaagiza watakatifu Wake wanaoamini, wasonge mbele kwa umoja, wakitoka nguvu hadi nguvu kubwa zaidi, kutoka imani hadi uhakikisho ulioongezeka na imani katika Ukweli na haki ya kusudi Lake.**[GRCsw 62.2]**

Tunapaswa kusimama imara kama mwamba kwa kanuni za Neno la Mungu, tukikumbuka kwamba Mungu Yuko pamoja nasi ili kutupa nguvu za kukutana na kila uzoefu mpya. Hebu tudumishe kanuni za haki daima, katika maisha yetu, ili tuweze kusonga mbele kutoka nguvu hadi nguvu kwa Jina la Bwana. Tunapaswa kuishikilia imani kwa utakatifu sana, imani ambayo imethibitishwa na maelekezo na idhini ya Roho wa Mungu tangu uzoefu wa maisha yetu ya awali hadi wakati huu. Tunapaswa kuthamini sana kazi ambayo Bwana amekuwa akiipeleka mbele kupitia kwa watu wanaozishika amri Zake, na ambayo, kwa uwezo wa neema Yake, itakua na nguvu zaidi na zaidi na ufanisi kadiri kadri muda unavyosonga mbele. Adui anatafuta kutia ukungu utambuzi wa watu wa Mungu, na kudhoofisha ufanisi wao, lakini ikiwa watafanya kazi kama Roho wa Mungu atakavyoelekeza, atafungua milango ya fursa na upendeleo mbele yao kwa kazi na watapajenga mahali palipokuwa ukiwa-Isaya 58:12.. Uzoefu wao utakuwa wa ukuaji wa mara kwa mara, hadi siku Bwana atakaposhuka kutoka mbinguni na nguvu na utukufu mwingi kuweka Muhuri Wake wa ushindi wa mwisho juu ya waaminifu Wake.**[GRCsw 62.3]**

**Ahadi ya Ushindi wa Mwisho**

Kazi iliyo mbele yetu ni moja ambayo itanyumbulisha kila nguvu ya mwanadamu. Itaiita zoezi la imani yenye nguvu, thabiti na kukesha kwa uendelevu. Wakati mwingine ugumu huo tutakaouona utakuwa wa kukatisha tamaa zaidi. Ukuu wa kazi utatushtua sana. Hata hivyo, kwa msaada wa Mungu, hatimaye watumishi Wake watapata ushindi. “Kwa hiyo,” ndugu zangu, “naomba msizimie” kwa sababu ya uzoefu wenye kujaribu ulio mbele yenu. Yesu atafanya kuwa na wewe;Bwana Atakutangulia mbele yako kwa Roho Wake Mtakatifu, akitayarisha njia; Naye atakuwa ni Msaidizi wenu katika kila dharura.**[GRCsw 62.4]**

“Kwa sababu hiyo nampigia magoti Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye jamaa yote ya mbinguni na duniani inaitwa, ili awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, mpate uimarishwe kwa uwezo na Roho Wake katika utu wa ndani; hiyo Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani; kwamba ninyi, mkiwa na mizizi na wenye msingi katika upendo, wapate kufahamu pamoja na watakatifu wote ni nini upana, na urefu, na kina, na kimo; na kujua upendo wa Kristo, upitao maarifa yote, mjazwe na yote utimilifu wa Mungu. **[GRCsw 63.1]**

“Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; atukuzwe katika kanisa katika Kristo Yesu hata vizazi vyote, ulimwengu usio na mwisho. Amina.”- General Conference Bulletin , Mei 1913, ukurasa wa 164, 165. **[GRCsw 63.2]**

**Sitarajii kuishi muda mrefu. Kazi yangu inakaribia kukamilika .... Sidhani kama nitakuwa na Ushuhuda zaidi kwa watu wetu. Watu wetu wenye akili timamu wanajua yaliyo mema kwa ajili ya kuinua na kujenga kazi. Lakini wakiwa na upendo wa Mungu mioyoni mwao, wanahitaji kuingia ndani zaidi na zaidi katika kujifunza mambo ya Mungu.-Review and Herald, Aprili 15, 1915. Imechapishwa tena katika Fundamentals of Christian Education, kurasa 547, 548.** 1915[1]**[GRCsw 63.3]**

[1] From Ellen G. White’s last message to the church, dictated from her sickbed during her last illness

## MUHTASARI WA KITABU NGAZI YA KUFIKIA MBINGUNI

(STEPS TO THE MESIAH)

**Ninawezaje Kuja Kwa Kristo?**

*<u>Sehemu ya Kwanza</u>*

Asili na ufunuo wa Mungu kwa wanadamu wote kwa pamoja hushuhudia upendo wa Mungu. Ni uvunjaji (uasi) wa Sheria ya Mungu - Sheria ya upendo – ndio kwamba umeleta misiba na kifo. Lakini hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu unafunuliwa. “Mungu ni upendo” imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya kila unyasi unaochipuka.

Yesu alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kudhihirisha upendo wa Mungu usio na kikomo. Upendo, rehema, na huruma zilikuwa zimefunuliwa katika kila tendo la maisha Yake; Moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo na upendo mwanana kwa watoto wa wanadamu. Alichukua asili ya mwanadamu, ili Aweze kufikia matakwa ya mwanadamu. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia Yeye. Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama inavyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu.

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa ambapo Yesu aliishi, aliteseka, na kufa. Alifanyika “Mtu wa Huzuni,” ili sisi tupate kufanywa washirika wa furaha ya milele. Lakini dhabihu hii kuu haikutolewa ili kuunda katika Moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kumfanya awe tayari kutuokoa. Hapana, hapana! “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee.” Yohana 3:16. Baba anatupenda, si kwa

sababu ya upatanisho mkuu, bali Alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda. Hakuna mwingine ila Mwana wa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu.

Hii inaweka thamani iliyoje kwa mwanadamu! Kupitia uasi, wana wa binadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Upendo usio na kifani wa Mungu kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Mawazo yana nguvu ya kutiisha juu ya nafsi na huleta akili katika utumwa wa mapenzi ya Mungu.

Mwanadamu hapo awali alijaliwa uwezo wa kiungwana na akili iliyo na usawa mzuri. Alikuwa mkamilifu katika nafsi yake, na kupatana na Mungu. Mawazo yake yalikuwa safi, malengo yake yalikuwa matakatifu. Lakini kwa kutokutii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kupitia dhambi ambayo haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu.

Haiwezekani sisi, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kujibadilisha. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya wanadamu kubadilishwa kutoka katika dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kuivuta kwa Mungu, kwa utakatifu. Kwa wote, kuna jibu moja tu, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Hebu na tuikubali njia hii iliyotolewa kwa ajili yetu ili tuweze kugeuzwa na kufanana Naye, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wanaohudumia, kwa maelewano na ushirika na Baba na Mwana.

Mtu atakuwaje mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi atafanywaje kuwa mwadilifu? Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kuletwa katika mapatano na Mungu, kwa utakatifu; lakini tunawezaje kumwendea Kristo?

Toba ni pamoja na huzuni kwa ajili ya dhambi na kuiacha. Hatutaacha dhambi mpaka tuone ubaya wake; mpaka tuiache kwa moyo, hakutakuwa na mabadiliko ya kweli katika maisha. Lakini moyo unapokubali kuongozwa na Roho wa Mungu, dhamiri

itahuishwa, na mwenye dhambi atatambua jambo fulani la kina, na utakatifu wa Sheria takatifu ya Mungu, na msingi Wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kisha usadikisho hushika akili na moyo.

Ombi la Daudi, baada ya anguko lake, linaonyesha asili ya huzuni ya kweli kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na jitihada za kutuliza hatia yake; hakuwa na hamu ya kutoroka hukumu inayomtishia ila aliongozwa katika maombi yake. Daudi aliona ukubwa wa kosa lake; aliona unajisi wa nafsi yake; yeye aliichukia dhambi yake. Haikuwa kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, lakini kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu, kurejeshwa katika maelewano na ushirika na Mungu.Toba kama hii haiwezi kufikiwa na uwezo wetu wenyewe na kuikamilisha; bali hupatikana tu kutoka Kristo.

Kristo Yuko tayari kutuweka huru kutokana na dhambi, lakini halazimishi nia hiyo. Tukikataa anaweza kufanya nini zaidi? Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Unapoona ukubwa wa dhambi, kama unavyojiona jinsi ulivyo, usikate tamaa kwa kupoteza matumaini. Ni wenye dhambi ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Shetani anapokuja kukuambia kuwa wewe ni mwenye dhambi mkuu, mtazame Mkombozi wako na uongee juu ya wema Wake. Ikiri dhambi yako, lakini mwambie adui kwamba “Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi” ili mimi nipate kuokolewa (1 Timotheo 1:15).

“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Mithali 28:13. Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na busara. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, Ambaye peke Yake Ndiye anayeweza kuwasamehe, na msameheane makosa yenu ninyi kwa ninyi. Wale ambao hawajanyenyekesha nafsi zao mbele za Mungu, kwa kukiri hatia yao, bado hawajatimiza hatua ya kwanza ya kukubalika sharti tuwe tayari kunyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Sheria ya Neno la Kweli. Kukiri ambako kumiminiwa kwa roho ya ndani hupata njia yake kwa Mungu wa huruma Asiye na kikomo. Kuungama kwa kweli siku zote huwa na tabia maalum, na hukubali dhambi fulani. Maungamo yote

yanapaswa kuwa ya uhakika na ya kulenga jambo mahususi. Imeandikwa, “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1John 1:9.

Ahadi ya Mungu ni, “Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote.” Yeremia 29:13. Moyo wote sharti utolewe, au mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tunapaswa kurejeshwa kwa mfano Wake.

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujitolea kwa nafsi, kusalimisha Mapenzi yetu yote kwa Mungu, inahitaji mapambano; lakini nafsi inapaswa kunyenyekea kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika utakatifu. Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima kuacha yote ambayo yangetutenganisha Naye. Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii Sheria Yake, ili kuunda tabia sahihi na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama vile ambavyo Mungu anataka kutoka kwao ili kuipata mbingu. Dini kama hiyo haina thamani.

Kristo akikaa ndani ya moyo, roho itajawa na upendo Wake, na furaha ya kuungana Naye, kwamba roho itashikamana Naye; na katika kumfikiria Yeye, nafsi itasahauliwa. Upendo kwa Mwenyezi Mungu utakuwa chemchemi ya Kila wazo na tendo. Mambo hayo hayalengi viwango vya chini kabisa, bali hulenga kupatana kikamilifu na Mapenzi ya Mkombozi wao.

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kutoa yote kwa Kristo? Jiulize swali, “Ni nini Kristo ametoa kwa ajili yangu?” Mwana wa Mungu alitoa maisha yake yote, kwa upendo na akapitia mateso kwa ajili ya ukombozi wetu. Je, sisi, tusiostahili, ambao ni walengwa wa upendo mkuu hivyo, tutazuia mioyo yetu Kwake? Je, Tunatoa nini zaidi wakati tunatoa yote? Ni Moyo uliochafuliwa na dhambi tu, ndiyo tunatoa na hakuna lingine la thamani tunalolitoa kwa Mungu, tunautoa moyo huu, ili Yesu ausafishe, ausafishe kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani.

Na ajabu ni kwamba, bado watu wanafikiri ni vigumu kuacha yote! (na kumbe kile tunachokiacha ni moyo mchafu tu). Mungu hataki tutoe chochote ambacho ni cha manufaa kwetu ili tubaki salama. Katika yote anayofanya, Yeye ana maslahi ya watoto Wake katika mtazamo Wake.

Wengi wanauliza, “Nifanyeje kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu?” Unatamani kujitoa Kwake, lakini u dhaifu katika uwezo wa kimaadili,una utumwa wa mashaka, na unatawaliwa na tabia za maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi ulio nao kuhusu ahadi zako zilizovunjwa na ahadi ulizopoteza hudhoofisha kujiamini kwako katika unyofu wako mwenyewe, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini huna haja kukata tamaa.

Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya uthubutu (uchaguzi). Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mtu, nguvu ya uamuzi, au ya kuchagua. Kila kitu kinategemea hatua sahihi ya uthubutu. Nguvu ya uhuru wa kuchagua ambao Mungu amewapa wanadamu; ni juu ya hii unapaswa kuifanyia mazoezi. Huwezi kubadilisha moyo wako, na huwezi kujibadili wewe mwenyewe, kwahiyo mpe Mungu mapenzi (matamanio) ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpa mapenzi yako; Naye Atafanya kazi ndani yako kutaka na kutenda sawasawa na mapenzi Yakemema. Kwa hivyo asili yako yote itaweza kuletwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; mapenzi yako yataelekezwa Kwake, mawazo yako yatakuwa sawa na Yeye.

Matamanio ya kuwa na wema na utakatifu ni sawa kadiri yanavyokwenda; lakini ukiishia hapa, hautafaidika kwa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kuweka mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo.

Kupitia mazoezi sahihi ya uthubutu, mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yako. Utakuwa na nguvu kutoka juu ili kukuweka imara, na hivyo kupitia

kuendelea kujitoa daima kwa Mungu utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani.

Kwa vile dhamiri yako imehuishwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu juu ya uovu/ubaya wa dhambi, na nguvu zake, hatia yake, na majanga yake; na sasa unaitazama dhambi kwa chuki. Ni amani ndiyo unayohitaji. Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeamua kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba akuoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya.

Basi amini kwamba Yeye Anafanya hivi kwa sababu ameahidi hivyo. Zawadi ambayo Mungu anatuahidi, ni sharti tuamini kwamba tunaipokea, na kwamba ni zetu. Wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako zilizopita; huwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe amini tu ahadi hiyo. Tubu dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Utapenda kumtumikia. Vile vile unapofanya hivi, hakika Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ikiwa unaamini katika ahadi hiyo, Mungu anaitoa kwako kweli (kiuhalisia). Usisubiri mpaka uhisi kuwa umefanywa mzima, lakini sema, “Naamini; ni hivyo, si kwa sababu ninaihisi, bali kwa sababu Mungu “Aliahidi.”

## *Sehemu ya Pili*

### **Ninawezaje Kubaki Mkweli kwa Kristo?**

Yesu anasema, “Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24. Kuna sharti kwa ahadi hii - kwamba tuombe sawasawa na Mapenzi ya Mungu. Lakini ni Mapenzi ya Mungu kutusafisha na dhambi zetu, kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Hivyo tunaweza

kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumepokea ahadi hizo.

Tangu sasa ninyi si mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa bei kubwa. Kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe.

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usirudi nyuma tena, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, “Mimi ni wa Kristo, nimejitoa Kwake,” na umwombe Akupe Roho Wake ili Akutunze kwa neema Yake. Kama ilivyo, unapojitoa kwa Mungu, na kumwamini, basi, unakuwa mtoto Wake, ndivyo na wewe wanapaswa kuishi ndani Yake.

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu anasamehe kila nafsi,yaani mtu mmoja mmoja. Hawamtilii maanani Mungu katika Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu hazikukusudiwa kwa ajili yako.Ahadi za Mungu zipo kwa ajili ya kila nafsi inayotubu. Inueni macho juu, ninyi wenye mashaka na kutetemeka; kwa maana Yesu Yu hai ili atuombee. Mshukuruni Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwanawe mpendwa.

“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mpya.” 2 Wakorintho 5:17. Huenda mtu asiweze kutaja wakati au mahali hasa, au kufuatilia mlolongo wote kwamba mambo yalikuwaje katika huu mchakato wa uongofu; lakini hii haithibitishi kuwa wewe haujaongoka.

Mabadiliko yataonekana katika mwenendo, tabia, na utendaji wako. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya vile ambavyo ulivyo sasa na ulivyokuwa. Nani ana moyo wako? Mawazo yetu yanamilikiwa na nani? Je, tunapenda kuzungumza juu ya nini au nani? Ni nani aliye na upendo wetu makini na nguvu zetu bora zaidi? Ikiwa sisi ni wa

Kristo, mawazo yetu yapo pamoja Naye. Hakuna uthibitisho wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo.

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana kwa wafuasi Wake. Ilikuwa furaha Yake Masihi kufanya Mapenzi ya Mungu. Kuna makosa mawili ambayo watoto wa Mungu hasa wanatakiwa kujilinda nayo: La kwanza ni lile la kujivunua kazi zao wenyewe, kujiamini kuwa wao wanaweza kufanya kitu fulani, ili kuweza kujileta wenyewe katika mapatano na Mungu. Yote ambayo mwanadamu anaweza kufanya bila Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee, kwa njia ya imani, ndiyo ambayo inaweza kutufanya watakatifu.

Kosa la pili lililo kinyume na la hatari ni kwamba watu huamini kwamba imani katika Kristo huwaachilia wanadamu kutoka katika kuishika Sheria ya Mungu; kwamba kwa kuwa na imani pekee tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, matendo yetu hayana la kufanya katika suala la ukombozi wetu.

Utii ni tunda la imani. Haki inafafanuliwa kwa kiwango cha Sheria takatifu ya Mungu, kama inavyoonyeshwa katika zile Amri kumi (Kutoka 20:3-20). Kile kinachoitwa imani katika Kristo ambacho kinadai kuachilia watu kutoka katika wajibu wa utii kwa Mungu, si imani, lakini ni kiburi na uelewa ulio na makosa. Sharti la uzima wa milele lilivyo sasa ndivyo lilivyokuwa siku zote - kama ilivyokuwa katika edeni (au paradiso) kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, sharti hilo ni Utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo uadilifu mkamilifu.

Ikiwa uzima wa milele ungetolewa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi furaha ya sayari zote na mbingu imo hatarini. Njia ingelifunguliwa wazi kwa ajili ya dhambi, pamoja na msururu wake wote wa misiba na taabu, hata kama watu hawafi.

Kristo anabadilisha moyo. Anakaa moyoni mwetu kwa imani. Tunapaswa kudumisha uhusiano huu na Kristo kwa imani na kujitoa daima kwa mapenzi yetu Kwake; na mradi

unafanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yake kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake mema.

Kadiri unavyomkaribia Masihi, ndivyo utakavyoona ulivyo na makosa zaidi machoni pako; maana maono yako yatakuwa wazi zaidi. Huu ni ushahidi kwamba udanganyifu wa Shetani unapoteza nguvu zake. Hakuna upendo wa kina kwa Yesu unaoweza kukaa katika moyo ambao hautambui dhambi yake wenyewe. Nafsi inayogeuzwa kwa neema ya Kristo itapendezwa na tabia Yake Mungu. Mtazamo wa dhambi zetu unasukuma na Yeye anayeweza kusamehe; na wakati nafsi, inatambua unyonge wake, na kumfikia Kristo, Yeye atajidhihirisha kwa uwezo Wake. Kadri hisia za kumhitaji zinavyotusukuma Kwake na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyotukuka zaidi juu ya tabia Yake, na kwa ukamilifu zaidi tutaiakisi sura Yake.

Badiliko la mioyo ambalo kwalo tunafanyika kuwa wana wa Mungu linapatikana katika Biblia kama kuzaliwa. Tena linalinganishwa na kuota kwa mbegu nzuri iliyopandwa na mkulima. Ni Mungu Ndiye anayeleta chipukizi la majani kutokea na kisha ua, na mwishowe matunda. Ni kwa uwezo Wake mbegu hukua. Kama vile Ua linavyoligeukia jua, ili miale yake angavu isaidie katika ukamilifu mzuri na ulinganifu wake; ndivyo sisi tutakiwavyo kuligeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni iangaze juu yetu, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika kufanana na Kristo.

Je, unauliza, “Ninawezaje kukaa ndani ya Kristo?” Kama jinsi ulivyompokea Kristo hapo kwanza. "Basi kama mlimpokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye.” Wakolosai 2:6. Kwa imani wewe ukawa Wake Kristo; na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote, moyo wako, mapenzi yako, huduma yako, hebu jitoe Kwake ili kutii matakwa Yake yote; nawe sharti uvibebe vyote, yaani umchukue Kristo (Ambaye Ndiye vyote), Ambaye ni utimilifu wa baraka zote, Akae moyoni mwako, Awe nguvu yako, Awe haki yako, na Msaidizi wako wa milele wa kukupa uwezo wa kutii.

Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, Nitwae, Ee Bwana, niweWako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote na itimizwe ndani yako." Niepushe kuyafanya yale ambayo sipaswi kuyafanya, na kuyafanya yale ambayo napaswa kufanya.  Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au iache kutokana na majaliwa Yake yatakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuwa unayatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Maisha ndani ya Kristo ni maisha ya utulivu. Kunaweza kuwa hakuna furaha yenye mihemko ya hisia, lakini kunapaswa kuwa na uvumilivu wa kuendelea kudumu katika Imani yenye matumaini. Wakati akili inapokaa juu ya ubinafsi, inageuzwa mbali na Kristo, Aliye chanzo cha nguvu na uhai. Kwa hivyo, ni juhudi ya mara kwa mara ya Shetani kutoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo.

Kristo alipotwaa asili ya mwanadamu juu Yake, Aliufungamanisha ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kamwe kuvunjwa na mamlaka yoyote, isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuweka vivutio vya kutushawishi kuvunja uhusiano huu yaani kuchagua kujitenga na Kristo. Lakini wacha tuendelee kuinua macho yetu kumtazama Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Masihi, tuko salama. Hakuna kinachoweza kutung'oa kutoka mkononi Mwake. Yote ambayo Kristo alikuwa kwa wanafunzi, anatamani yawe kwa watoto Wake leo.

Yesu alituombea, na aliomba kwamba tuwe na umoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba.  Huu ni muungano wa thamani kiasi gani! Hivyo, tukimpenda na kukaa ndani Yake, "tutakua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye Aliye kichwa, Kristo." Waefeso 4:15.

Mungu Ndiye chanzo cha uhai na nuru na furaha kwa ulimwengu. Popote uzima wa Mungu unapokuwepo ndani ya mioyo ya watu, uzima huo utatiririka kwa wengine kwa upendo na baraka.

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinuliwa na ukombozi wa wanadamu walioanguka. Kwa hili hakuyahesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake Yeye Mwenyewe, bali aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Wakati upendo wa Kristo umo ndani ya moyo, ni kama manukato au harufu nzuri isiyoweza kufichwa. Upendo kwa Yesu utadhihirika katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinuliwa kwa ubinadamu. Upendo kwa Kristo huleta mwitikio wa upendo, rehema, na huruma yenye mguso kwa viumbe vyote ambavyo Baba yetu wa mbinguni Anavitunza. Wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine aliowafia wapate kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kufanya duniani, ili dunia iwe mahali bora zaidi katika kukaa kwao humo. Roho hii ndiyo chanzo cha uhakika cha nafsi iliyoongoka kweli kweli. Mara tu mtu anapokuja kwa Kristo ndipo unazaliwa ndani ya moyo wake hamu ya kufanya ijulikane kwa wengine ni urafiki wa thamani gani ameupata kwa Yesu. Ikiwa tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na kitu cha kusema. Tutajaribu kuwasilisha kwa wengine vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao. Kutakuwa na nguvu yenye matamanio makubwa katika kufuata njia ambayo Yesu aliipita.

Na jitihada za kuwabariki wengine zitaleta mwitikio wa baraka juu yetu wenyewe. Wale ambao wanakuwa washiriki katika kazi ya upendo, huletwa karibu zaidi na Muumba wao. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na kuwa na tabia ya kupendeza kama Kristo kwa mhusika, na kisha huleta amani na furaha kwa mhusika(mtoaji). Nguvu huja kwa kujizoesha. Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuacha mazingira ya nyumba zetu, ikiwa hapo ni pale ambapo wajibu wetu uko, ili kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Kwa roho ya upendo tunaweza kufanya kazi kwa unyenyekevu katika maisha "kwa Bwana." Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu umo moyoni, utadhihirika katika maisha yetu. Haupaswi kungojea hafla nzuri au kutarajia uwezo wa ajabu kabla ya kwenda kufanya kazi kwa

ajili ya Mungu. Wanafunzi wanyenyekevu na maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine wakati wote.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika pamoja Naye. Ikiwa tutasikiliza tu, Asili huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Kazi zilizoumbwa na Mungu zitatufundisha masomo ya thamani ya utii na uaminifu.

Hakuna machozi yanayotolewa ambayo Mungu hayatambui. Hakuna mwenendo asiyoutia alama. Kama tungeweza kumwamini kikamilifu, mahangaiko yote yasiyofaa yangetupiliwa mbali. Maisha yetu yasingejazwa na kukata tamaa kama ilivyo sasa; kwa maana kila kitu, kiwe kikubwa ama kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu.

Mungu huzungumza nasi kupitia kazi Zake na majaliwa na kupitia ushawishi wa Roho Wake juu ya moyo yetu. Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tunayomistari iliyo wazi zaidi ya ufunuo wa tabia Yake, kushughulika Kwake na wanadamu, na kazi kuu ya ukombozi. Jaza moyo wote kwa Neno la Mungu. Neno ni maji yaliyo hai, yakizima kiu yako iwakayo. Neno ni mkate wa uzima kutoka mbinguni.

Siri ya ukombozi ni jambo ambalo malaika wanatamani kuliangalia na kulijua ila ni fumbo na siri; ukombozi wa mwanadamu itakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika enzi zote zisizo na kikomo za milele. Kama ni hivyo, Je, haifai tufikirie sasa kwa makini na kujifunza leo hii? Tunapotafakari juu ya Mwokozi, kutakuwa na njaa na kiu ya nafsi ya kuwa kama Yeye Ambaye tunamwabudu.

Biblia iliandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kweli kuu zinazohitajika kwa wokovu zinafanywa wazi kama mchana. Hakuna kitu kinachohesabiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko Matakatifu. Lakini kuna faida kidogo inayopatikana kwa kusoma Biblia haraka-haraka. Fungu moja likisomwa kwa makini hadi tukagundua umuhimu kwa  akili zetu na uhusiano wake, na mpango wa wokovu ukawa dhahiri, huu ndio usomaji wa thamani zaidi kuliko usomaji wa sura nyingi bila malengo dhahiri na hakuna maagizo chanya yaliyopatikana.

Weka Biblia yako pamoja nawe. Upatapo nafasi, isome; yaweke maandishi kwenye kumbukumbu yako. Hatuwezi kupata hekima bila uangalifu wa dhati na kujifunza kwa sala.

Kamwe Biblia haipaswi kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa Zake, tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anawathaminiwanadamu? Yeye alimtoa Mwanawe ili afe kwa ajili yao na anamtuma Roho Wake Mtakatifu kuwa mwalimu wa mwanadamu, Naye ni kiongozi wa kudumu!

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu anazungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake. Ili kuwasiliana na Mungu, sharti tuwe na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi, maisha ya kila siku. Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni sharti tumjulishe Mungu mambo yalivyo kwetu, bali ni ili Atuwezeshe kumpokea Yeye mioyoni mwetu. Maombi hayamshushi Mungu kwetu, lakini maombi hutupeleka juu Kwake.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupa utimilifu wa baraka Zake. Inashangaza kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! Mungu Yuko tayari kutubariki na Anawiwa kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi. Malaika wa mbinguni wanashangaa wanapofikiria juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, nao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana, wakati Moyo wa Mungu wenye upendo usio na kikomo una matamanio nao, Naye Yupo tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria.

Giza la mwovu linawafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii fursa

ya maombi. Walakini maombi ndio ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala ya mbinguni, ambapo rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote zinatunzwa.

Kuna masharti fulani ambayo kwayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu: Moja ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Tukiwaza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote tuijuayo; Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu na aliyeungama hukubaliwa daima. Wakati wote makosa yanayojulikana yanaposahihishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia kaw bidii ahadi Zake; kwani wakati wa kujibiwa utakuja hakika, na tutapokea baraka tunazozihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa namna tutakavyo na kila kitu tunachokitamani ni dhana za kufikirika.

Tunapokuja kwa Mungu katika maombi, tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Kuendelea kudumu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea majibu yetu. Sharti tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu.

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ndiyo maisha ya kiroho. Sala ya familia au ya hadhara pekee yake haitoshi. Maombi ya siri yanasikika kwa Mungu Ajibuye maombi.

Hakuna wakati au mahali pasipofaa kutoa ombi kwa Mungu. Katika umati wa watu mtaani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kumsihi Mungu Atupe mwongozo wa Kiungu.

Hebu roho na ivutwe na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya anga la mbinguni. Sisi tunaweza kuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa

mawazo yetu yatamgeukia Yeye kwa ile kawaida ya ua linavyoligeukia jua. Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu.

Huwezi kumlemea; huwezi kumchosha. Yeye hachoshwi na matakwa ya watoto Wake.

Tunapata hasara tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo sisi kwa sisi katika utumishi kwa Mungu. Ikiwa Wakristo watashirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Kweli za thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa na wangeburudishana wao kwa wao.

Ni sharti tukusanyike pamoja kwa ajili ya msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa vinapaswa kuwa mada ya kutafakari, mada ya mazungumzo, na hisia zetu za furaha zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayoipokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini kila kitu kilicho katika mikono ile iliyotundikwa msalabani kwa ajili yetu.

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mbawa za sifa kwa Mungu. Tunapoonyesha shukrani zetu, ndivyo tukaribiavyo kuabudu na majeshi ya mbinguni. Wengi nyakati fulani wanatatizwa na mapendekezo ya kutilia shaka kuhusu Mungu. Mungu kamwe hatuambii tuamini bila kutoa uthibitisho wa kutosha wa kujenga imani yetu. Tunaweza kuficha uhalisia au ukweli Kwa namna tuwezavyo, ila sababu halisi ya shaka na kutokuamini, katika hali nyingi, ni kupenda dhambi. Ni sharti tuwe na nia ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo kuitii.

Kabla ya kuingia kwa dhambi, Adamu alifurahia ushirika wa wazi na Muumba wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga yeye mwenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutenda dhambi, jamii ya kibinadamu imekatiliwa mbali na upendeleo huu mkuu. Kwa mpango wa ukombozi, hata hivyo, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza bado kuwa na uhusiano na Mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa

Roho Wake, na nuru ya Bwana imekuwa ikipandikizwa ulimwenguni kwa mafunuo, kupitia watumishi Wake wateule. "Watu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Petro 1:21.

Wakati wa karne ishirini na tano za kwanza za historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa (Musa aliishi miaka 2500 hivi baada ya Adamu kuumbwa, na ndiye mwandishi wa kwanza). Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na maarifa haya yalipitishwa kutoka kwa baba kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vilivyofuatana. Maandalizi ya Neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa.

Mafunuo yaliyovuviwa yalijumuishwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa muda mrefu kipindi cha miaka elfu na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na Sheria, hadi Yohana, mwandishi wa Kweli kuu za injili (takribani Kutoka 1500 KK hadi 100 BK).

Biblia inaelekeza kwa Mungu kama mwandishi Wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa mtindo wake tofauti vitabu vyake mbalimbali vinawasilisha sifa za waandishi kadhaa. Kweli zilizofunuliwa zote "hutolewa kwa pumzi ya Mungu" (2 Timotheo 3:16); lakini zinaonyeshwa kwa maneno ya wanadamu, kwani si imla, ila walipewa njozi na ndoto na wakaandika kwa maneno yao. Roho Mtakatifu ametoa nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, alama na takwimu; na wale waliofunuliwa Kweli hizi, wameonyesha wenyewe mawazo hayo katika lugha ya kibinadamu.

Amri kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na ziliandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Amri Kumi ni za Mungu Mwenyewe. Tunatakiwa tuwe waangalifu sana, kwani amri za mataifa yetu tunazitilia maanani, na tunapozivunja tunapata shida, sembuse Amri za Mwenyezi Mungu? Hakuna awezaye kushika sheria na kutembea na

Mwenyezi Mungu isipokuwa amepata msaada kutoka Kwake, na Kila mwanadamu aombaye msaada huo, Mungu Yupo tayari kumpa.

Unabii 351 wa Agano la Kale Uliotimizwa Katika Yesu Krist

Unabii---------------

Maelezo------------

Utimilifu------------

1. Mwa 3:15 Mbegu au Uzao wa mwanamke (kuzaliwa na bikira)- Wagalatia 4:4-5; Mathayo 1:18

2. Mwa 3:15 Atamponda kichwa Shetani- Waebrania 2:14; 1 Yohana 3:8

3. Mwa 5:24 Kupaa mbinguni kimwili kulionyeshwa- Marko 16:19

4. Mwa 9:26-27 Mungu wa Shemu atakuwa Mwana wa Shemu- Luka 3:36

5. Mwa 12:3 Uzao wa Ibrahimu utabariki mataifa yote-Wagalatia 3:8; Matendo 3:25-26

6. Mwa 12:7 Ahadi Iliyotolewa kwa Uzao wa Ibrahimu- Wagalatia 3:16

7. Mwa 14:18 Kuhani kwa mfano wa Melkizedeki -Waebrania 6:20

8. Mwa 14:18 Mfalme wa Amani na Haki- Waebrania 7:2

9. Mwa 14:18 Karamu ya Mwisho ilitabiri- Mathayo 26:26-29

10. Mwa 17:19 Uzao wa Isaka (Mwa 21:12)- Warumi 9:7

11. Mwa 22:8 Mwana-Kondoo wa Mungu aliyeahidiwa- Yohana 1:29

12. Mwa 22:18 Kama uzao wa Isaka, atabariki mataifa yote- Wagalatia 3:16

13. Mwa 26:2-5 Uzao wa Isaka ulioahidiwa kama Mkomboz-i Waebrania 11:18

14. Mwa 28:12 Daraja la kwenda mbinguni -Yohana 1:51

15. Mwa 28:14 Uzao wa Yakobo -Luka 3:34

16. Mwa 49:10 Wakati wa kuja Kwake- Luka 2:1-7; Gal 4:4

17. Mwa 49:10 Uzao wa Yuda- Luka 3:33

18. Mwa 49:10 Aliyeitwa Shilo au Aliyetumwa- Yohana 17:3

19. Mwa 49:10 Masihiaja kutoka kabila ya Yuda kupoteza utambulisho- Yohana 11:47-52

20. Mwa 49:10 Utii wa watu utakuwa Kwake- Yohana 10:16

21. Kutoka 3:13-15 "MIMI NIKO" Mkuu-Yohana 4:26; 8:58

22. Kutoka 12:5 Mwana-Kondoo asiye na dosari -Ebr 9:14; 1 Pet 1:19

23. Kutoka 12:13 Damu ya Mwana-Kondoo huokoa kutoka kwa ghadhabu -Rum 5:8

24. Kutoka 12:21-27 Kristo Ndiye Pasaka yetu- 1 Kor 5:7

25. Kutoka 12:46 Hakuna mfupa wa Mwana-Kondoo utakaovunjwa -Yohana 19:31-36

26. Kutoka 15:2 Kuinuliwa Kwake kulitabiriwa kama Yeshua -Matendo 7:55-56

27. Kutoka 15:11 Tabia Yake-Utakatifu- Luka 1:35; Matendo 4:27

28. Kutoka 17:6 Mwamba wa Kiroho wa Israeli- 1 Kor 10:4

29. Kutoka 33:19 Tabia Yake-Mtu Mwenye Huruma -Luka 1:72

30. Mambo ya Walawi 1:2-9 Sadaka Yake yenye harufu nzuri kwa Mungu- Efe 5:2

31. Mambo ya Walawi 14:11 Mwenye ukoma kusafishwa-Ishara ya ukuhani- Luka 5:12-14; Matendo 6:7

32. Law 16:15-17 Atakufa kifo cha mara moja cha Kristo, siyo kama dhabihu kila siku- Ebr 9:7-14

33. Law 16:27 Atateseka nje ya Kamb-i Mathayo 27:33; Ebr. 13:11-12

34. Law 17:11 Damu - uhai wa mwili- Mathayo 26:28; Marko 10:45

35. Law 17:11 Ni damu inayofanya upatanisho- Rum. 3:23-24; 1 Yohana 1:7

36. Law 23:36-37 Sadaka ya Kinywaji: “Mtu akiona kiu”- Yohana 7:37

37. Hesabu 9:12 Hakuna mfupa Wake uliovunjwa- Yohana 19:31-36

38. Hesabu 21:9 Kama Nyoka juu ya mti - Kristo aliinua- Yohana 3:14-18; 12:32

39. Hesabu 24:17 Wakati huo: “Nitamwona, lakini si sasa.”- Yohana 1:14; Gal 4:4

40. Kumb 18:15 “Kweli Huyu ni Nabii Yule”- Yohana 6:14

41. Kumb 18:15-16 “Kama mngalimwamini Musa, mngaliniamini Mimi.-” Yohana 5:45-47

42. Kumb 18:18 Aliyetumwa na Baba kusema Neno Lake- Yohana 8:28-29

43. Kumb 18:19 Yeyote asiyesikiliza lazima abebe dhambi Yake- Matendo 3:22-23

44. Kumb 21:23 Amelaaniwa aangikwaye juu ya mti-- Gal 3:10-13

45. Yoshua 5:14-15 Kapteni wa wokovu wetu -Ebr 2:10

46. Ruthu 4:4-10 Kristo, Ndugu yetu, ametukomboa- Efe 1:3-7

47. 1 Sam 2:35 Kuhani Mwaminifu -Ebr 2:17; 3:1-3, 6; 7:24-25

48. 1 Sam 2:10 Atakuwa Mfalme aliyepakwa mafuta kwa Bwana- Mathayo 28:18; Yohana 12:15

49. 2 Sam 7:12 Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1

50. 2 Sam 7:13 Ufalme Wake ni wa milele -2 Pet 1:11

51. 2 Sam 7:14a Mwana wa Mungu- Luka 1:32; Rum 1:3-4

52. 2 Sam 7:16 Nyumba ya Daudi ilianzishwa milele- Luka 3:31; Ufu 22:16

53. 2 Wafalme 2:11 Kupaa mbinguni kimwili kuliashiria- Luka 24:51

54. 1 Nyakati 17:11 Uzao wa Daudi- Mathayo 1:1; 9:27

55. 1 Nyakati 17:12-13Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi milele- Luka 1:32-33

56. 1 Nyakati 17:13 “Nitakuwa Baba Yake, Yeye…Mwanangu.”- Ebr 1:5

57. Ayubu 9:32-33 Mpatanishi kati ya mwanadamu na Mungu -1 Tim 2:5

58. Ayubu 19:23-27 Ufufuo ulitabiriwa- Yohana 5:24-29

59. Zaburi 2:1-3 Uadui wa wafalme uliopangwa tangu mwanzo- Matendo 4:25-28

60. Zaburi 2:2 Kumiliki cheo, Mpakwa Mafuta (Kristo)- Yohana 1:41; Matendo 2:36

61. Zaburi 2:6 Tabia Yake-Utakatifu- Yohana 8:46; Ufu 3:7

62. Zaburi 2:6 Kumiliki cheo Mfalme -Mathayo 2:2

63. Zaburi 2:7 Alimtangaza Mwana Mpendwa- Mathayo 3:17; Warumi 1:4

64. Zaburi 2:7-8 Kusulubiwa na Kufufuka kulielezea- Matendo 13:29-33

65. Zaburi 2:8-9 Atatawala mataifa kwa fimbo ya chuma- Ufunuo 2:27; 12:5; 19:15

66. Zaburi 2:12 Uzima huja kwa imani katika Yeye- Yohana 20:31

67. Zaburi 8:2 Vinywa vya watoto wachanga hukamilisha sifa zake- Mathayo 21:16

68. Zaburi 8:5-6 Kudhalilishwa na kuinuliwa kwake- Ebr 2:5-9

69. Zaburi 9:7-10 Atahukumu ulimwengu kwa haki- Matendo 17:31

70. Zaburi 16:10 Hakutaka kuona uharibifu- Matendo 2:31; 13:35

71. Zaburi 16:9-11 Angefufuka kutoka kwa wafu- Yohana 20:9

72. Zaburi 17:15 Ufufuo ulitabiriwa- Luka 24:6

73. Zaburi 18:2-3 Pembe ya wokovu- Luka 1:69-71

74. Zaburi 22:1 Kuachwa kwa sababu ya dhambi za wengine- 2 Kor 5:21

75. Zaburi 22:1 “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?”- Mathayo 27:46

76. Zaburi 22:2 Giza juu ya Kalvari kwa saa tatu- Mathayo 27:45

77. Zaburi 22:7 Wanapiga kelele na kutikisa kichwa- Mathayo 27:39-44

78. Zaburi 22:8 “Alimtumaini Mungu, na amwokoe”- Mathayo 27:43

79. Zaburi 22:9-10 Alizaliwa Mwokozi- Luka 2:7

80. Zaburi 22:12-13 Wanatafuta kumwuua- Yohana 19:6

81. Zaburi 22:14 Damu Yake ilimwagika walipomchoma ubavuni- Yohana 19:34

82. Zaburi 22:14-15 Aliteseka sana pale Kalvari-Mark 15:34-37

83. Zaburi 22:15 Aliona kiu -Yohana- 19:28

84. Zaburi 22:16 Wamtoboa mikono na miguu- Yohana 19:34-37; 20:27

85. Zaburi 22:17-18 Walimvua nguo zake mbele ya macho ya watu- Luka 23:34-35

86. Zaburi 22:18 Waligawanya mavazi Yake- Yohana 19:23-24

87. Zaburi 22:20-21 Alijikabidhi kwa Mungu- Luka 23:46

88. Zaburi 22:20-21 Nguvu za Shetani zikimchubua Mkombozi kisigino- Ebr 2:14

89. Zaburi 22:22 Ufufuo Wake ulitangazwa- Yohana 20:17

90. Zaburi 22:27-28 Atakuwa mtawala wa mataifa- Kol 1:16

91. Zaburi 22:31 “Imekwisha”- Yohana 19:30; Ebr 10:10-12, 14, 18

92. Zaburi 23:1 “Mimi Ndimi Mchungaji Mwema”- Yohana 10:11; 1 Pet 2:25

93. Zaburi 24:3 Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Wafilipi 2:9

94. Zaburi 30:3 Ufufuo Wake ulitabiri- Matendo 2:32

95. Zaburi 31:5 “Mikononi Mwako naiweka roho Yangu”- Luka 23:46

96. Zaburi 31:11 Marafiki Zake walimkimbia- Marko 14:50

97. Zaburi 31:13 Wakafanya shauri la kumwua- Mathayo 27:1; Yohana 11:53

98. Zaburi 31:14-15 “Alimtumaini Mungu, sasa na amwokoe”- Mathayo 27:43

99. Zaburi 34:20 Hakuna hata mfupa Wake uliovunjika- Yohana 19:31-36

100. Zaburi 35:11 Mashahidi wa uongo walisimama dhidi Yake- Mathayo 26:59

101. Zaburi 35:19 Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

102. Zaburi 38:11 Marafiki Zake walisimama mbali- Luka 23:49

103. Zaburi 38:12 Maadui walijaribu kumnasa kwa hila- Marko 14:1; Mathayo 22:15

104. Zaburi 38:12-13 alikaa kimya mbele ya washtaki Wake- Mathayo 27:12-14

105. Zaburi 38:20 Alizunguka-zunguka akitenda mema -Matendo 10:38

106. Zaburi 40:2-5 Furaha ya ufufuo Wake ilitabiriwa- Yohana 20:20

107. Zaburi 40:6-8 Furaha Yake—mapenzi ya Baba- Yohana 4:34; Ebr 10:5-10

108. Zaburi 40:9 Alipaswa kuhubiri Haki katika Israeli- Mathayo 4:17

109. Zaburi 40:14 Kukabiliwa na maadui katika Bustani- Yohana 18:4-6

110. Zaburi 41:9 Kusalitiwa na rafiki anayemfahamu- Yohana 13:18

111. Zaburi 45:2 Maneno ya Neema yanatoka midomoni Mwake- Yohana 1:17; Luka 4:22

112. Zaburi 45:6 Kumiliki cheo, Mungu au Elohim- Ebr 1:8

113. Zaburi 45:7 Upako maalum wa Roho Mtakatifu- Math 3:16; Ebr 1:9

114. Zaburi 45:7-8 Anayeitwa Kristo (Masihi au Mpakwa Mafuta)- Luka 2:11

115. Zaburi 45:17 Jina Lake likumbukwe milele- Efe 1:20-21; Ebr 1:8

116. Zaburi 55:12-14 Alisalitiwa na rafiki, si adui- Yohana 13:18

117. Zaburi 55:15 Kifo kisichotubu cha Msaliti- Math 27:3-5; Matendo 1:16-19

118. Zaburi 68:18 Kuwapa wanadamu zawadi- Waefeso 4:7-16

119. Zaburi 68:18 Alipaa Mbinguni- Luka 24:51

120. Zaburi 69:4 Alichukiwa bila sababu- Yohana 15:25

121. Zaburi 69:8 Mgeni kwa ndugu Zake- Yohana 1:11; 7:5

122. Zaburi 69:9 Mwenye Bidii kwa Nyumba ya Bwana- Yohana 2:17

123. Zaburi 69:14-20 Uchungu wa Masihi wa roho kabla ya kusulubiwa- Mathayo 26:36-45

124. Zaburi 69:20 “Nafsi Yangu ina huzuni nyingi”- Mathayo 26:38

125. Zaburi 69:21 Aliyepewa siki alipokuwa na kiu- Mathayo 27:34

126. Zaburi 69:26 Mwokozi Alitolewea kafara na kupigwa na Mungu -Yohana 17:4; 18:11

127. Zaburi 72:10-11 Watu wakuu wangemtembelea- Mathayo 2:1-11

128. Zaburi 72:16 Chembe ya ngano kuanguka ardhini- Yohana 12:24-25

129. Zaburi 72:17 Imani katika Jina Lake itazaa watoto- Yohana 1:12-13

130. Zaburi 72:17 Mataifa yote yatabarikiwa Naye- Gal 3:8

131. Zaburi 72:17 Mataifa yote yatamwita mbarikiwa- Yohana 12:13; Ufunuo 5:8-12

132. Zaburi 78:1-2 Angefundisha kwa mifano- Mathayo 13:34-35

133. Zaburi 78:2b Kutangaza Hekima ya Mungu kwa mamlaka- Mathayo 7:29

134. Zaburi 80:17 Mkono wa kuume wa Mtu wa Mungu- Marko 14:61-62

135. Zaburi 88 Mateso na Laana ya Kalvari- Mathayo 27:26-50

136. Zaburi 88:8 Walisimama mbali na kumtazama- Luka 23:49

137. Zaburi 89:27 Mzaliwa wa kwanza- Kol 1:15-18

138. Zaburi 89:27 Imanueli ni mkuu kuliko wafalme wa kidunia- Luka 1:32-33

139. Zaburi 89:35-37 Uzao wa Daudi, kiti cha enzi, ufalme wadumu milele- Luka 1:32-33

140. Zaburi 89:36-37 Tabia Yake-Uaminifu- Ufu 1:5; 19:11

141. Zaburi 90:2 Yeye ni wa milele- (Mika 5:2) Yohana 1:1

142. Zaburi 91:11-12 Alitambuliwa kama Masihi, Kristo atajaribiwa- Luka 4:10-11

143. Zaburi 97:9 Kuinuliwa Kwake kulitabiri- Matendo 1:11; Efe 1:20

144. Zaburi 100:5 Tabia Yake-Wema Mathayo- 19:16-17

145. Zaburi 102:1-11 Mateso na Lawama za Kalvari- Yohana 19:16-30

146. Zaburi 102:25-27 Masihi Ndiye Mwana Aliyekuwepo Zamani- Waebrania 1:10-12

147. Zaburi 109:25 Alidhihakiwa- Mathayo 27:39

148. Zaburi 110:1 Mwana wa Daudi- Mathayo 22:42-43

149. Zaburi 110:1 Apaa hadi mkono wa kuume wa Baba- Marko 16:19

150. Zaburi 110:1 Mwana wa Daudi aitwaye Bwana- Mathayo 22:44-45

151. Zaburi 110:4 Kuhani kwa utaratibu wa Melkizedeki- Waebrania 6:20

152. Zaburi 112:4 Tabia Yake-Mwenye Huruma, Neema, et al- Mathayo 9:36

153. Zaburi 118:17-18 Ufufuo wa Masihi wahakikishwa -Luka 24:5-7; 1 Kor 15:20

154. Zaburi 118:22-23 Jiwe lililokataliwa ni Msingi wa pembeni mwa jengo -Mathayo 21:42-43

155. Zaburi 118:26a Aliyebarikiwa awasilishwa kwa Israeli- Mathayo 21:9

156. Zaburi 118:26b Atakuja Hekaluni, likiwa limesimama- Mathayo 21:12-15

157. Zaburi 132:11 Uzao wa Daudi (tunda la Mwili Wake)- Luka 1:32; Matendo 2:30

158. Zaburi 129:3 Alipigwa mijeledi -Mathayo 27:26

159. Zaburi 138:1-6 Ukuu wa Uzao wa Daudi wawashangaza wafalme- Mathayo 2:2-6

160. Zaburi 147:3-6 Huduma ya Kristo duniani ilielezewa- Luka 4:18

161. Mithali 1:23 Atatuma Roho wa Mungu -Yohana 16:7

162. Mithali 8:23 Aliyechaguliwa tangu milele -Ufunuo 13:8; 1 Pet 1:19-20

163. Wimbo 5:16 Yule bora kabisa- Yohana 1:17

164. Isaya 2:3 Atawafundisha mataifa yote- Yohana 4:25

165. Isa 2:4 Atahukumu miongoni mwa mataifa -Yohana 5:22

166. Isa 6:1 Isaya alipoona utukufu Wake -Yohana 12:40-41

167. Isa 6:8 Aliyetumwa na Mungu -Yohana 12:38-45

